NAKALA YA MTANDAO

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Pili - Tarehe 20 Aprili, 2016

*(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

### HATI ZA KUWASISLISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 *(The 2nd National Five Year Development Plan, 2016/2017 – 2020/2021).*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti juu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 hadi mwaka 2020/2021.

**NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Maswali.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 11

### Ahadi ya Kupeleka Gari la Wagonjwa Katika Kituo cha Afya Mgololo

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Serikali iliahidi kupeleka gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Mgololo lakini hadi sasa gari hilo halijapelekwa:-

Je, ni lini gari hilo litapelekwa ili liweze kusaidia Vijiji vya Idete, Itika, Holo, Isaula, Rugema, Makungu, Rugolofu na Kitasengwa?

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ina gari moja linalotumika kuhudumia wagonjwa. Hata hivyo, gari hilo ni chakavu kiasi cha kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Halmashauri inapaswa kuweka kipaumbele na kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa kwa kuzingatia mahitaji yaliyopo. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Halmashauri imeomba shilingi milioni 543.0 kwa ajili ya kununua magari matatu *(ambulance)* ambapo kati ya hayo gari moja litapelekwa katika Kituo cha Afya Mgololo na mengine katika Vituo vya Afya vya Sadani na Kasanga ili yasaidie kuwafikisha wagonjwa wenye dharura kwenye vituo vya kutolea huduma kwa haraka.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigola, swali la nyongeza!

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri, lakini pamoja na majibu yake Naibu Waziri kwamba hili gari kwenye bajeti ya mwaka 2013/2014 na swali la msingi niliuliza mwezi wa Tisa na kwenye bajeti walisema kwamba wametenga milioni 150 kwa ajili ya ununuzi wa hili gari la wagonjwa wa kule Mgololo, mpaka leo hili gari halijapelekwa. Niliwahi kumuuliza Waziri wa Afya akaniambia kwamba kuna magari matano

yamenunuliwa mojawapo litapelekwa kule, lakini mpaka leo halijakwenda. Je, bajeti ya mwaka uliopita ambayo ilitengwa kwa ajili ya hilo gari, hiyo fedha ya shilingi milioni 150 ilikwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hii gari ni ya msingi sana, kwa sababu itahudumia Kata tatu, kuna ya Kiyowela, Kata ya Idete na Kata ya Makungu. Kule kuna watu wanakaribia karibu 120,000 hivi, akinamama wanapata taabu sana kuna milima, jiografia ya kule ni ngumu sana. Sasa naomba Mheshimiwa Naibu Waziri anithibitishie kwa sababu hii pesa ya Halmashauri haina uhakika, ni lini hii gari hili la wagonjwa litapelekwa Mufindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI!

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri wazi kwamba nilifika Mufindi katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge mpaka Mgogolo. Hili ni miongoni mwa Jimbo ambalo lina changamoto kubwa kutokana na jiografia yake ilivyo. Hata hivyo, nipende kumshukuru pia kwa juhudi kubwa anayofanya katika kuhakikisha mambo yanakwenda katika Jimbo lake kwa sababu katika miaka mitano iliyopita alikuwa akipigania mambo mbalimbali katika maeneo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la msingi la kwanza aliposema bajeti ya mwaka ilitengwa lakini haikupatikana ni kweli, na nyinyi mnafahamu sio bajeti ya *ambulance* peke yake, isipokuwa miradi mingi sana ya maendeleo katika kipindi kilichopita, imekumbwa na changamoto kubwa sana hasa ya upelekaji wa fedha. Maombi haya yalikuwa ni katika maombi maalum, hivyo ni imani yangu kwamba katika bajeti ya mwaka huu sasa kwa vile jiografia yake inajulikana, Ofisi ya Rais - TAMISEMI tutaweka kipaumbele kuhakikisha gari hilo linapatikana. Kikubwa zaidi katika hayo yote maana yake maombi maalum wakati mwingine yana changamoto kubwa sana na sana sana zinalenga katika *collection* ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote tushikamane kwa pamoja kuisaidia nchi yetu ili tupate mapato ya kutosha, yale maombi maalum yote tuliyoyapeleka, Serikali iweze kuona ni jinsi gani yatayafanyiwa kazi.

Sehemu ya pili, ni kwamba ni lini gari litapatikana, nimesema kwamba, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa sababu tunaguswa na hili, katika uongozi wetu wa sasa tutapambana kwa kadri iwezekanavyo. Ndugu yangu wa Mufindi tujitahidi kwa pamoja Mungu akijalia tutapata gari, naomba amini Ofisi yako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, sasa aulize swali lake.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijauliza swali napenda niwajulishe ndugu zangu na wananchi wa Jimbo la Kavuu kwamba, sijasimamishwa shughuli za Bunge. Sasa naomba swali langu Na. 12 lipatiwe majibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pudenciana haturuhusiwi kufanya hivyo kwa mujibu wa Kanuni, tafadhali uliza swali lako.

Mheshimiwa Pudenciana uliza swali lako.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba swali langu namba 12 lipatiwe majibu.

Na.12

**Hitaji la Maji Safi na Salama – Kata ya Jimbo la Kavuu**

**MHE.DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Kata ya Mamba, Majimoto, Chamalema na Mwamapuli zitapatiwa maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, Mbunge wa Kavuu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua tatizo la maji katika Kata ya Mamba, Serikali imetenga shilingi milioni 24.2 katika bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa ajili ya kuchimba kisima kirefu katika Kijiji cha Ntaswa ambacho hakina maji, kati ya vijiji nane vilivyopo. Aidha, kwenye Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Maji Awamu ya Pili, zimetengwa shilingi milioni 650 ili kupanua mradi mserereko kutoka Kilida hadi Ntaswa na Kisansa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo havijapata huduma ya maji katika Kata ya Majimoto ni Luchima na Ikulwe ambavyo vimetengewa shilingi milioni 48.4 katika bajeti ya mwaka 2015/2016 kwa ajili ya kuchimba visima virefu katika kila kijiji. Vijiji vilivyobaki vinapata maji kupitia mradi uliogharimu shilingi milioni 526,8 na umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka 2015/2016, zimetengwa milioni 48.4 kwa ajili ya kuchimba visima viwili katika Vijiji vya Chamalendi na Mkwajuni, vilivyopo Kata ya Chamalendi ili kutatua tatizo la maji kwa wananchi maeneo hayo. Katika Kata ya Mwamapuli Vijiji vyenye matatizo ya maji ni Mwamapuli Ukigwaminzi na Lunguya ambavyo vimetengewa shilingi milioni 77.4 ambapo vitachimbwa visima virefu vitatu vya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikwembe swali la nyongeza!

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pia nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nasikitika kwamba, pesa hizi ni za bajeti ambayo tunakwenda kumalizia, naomba nijue ni lini pesa hizi zitatoka ziende zikafanye kazi hiyo kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili, kwa uzoefu unavyojionesha pesa hizi zinaweza zikatoka mwisho wa bajeti yaani Juni 30. Je, pesa hizi zinapotoka zinakwenda wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI!

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, pesa hizi ni za bajeti ya mwaka huu 2015/2016, lakini kama nilivyojibu awali, miradi mingi sana ya maji katika kipindi hiki toka tunapotoka katika mwaka wa uchaguzi mpaka hivi sasa, ni miradi mingi sana siyo katika Jimbo la Kavuu peke yake, isipokuwa miradi mingi sana imekuwa ikisuasua kutokana na upelekaji wa fedha. Hata hivyo Serikali imefanya juhudi kubwa sana mara baada ya kukusanya mapato makubwa Serikalini kuhakikisha kwamba maeneo mbalimbali ambayo miradi ilikuwa imesimama sasa ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba Wizara ya Maji kwa kupitia Wizara ya Fedha, maeneo mbalimbali ambayo miradi mingine ilikwama sasa hivi imeshaanza kufanya kazi. Imani yangu kubwa iliyoko ni kwamba Ndugu yangu Mbunge ambaye najua siku zote ulikuwa ukipambana Jimboni kwako katika maeneo haya, kwa kipindi hiki tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo, Serikali iweze kupeleka maeneo yote ambayo miradi ilisimama ilimradi, miradi ikamilike katika mwaka huu wa fedha,

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, hata katika ripoti za Mkaguzi wa Serikali kuna miradi mingine inakwama kwa sababu fedha zinafika mwishoni. Kwa hiyo, niwaombe hasa ma-*engineer* wetu kule *site* kwamba, wajipange vizuri kiasi kwamba pesa hii itakapofika wahakikishe usimamizi unakwenda kwa haraka ilimradi wananchi wa Jimbo la Kavuu waweze kupata huduma za maji katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mlata!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa hapa Bungeni tumekuwa tukipitisha fedha nyingi sana kwa ajili ya kwenda kutatua matatizo ya maji kule vijijini ikiwemo Mkoa wa Singida, lakini yamekuwa ni mazoea kwamba ma-*engineer* wanakwenda kuchimba maji maeneo ambapo hakuna maji ya kutosha na hivyo fedha nyingi kupotea.

Je, Serikali ni lini itakuja kutuletea idadi ya fedha ambazo zimepotezwa kwa sababu ya ma-*engineer* kwenda kuchimba maji kwenye maeneo ambayo hakuna maji matokeo yake wananchi wanaendelea kuteseka na adha za maji? Ni lini Serikali itatuletea *figures* hizo? Asante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI. Samahani Naibu Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Maji anataka kujibu. Waziri wa Maji, karibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji chini ya ardhi ni gumu sana na tuchukulie mfano Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora ulifanyiwa *study* na Wajapani na waka-*confirm* kwamba chini kuna maji, lakini wamekwenda kuchimba maji yamekosekana kutokana na mfumo wenyewe wa miamba chini ya ardhi. Kwa sasa Wizara ya Maji imetengeneza utaratibu mpya kwamba, *study* ya maji pamoja na uchimbaji utafanywa na mtu mmoja. Kitu tulichokiona ni kwamba, *study* inafanywa na Mhandisi Mshauri, anayekuja kuchimba ni mwingine na unakuta tunapoteza pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kitu tulichokifanya sasa hivi kwamba, pale tutakapotoa fedha kwa ajili ya kuchimba visima tunatafuta Mkandarasi mmoja na huyo huyo ndiyo anafanya *study*. Ili akifanya *study* akichimba kama maji hayakupatikana basi pesa hatutamlipa na kuhakikisha kwamba huo upotevu wa pesa unakuwa haupatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye hoja ya pili, tutafanya tafiti na tutatoa taarifa kwenye Bunge hili kuona ni fedha kiasi gani ambazo zimepotea baada ya huo utaratibu wa kuchimba visima na maji hayapatikani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Albert Ntabaliba Obama, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake!

Na. 13

**Fedha Zilizotolewa kwa Ajili ya Kutoa Huduma za Afya kwa Makundi Maalum**

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA (K.n.y. MHE. ALBERT O. NTABALIBA)** aliuliza:-

Mwaka 2011/2012 tuliweka Mkataba kati ya Halmashauri ya Buhigwe na Hospitali ya *Heri Mission,* Biharu Hospitali na *Mulera Dispensary* juu ya kutoa huduma ya matibabu kwa wazee, watoto na akinamama bure na Serikali imetoa fedha hizo na wananchi wamenufaika na huduma hizo lakini tangu Disemba, 2015 hadi sasa fedha hazitolewi tena:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali imeacha kutoa fedha ilizokuwa ikitoa?

(b) Je, ni lini sasa fedha hizo zitaanza tena kutolewa ili huduma hizo ziendelee?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI!

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Ntabaliba Obama, Mbunge wa Buhigwe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe inatakiwa kuchangia 15% ya fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya katika Hospitali Teule ya *Heri Mission*, Kituo cha Afya Biharu na Zahanati ya Mulera. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016, robo ya kwanza na ya pili hadi Disemba, 2015 tayari zimepelekwa shilingi milioni 27.5 katika Hospitali Teule ya *Heri Mission,* shilingi milioni 8.0 zimepelekwa katika Kituo cha Afya cha Biharu na shilingi milioni 8.0 zimepelekwa Zahanati ya Mulera. Fedha ambazo hazijapelekwa ni za robo tatu (Januari – Machi, 2016) na robo ya nne (Aprili – Juni, 2016) kutokana na kutopokelewa kwa fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya kutoka Hazina.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu hili, fedha ambazo hazijapelekwa katika vituo hivyo vya kutolea huduma za afya ni za robo ya tatu na robo ya nne ambazo zitapelekwa baada ya Halmashauri kupokea fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Busket Fund*) kutoka Hazina. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri kuimarisha usimamizi kwa kushirikiana na wamiliki binafsi wa hospitali ili makundi yanayotakiwa kutibiwa bure waweze kupata huduma hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Obama, swali la nyongeza!

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Niliuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Obama mimi mwenyewe naitwa Dkt. Hadji Mponda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa mkataba kati ya Halmashauri ya Buhigwe na ile Hospitali ya *Mission* umesitishwa kwa sababu ya fedha, sasa ni nini Serikali wana njia mbadala ya kutoa huduma za afya bure kwa makundi haya ya wazee na watoto?

Swali la pili, mkataba kama huo huo uliofanyika Buhigwe na mwaka 2011 - 2013 ulifanyika katika Wilaya ya Ulanga ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga waliingia mkataba na Hospitali ya Lugala, ni Hospitali ya *Mission,* lakini mkataba ule ulidumu kwa muda wa miezi sita mpaka leo umesitishwa. Sasa swali langu ni lini Halmashauri hiyo ya Malinyi pamoja na TAMISEMI wataufufua mkataba ule kwa kurudisha huduma hizi bure kwa makundi haya mawili ya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano?

**NAIBU WAZIRI WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza katika sehemu ya (a) ni kwamba nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, mkataba huu haujasitishwa, kilichotokea ni kwamba kuna fedha za *quarter* ya kwanza ambayo imekuja mpaka mwezi Disemba ambapo tunarajia sasa kuna pesa zingine zitakuja mpaka hivi sasa na nimesema pale mwanzo kwamba matarajio zile pesa zikishafika Halmashauri, basi lazima zielekezwe katika sehemu hizi tatu ilimradi wananchi waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili, kwa sababu hili ni suala la Hospitali ya *Lugala Mission* sijakuwa na taarifa nayo za kutosha, lakini nina imani kwamba mikataba yote kilichozingatiwa ni kwamba, inakwenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezekano ni kwamba naomba nishauri hasa Baraza la Madiwani hasa katika vikao vyao vya Kamati ya Fedha. Lazima fedha zinapokuja, wasimamie fedha hizi maelekezo yake ni wapi, kwa sababu sehemu zingine inawezekana fedha zikapita lakini watu katika kufanya maamuzi wakaelekeza pesa sehemu ambazo siyo muafaka mwisho wake wakati mwingine mikataba inavunjika wakati kumbe kuna watu hawajatimiza majukumu yao. Imani yangu ni kwamba, kila mtu atatimiza wajibu wake ilimradi wananchi wetu waweze kupata huduma bora kwa ajili ya kuhakikisha afya ya mama na mtoto inaimarika katika nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, sasa aulize swali lake. Mheshimiwa Suzan Lyimo!

Na. 14

**Karo Elekezi kwa Shule Binafsi**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Serikali ilitoa kauli kuwa itapanga gharama za karo elekezi kwa shule zote za binafsi hapa nchini:-

(a) Je, Serikali imegundua kiwango cha gharama kwa kila mwanafunzi *(unit cost)* kwa shule za bweni na za kutwa ni kiasi gani?

(b) Je, kiwango hiki hakitasababisha kuporomoka kwa ubora wa elimu ambayo ilikuwa ikitolewa hapo awali na shule binafsi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi imefanya utafiti kuhusu gharama za kumsomesha mwanafunzi wa elimu ya msingi na sekondari. Kupitia utafiti huo, imebainika kuwa ada zinazotozwa katika shule za binafsi zinatofautiana kwa kiasi kikubwa kulingana na huduma zinazotolewa, aina ya shule na miundombinu iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utafiti huo, Wizara yangu ilifanya mazungumzo na baadhi ya taasisi zinazosimamia shule zisizo za Kiserikali na kukubaliana namna ya kufikia viwango vya ada elekezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi ambazo tumefanya nazo mazungumzo ni pamoja na Umoja wa Wamiliki na Mameneja wa Shule na Vyuo visivyo vya Serikali *(TAMONGSCO)*, Kamisheni ya Huduma za Jamii za Kikristo *(CSSC)* na Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA). Kutokana na tofauti za ubora na idadi ya huduma zinazotolewa na shule, Wizara sasa imeanza zoezi la kupanga shule hizi kwa makundi ili kuweka viwango vya ada kwa kuzingatia ubora na huduma na hivyo kutoathiri kiwango cha elimu inayotolewa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inatarajia kuwa utaratibu wa ada elekezi hautaathiri ubora wa elimu katika shule binafsi kwa sababu ada hiyo itapangwa kulingana na ubora na huduma na miundombinu iliyopo shuleni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo, swali la nyongeza!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa nafasi na nasikitika sana kwa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi (CCM) iliyoruhusu kufanya elimu kuwa *commodity*, kuwa biashara. Pia ni Serikali hii hii inayoleta ada elekezi na kwamba utafiti umefanyika na wamebaini kwamba shule zinatofautiana. Hapakuwa na haja ya utafiti kwa sababu inajulikana shule hizi zinatofautiana. Sasa swali langu ni kwamba wanipe sababu ni kwa nini wanataka shule hizi za binafsi ziwe na ada elekezi huku wakijua kabisa kwamba shule hizi zinatofautiana ubora na ni wazi hata katika matokeo ya mitihani kwa muda wa miaka 10 mfululizo shule hizi zinaongoza? Watupe sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka kujua Serikali haioni kwamba shule hizi ada inakuwa kubwa kwa sababu kubwa moja tu, kwamba kuna tozo nyingi, kwa mfano wanalipa *property tax,* lakini vilevile kwenye suala la ukaguzi, wakati shule za Serikali wanalipa chini ya shilingi 3,000, hawa kila mwanafunzi anapaswa kulipa shilingi 5,000 ya ukaguzi. Je, ni lini Serikali itaondoa tozo kwenye shule hizi ili ada yao iweze kuwa kidogo na ili wazazi waweze lakini pia kwa nini msiboreshe shule zenu za Serikali ili wazazi waweze kuwapeleka kwenye shule za Serikali kwa sababu hakuna mwananchi yeyote asiyependa bure? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kusema, pamoja na kwamba elimu imekuwa ikitolewa kwa kushirikiana na taasisi binafsi na pamoja na kwamba kumekuwa na *element* ya biashara, lakini lazima tuzingatie kwamba elimu siyo biashara *per se*, elimu ni haki ya kila Mtanzania na si mwenye uwezo tu wa fedha ndiyo anayestahili kupata elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na dhana hiyo, kumekuwa na wazazi wengi ambao wangetamani kupeleka watoto wao katika shule mbalimbali, lakini wakati huo huo kumekuwa na ada za aina tofauti tofauti wakati mwingine si halisia kulinganisha na uwekezaji uliofanyika.

Hata hivyo, dhana kubwa ya uwekezaji ni pamoja na mwekezaji kuja na mtaji na si tu kuwekeza kwa kutegemea mtaji ule unaokusanywa kutokana na ada za wanafunzi kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, kutokana pia na kilio kutoka kwa wananchi wengi na hilo si tu kwamba litakuwa linafanyika kwa mara ya kwanza kwa Wizara yetu ya Elimu, bali pia limekuwa likifanyika katika maeneo mbalimbali ikiwemo mafuta kwa mfano *EWURA*, wamekuwa wakipanga bei kutegemeana na uhalisia ili bei zinazotozwa zilingane na uhalisia. Kwa misingi hiyo ndiyo maana tumeona kuna umuhimu wa kushirikisha wadau wengi ili kupata bei ambayo haitaathiri utoaji wa huduma, lakini wakati huo kuwawezesha wananchi wengi zaidi kufaidika na sera hii nzuri ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, pamoja na jitihada kubwa inayofanywa na Serikali ya kuhakikisha kwamba shule zake za Serikali zinaboreshwa, ikiwemo shukrani kubwa kwa Bunge kupeleka Shilingi bilioni sita kwa ajili ya Madawati, hiyo ni sehemu ya kuboresha elimu katika shule za msingi, napenda tu niseme kwamba, sehemu za tozo ambazo zimekuwa zikitozwa zinaendana na uhalisia. Kwa misingi hiyo, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge kukaa katika viatu vya wananchi ambao wapo na tunawawakilisha kuona kwamba kila jambo tunalolifanya, kila biashara inayofanyika, inaendana na uhalisia na si kuwa ni sehemu ya unyonyaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo swali la nyongeza!

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwanza na-*declare interest*, mimi ni mmiliki wa shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyoongea, kuna vikao kadhaa vinaendelea kati ya Wamiliki, Mameneja na Serikali, Ofisi ya Kamishna Wizara ya Elimu, lakini mpaka sasa hatujafikia muafaka kwa sababu ya hiki ambacho amekiongea Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaonekana kama vile tunafanya mchezo, lakini jambo hili ni gumu sana. Shule zimetofautiana, wapo wamiliki wamewekeza na wamekopa fedha benki. Zipo shule zina utofauti wa vijijini na mjini. *Menu* ya chakula huwezi kulinganisha *menu* ya chakula shule za Dar es Salaam na shule za Rukwa, Mbeya ama Mwanza. Hata hivyo, mpaka wiki iliyopita, tumekutana na Serikali kwamba hata hawajafanya utafiti kwenye shule za msingi lakini ada elekezi inataka kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali, ni lini Serikali itaita tena kikao cha mwisho *TAMONGSCO* pamoja na Serikali wakae pamoja waweze kufanya utafiti wa pamoja? Serikali ifanye utafiti na shule binafsi zifanye utafiti ili wakae pamoja waweze kufanya *negotiation* ili ada elekezi itolewe si kwa upande mmoja tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ambavyo ameeleza Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshawahi kukaa na wadau hao, lakini niseme tu kwamba ni msingi huo huo ambao Serikali haitaki kuwanyanyasa wawekezaji wake ambao ni Washirika wakubwa wa elimu na ndiyo maana tumefanya tafiti katika maeneo mbalimbali. Mfano, tumeshakwenda katika maeneo hata ya vijijini, kuna shule za Sekondari kama Fingwa kule Rukwa, Idigima-Mbozi na Kitunda kule Kalambo, hizo zinatoza laki moja kule vijijini kabisa kwa Sekondari lakini ukienda kwenye shule nyingine, kama Feza yenyewe inatoza shilingi milioni 9.4, ukichukua *St. Joseph* shilingi milioni 5.9, ukichukua *Mwanza Alliance* shilingi milioni 4.8 na ndiyo maana tunafanya utafiti ili kuona kwamba bei zitakazotolewa kwanza zitapangwa kutegemeana na madaraja na shule mahali ilipo na uhalisia wa utoaji wa hiyo elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo siyo lengo la Serikali kuwatesa au kuwanyanyasa wawekezaji, bali ni kutoa bei inayofanana na uhalisia na hiyo itachochea utoaji wa elimu bora, lakini vilevile uwekezaji ulio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kikao napenda niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge, si kwamba Wamiliki tu wa shule ndiyo wanaostahili kukaa vikao, vikao hivi vitawashirikisha hata walezi pamoja na wazazi, pamoja na wananchi wengine ikiwemo Wabunge ili tupate bei zenye uhalisia.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, TAMISEMI!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu suala la elimu na TAMISEMI tunaguswa sana na bahati nzuri Naibu Waziri wa Elimu ametoa maelezo ya kutosha, kulikuwa na suala lini litafanyika hili, maana yake hili ndiyo suala la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Naibu Waziri ameshazungumza kwamba, hicho kikao kitaitwa na hili naomba nikiri wazi, kwa sababu nchi yetu ni pana sana, lengo kubwa la Serikali ni kui-*support private sector,* lakini pia kuangalia na watu hao wanaopata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kwamba, mchakato huu ni mpana kwa kushirikiana na wadau wote, imani yangu ni kwamba, tutakapofika mwisho wa siku hasa wamiliki wa shule na ndugu yangu Mulugo akiwa mmojawapo, tutafika maeneo ambayo Mtanzania wa kawaida wa kila *level* ataweza kuguswa kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, sasa aulize swali lake!

Na.15

**Ujenzi wa Chuo cha VETA Mkoani Kagera**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Mkoa wa Kagera hauna Chuo cha VETA chenye hadhi ya Chuo cha Mkoa na kwa sababu hiyo wananchi wa Mkoa huo hawapati elimu inayostahili. Hivyo, Serikali iliamua kujenga Chuo cha aina hiyo Bukoba kwenye Kata ya Nyakato ambako kiwanja kilipatikana na mipango yote ilifanywa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutembelea mara kwa mara eneo hilo, lakini ni muda mrefu sasa umepita hakuna chochote kinachoendelea:-

Je, ni lini ujenzi huo utaanza na kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Chuo cha VETA cha Mkoa wa Kagera unategemea kuanza baada ya hatua za maandalizi ya msingi zitakapokamilika. Serikali kwa sasa imeshalipa kiasi cha shilingi 4,779,896 kwa ajili ya kupata Hati miliki kwa eneo lenye hekta 40.9 lililopo katika Kijiji cha Burugo, Kata ya Nyakato ambapo chuo kitajengwa. Aidha, uchambuzi wa stadi zitakazofundishwa katika Chuo hicho umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuandaa michoro kwa ajili ya majengo na miundombinu ya chuo, kuandaa mitaala kulingana na stadi zilizotambuliwa, kuandaa mipango ya ukarabati wa miundombinu hasa kiliometa nne mpaka tano za barabara kutoka barabara kuu na kuhakikisha maji na umeme yanapatikana katika eneo hilo. Aidha, Serikali inaendelea na mazungumzo na Serikali ya Watu wa China kuhusiana na ufadhili wa ujenzi wa Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inategemea kukamilisha ujenzi wa Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Kagera kutegemeana na upatikanaji wa Fedha na juhudi mbalimbali ikiwemo ushirikishwaji wa Wafadhili wa ndani na nje ya nchi kama sehemu ya kuchangia juhudi za Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza, swali la nyongeza!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pia nishukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali wawili ya nyongeza.

La kwanza, nasikitika kwamba swali langu halijajibiwa, suala la Chuo cha VETA Kagera limezungumziwa muda mrefu sana humu ndani na nje ya humu ndani. Mkoa wa Kagera mzima hauna Chuo cha VETA cha hadhi ya Mkoa. Kwa hiyo, vijana wote wanaomaliza kidato cha nne au darasa la saba hawana fursa ya kupata mafunzo ya ufundi kuweza kujisitiri kwenye maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliaminishwa kwamba chuo hiki kingejengwa mwaka jana, tukatoa ardhi na mipango mingine ikaendelea na Waziri amefika pale mara mbili, tatu, ameangalia na kusema kwamba ujenzi unaanza, lakini hadi leo kwenye majibu tuliyopewa hapa hakuna matumaini hata kidogo chuo hiki kuanza kujengwa wakati wowote. Kwa hiyo swali langu halijajibiwa, ningependa kujua ni lini hasa kinakwenda kujengwa? Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, tupo humu ndani kwa ajili ya Bajeti ya mwaka ujao, ningependa kujua ni kiasi gani kimeombwa kwenye Bajeti hii kwa ajili ya chuo hicho, hayo mambo ya barabara , miundombinu, michoro na chuo chenyewe, ni kiasi gani kimeombwa kwenye Bajeti hii kwa ajili ya Chuo hicho? Asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niungane na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza kwa jitihada kubwa ambazo anazifanya juu ya chuo hiki, nami naona umuhimu wa chuo hiki katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anaweza kusema kwamba hatujajibu swali lake kwa sababu yeye anataka ni lini, lakini ujenzi wa chuo unaanza baada ya kupitia hatua mbalimbali na baadhi ya hatua zilizopitiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba eneo litakalojengwa chuo hicho limepimwa na ndiyo maana Serikali tayari imeshatoa fedha. Vilevile kushirikisha wadau wengine na baada ya kukamilika jitihada hizo, ndipo sasa tunaweza tukasema tukishakuwa na fedha tuanze kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu uzito juu ya chuo hicho lakini kimsingi niseme tu kwamba kwa sababu tulishapata hali ya mwelekeo ya baadhi ya wadau kutaka kukisaidia chuo hicho ndiyo tumekuwa tukiendelea nao na mazungumzo yeye mwenyewe ni shahidi, walishawahi kutembelea mpaka huko Kagera. Kwa hiyo naomba tu kwa sababu amekuwa na imani nasi atuamini na

ajue kwamba muda wowote tutampa taarifa kadri tunavyoendelea na jitihada za ujenzi wa Chuo hicho.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani sasa aulize swali lake.

Na.16

**Kusaidia Wavuvi Wadogo Kujikwamua na Umaskini**

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM** aliuliza:-

Uvuvi ni moja ya vipaumbele vinavyosaidia kusukuma maendeleo ya wananchi wengi wa Tanzania na Taifa letu ni miongoni mwa mataifa maskini duniani:-

Je, Serikali ya Awamu ya Tano imejipanga kwa kiasi gani ili kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo wa Tanzania ili kusaidia maendeleo ya Taifa na pia kujikwamua na umaskini uliokithiri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, Mbunge wa Kojani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Maendeleo na Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi *(SWIOFish)* ambao unatekelezwa Tanzania bara na Visiwani. Mradi umelenga kuboresha utawala bora kwenye jamii za wavuvi, kusaidia mitaji, kutoa elimu ya uvuvi endelevu na kuboresha miundombinu ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(Tanzania Agricultural Development Bank - TADB)* na dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali *(TIB)* ili kutoa fursa ya kupata mikopo kwa ajili ya kununua zana za uvuvi. Pia Serikali inaendelea kuwahamasisha wavuvi wajiunge katika Vyama vya Ushirika ikiwemo kuanzisha *SACCOS* ili kuweza kukopesheka kwenye Taasisi nyingine za kifedha

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa wavuvi wadogo ili waweze kuvua katika bahari kuu. Hadi sasa wawakilishi wa wavuvi 99 kutoka Kamati za Uvuvi Zanzibar na Vikundi vya Usimamizi wa Uvuvi *(BMUs)* Tanzania Bara wamepatiwa mafunzo hayo wakiwemo 47 kutoka Pemba ikiwemo Jimbo la Kojani. Wavuvi hawa baada ya kupatiwa mafunzo hutakiwa kurudi na kufundisha wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo haya ni endelevu na katika mwaka wa fedha 2016/2017 imepangwa wavuvi 50 wapatiwe mafunzo ya namna hiyo. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imekuwa ikitoa mafunzo kwa wavuvi walio katika Kamati za Uvuvi na *BMUs* namna ya kudhibiti uvuvi haramu ili kuwahakikishia wavuvi wadogo uvuvi endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mpango kutoa ruzuku kwa wavuvi wadogo unaolenga kuwasaidia kuoata zana bora na vifaa vya kuvulia zikiwemo injini za boti kwa kuchangia asilimia 40% ya gharama. Katika awamu ya kwanza, injini 73 zimenunuliwa na taratibu za kuzisamabaza zinaendelea.

Vilevile, Serikali kupitia miradi na programu mbalimbali imejenga mialo na masoko ya samaki katika Ukanda wa Ziwa Victoria 29, Ziwa Tanganyika minne na Bahari ya Hindi mitatu. Kuwepo kwa mialo hii kumepunguza upotevu wa samaki baada ya kuvuliwa hivyo kuongeza thamani na bei ya samaki kwa wavuvi wadogo. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maalim, swali la nyongeza!

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika nafurahi sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na majibu yake mazuri, nafurahi kwa kukubali kwamba kuna mradi unaotoa mafunzo na mitaji kwa wavuvi, lakini naomba niseme kwamba, mradi huu kuna bado katika Jimbo langu ambako kuna wavuvi wengi haujafika. Sasa naomba maelezo yake ni lini mafunzo na mitaji hii katika Jimbo langu la Kojani ili kuwafaidisha wavuvi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika mipango ambayo imepita, Jimbo la Mheshimiwa halikuwepo katika mpango, lakini katika bajeti inayokuja nitakuhakikishia kwamba wananchi wa Jimbo lako vilevile watapata mradi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gibson Ole-Maiseyeki Mbunge wa Arumeru Magharibi sasa aulize swali lake.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Rekebisha jina langu kidogo, naitwa Gibson Ole-Meiseyeki, umeandika Ole-Maiseyeki. Sasa naomba swali langu namba 17 lipate majibu ya Serikali.

Na.17

**Upatikanaji wa Mbegu Bora ya Mifugo**

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI** aliuliza:-

Kwa nini Serikali isifanye jitihada za makusudi za kuwatafutia wafugaji mbegu bora za mifugo aina mbalimbali na kuwasambazia wafugaji kwa bei nafuu ili kuondokana na aina za mifugo ambayo haina tija kwa wafugaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya jitihada za makusudi kuhakikisha wafugaji wanapata mbegu bora za mifugo kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo uhimilishaji kwa kutumia mbegu bora za mifugo zinazozalishwa katika Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji cha Usa River *(NAIC)*. Katika kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi 2015/2016 kituo kilizalisha jumla ya dozi 951,789 za mbegu bora za ng'ombe na kusambazwa nchini ambapo jumla ya ng'ombe 871,183 wa maziwa na ng,ombe 80,606 wa nyama walihimilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika jitihada za kuwezesha wafugaji kupata huduma hii kwa urahisi, Serikali imeanzisha vituo sita vya Kanda vilivyopo, Kibaha (Pwani), Lindi (Lindi), Kizota (Dodoma), Uyole (Mbeya), Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo cha Mwanza (Mwanza) na Mpanda (Katavi). Pia Serikali inaendelea na ujenzi wa kituo kingine cha Taifa cha Uhimilishaji cha *Sao Hill* kilichopo kwenye shamba la kuzalisha mitamba la *Sao Hill* (Mafinga-Iringa) kwa lengo la kusambaza huduma hii ya uhimilishaji katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali inazalisha na kuwasambazia wafugaji mifugo bora (majike na madume) kwa bei ya ruzuku kutoka katika mashamba yake. Mashamba haya yanazalisha mitamba ya ng'ombe wa maziwa, mitamba na madume ya ng'ombe wa nyama, mbuzi wa maziwa na nyama, kondoo na nguruwe. Kwa mfano, mtamba wa ng'ombe wa maziwa unauzwa kati ya shilingi 800,000 – 1,000,000/= ikilinganishwa na bei ya soko iliyopo ya kati ya shilingi 1,200,000/= na 2,300,000/=. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 hadi 2015/2016, jumla ya mitamba 4,520 ilizalishwa na kusambazwa katika mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuona fursa ya kibiashara katika kuzalisha mbegu bora za mifugo ili kukidhi mahitaji. Aidha, nawashauri Waheshimiwa Wabunge waendelee kuwahamasisha wafugaji wakiwemo wa Jimbo la Arumeru Magharibi kutumia

huduma za kuboresha mifugo zinazopatikana kwenye vituo vyetu ili kujipatia mifugo yenye tija.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Meiseyeki, swali la nyongeza.

**MHE. GIBSON B. MEISEYEKI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu tukizungumzia hasa mifugo, ng'ombe hawa wa nyama ni aina ile ambayo inachukua muda mrefu sana kumtunza ng'ombe kufika angalau kilo 100 unaweza kuchukua karibu miaka minne au mitano ng'ombe kufikisha kilo 100. Sioni *commitment* ya Serikali hapa hasa ukilinganisha kwa hii bei ambayo wameitaja hapa shilingi laki nane kwa milioni moja kwa mtamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii bei ni kubwa sana na sidhani kama, labda naomba ku-*declare interest,* mimi ni mfugaji na ni mkulima pia. Hii bei ya shilingi 800,000/= na shilingi 1,000,000/= ndiyo bei iliyoko sokoni, sasa kuambiwa kwamba hii ndiyo bei yenye ruzuku sitakubaliana na hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kupata *commitment* ya Serikali katika kubadilisha hasa aina ya mifugo tuliyonayo, ni lini Serikali itakuja na bei ambayo ni *affordable* kwa wakulima wetu ili tuweze kubadilisha mbegu hizi za hawa ng'ombe ambao wanachukua muda mrefu kuongeza uzito?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ni Tanzania ndiyo nchi pekee duniani ambayo maziwa ni rahisi kuliko maji ya kunywa, ni lini Serikali itakuja na bei elekezi ya lita moja ya maziwa ya ng'ombe ili iweze kuwa na tija kwa wafugaji ambao wanahangaika sana na mifugo, lakini hawapati chochote kutokana na nguvukazi yao hiyo na pengine inaweza kuwahamasisha vijana zaidi kushiriki kwenye ufugaji. Ni lini Serikali itakuja na bei elekezi ya lita moja ya maziwa *fresh* ya ng'ombe ili wakulima wetu waweze kupata tija?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa bei ya sasa ya mitamba inaonekana kwamba iko juu, lakini kama nilivyosema ukilinganisha na bei iliyoko kwenye soko bado kuna ruzuku.

Kama nilivyosema tofauti inafikia kwenye mitamba yenye ruzuku ya Serikali ni kati ya shilingi 800,000/= na 1,200,000/= wakati kwenye soko inafikia kati ya 1,2000,000/= hadi 2,300,000/=. Kuna tofauti hapo, lakini nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kwamba bei hii inashuka ili wafugaji wengi waweze kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunamshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine, tujaribu kutumia huduma za uhimilishaji kwasababu zinakuwa bei yake ni afadhali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei elekezi, bei ya maziwa kama bidhaa nyingi nchini kwetu zinaamuliwa na kanuni za soko. Tunachoweza kusema ni vigumu kuweka bei elekezi lakini tunachofanya kama Serikali ni kujaribu kuweka mazingira mazuri ya uchakataji wa maziwa, kujenga viwanda ili bidhaa za maziwa ziweze kupata bei.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Waziri wa Viwanda!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, napenda niongeze jibu moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kujenga uchumi wa viwanda na tuwe shindani lazima mazao ya chakula yawe ya bei nafuu. Kwa hiyo, wakulima wanaofuga ng'ombe, wajibu wa Serikali ni kuwawezesha ili bei ya maziwa iwe chini, bei ya chakula iwe chini, wafuge na kuzalisha kwa tija kusudi uwekezaji Tanzania uwe nafuu, viwanda vya dunia nzima vije Tanzania. Nawapongeza wakulima wa maziwa na bajeti yetu itawasemea.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti atauliza na Mheshimiwa Faida Mohamed ndiye atakayeuliza swali kwa niaba yake.

Na. 18

**Mkakati wa Kuwanusuru Vikongwe Nchini**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR (K.n.y. MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS NYIMBO)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kunusuru mauaji ya vikongwe nchini?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Mambo ya Ndani ya Nchi!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeweka mikakati mbalimbali ya kunusuru mauaji ya vikongwe nchini ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya operesheni na misako ya mara kwa mara kubaini waganga wa jadi wanaojihusisha na upigaji ramli chonganishi na wasiofuata sheria;

(ii) Kutoa elimu kupitia Polisi Jamii, wadau mbalimbali wa ulinzi na usalama, madhehebu ya dini na mashirika na taasisi binafsi, lengo likiwa ni kuwaelimisha wananchi madhara ya kujichukulia sheria mkononi; na

(iii) Kuanzishwa kwa vikosi kazi ili kuweza kufuatilia na kutafuta taarifa mbalimbali za watuhumiwa wanaotenda matukio hayo maarufu kama wakata mapanga, kabla na baada ya kufanyika kwa tukio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwenye Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa wananchi kuacha vitendo vya kujichukulia sheria mkononi vinavyosababisha mauaji kwa nchi yetu inaendeshwa kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida Mohamed, swali la nyongeza.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo hivi vya kuwaua wazee wetu ama tunavyoita vikongwe lakini hao mimi kwa lugha hii ya vikongwe hata siipendi, wazee wetu! Wazee ni dhamana yetu sisi vijana ama wananchi wote, lakini kuna watu katika mikoa mingine wanawaua wazee wetu, wengine wakiwa hai wanawafukia. Hiyo tunaoneshwa kabisa katika vyombo mbalimbali vya habari. Wengine wanawaua watu kwa kuwafukia kwa sababu wazee wetu wana macho mekundu na watu hawajui kwamba kuwa na macho mekundu ni kupikia kuni kwa wingi, sasa...

**MBUNGE FULANI:** Na mavi ya ng'ombe.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Na mavi ya ng'ombe, wengine wanasema kinyesi cha ng'ombe, wanapikia kinyesi cha ng'ombe wengine macho yanakuwa mekundu.

Je tutawasaidiaje wazee hawa kuwaondoshea kuwa na macho mekundu kwa kuwapelekea gesi kwa wingi kule vijijini ili waweze kuwa na macho mazuri, wasipate kuuliwa kwa itikadi za kishirikina? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amejibu hapa kama kunatolewa elimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Faida hilo ni swali la nyongeza au la pili?

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** La pili la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hapa Serikali inatoa elimu, hata sisi Wabunge tunapaswa kutoa elimu katika maeneo yetu, lakini sasa athari hii ya kuwaua wazee wetu itakwenda vizazi na vizazi vijavyo huko mbele. Watoto wetu wanajifunza nini kuhusiana na jambo hili hapo mbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawachukulia hatua gani kuwaondosha hawa watu wanaowaua wazee wetu? Inawachukulia hatua gani kali kukomesha hasa katika mikoa hiyo ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na kwingineko, wazee wetu wanauliwa sana? Naomba jibu maridhawa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, japokuwa swali la kwanza sina uhakika kama ni la Wizara yako. Wewe jibu maswali yanayohusika na Wizara yako.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna mikakati mbalimbali ambayo tayari imeshaanza kuchukuliwa na Serikali kuhakikisha kwamba matumizi ya kuni ama hayo mavi ya ng'ombe kwa ajili ya kupikia yanapungua, ikiwemo kuanzisha kwa nishati mbadala, matumizi ya majiko bunifu na kadhalika, lakini pia harakati za Serikali kusambaza umeme vijijini zinasaidia sana kuhakikisha wananchi wanatumia nishati iliyokuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lake la pili anazungumzia kwamba hatua gani ambazo Serikali imechukua ili kudhibiti matukio kama haya. Nataka tu nimhakikishie kwamba takwimu ambazo tunazo kuanzia mwezi Julai, 2015 mpaka Machi, 2016 tayari kuna watuhumiwa 135 ambao wameshakamatwa na kesi kama 222 ambazo zinaendelea mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Jeshi la Polisi ama Serikali kupitia Jeshi la Polisi, linafanya kazi kubwa sana kuhakikisha kwamba linawadhibiti wale wananchi wote ambao wamekuwa wakijichukulia sheria mkononi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya Mwaka 1996 – 2020**

**MHE. HASSAN E. MASALA (K.n.y. MHE. HAMIDA M. ABDALLAH)** aliuliza:-

Vijana wengi wa Mkoa wa Lindi karibu 40% hawana ajira kutokana na ukosefu wa viwanda mkoani humo; na kwa kutambua kuwa sehemu kubwa ya uchumi wetu unategemea kilimo na Serikali ilitunga Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996 -2020 itakayosimamia maendeleo ya viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao:-

Je, Sera hiyo imesimamiwa vipi katika kuvifanya viwanda vilivyopo vya usindikaji wa mazao viendelezwe ili kuongeza thamani ya mazao yetu na kukuza uchumi na hatimaye vijana kupata ajira katika Mkoa wa Lindi?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuchochea maendeleo ya viwanda nchini, Serikali iliandaa na kuanza utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda *(Sustainable Industrial Policy – (SIDP) 1996 -2020*) na baadaye iliandaa Mkakati Unganishi wa Kuendeleza Sekta ya Viwanda *(Integrated Industrial Development Strategy 2025)* ili kuimarisha utekelezaji wa Sera hiyo. Moja ya vipaumbele vya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ililenga katika kipindi cha muda mfupi kuendeleza viwanda vinavyoongeza thamani ya rasilimali zinazopatikana nchini ikiwemo mazao ya kilimo ili kukuza uchumi na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa utekelezaji wa Sera unaanza mwaka 1996, mkoa wa Lindi ulikuwa na viwanda vitano vinavyosindika mazao ya kilimo, vikiwepo viwanda vya kubangua korosho na viwanda vingine vidogo vidogo vya samani, kukamua mafuta ya ufuta, usindikaji nafaka na kadhalika. Aidha,

viwanda hivyo vilibinafsishwa na kwa bahati mbaya havijawahi kufanya kazi hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na utekelezaji wa Sera, ikijumuisha uhamasishaji wa sekta binafsi kuwekeza kwenye viwanda, upatikanaji wa miundombinu muhimu kama vile maji, umeme, mawasiliano, barabara na kuimarisha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu za sasa zinaonesha Mkoa wa Lindi una jumla ya viwanda vinavyosindika mazao pekee vipatavyo 329 vinavyoajiri watu 770 na kati ya hivyo viwanda vikubwa vinavyoajiri watu watano mpaka kumi vipo kumi. Kwa kushirikiana na Msajili wa Hazina, sasa tunapitia vile Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa ili viweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati unganishi wa kuendeleza Sekta ya viwanda umeibua mwambao wa Pwani kuwa kitovu cha kuendeleza viwanda na kuuza mauzo nje (*Water Front Industrial and Export Frontiers*). Lengo la mkakati ni pamoja na kukuza sekta ya viwanda vijijini itakayoongozwa na maendeleo ya kilimo na kutoa fursa ya ukuaji wa viwanda vidogo na vya kati kwa kuchukua hatua za makusudi za kuvisaidia katika ngazi zote za maendeleo ili viweze kukua.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa juu ya Mkoa wa Lindi, lakini naomba pia nitumie nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza. Kama ambavyo yeye amekiri, Mkoa wa Lindi kwa ujumla ulikuwa na viwanda vingi ambavyo sasa hivi vyote vimebinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nachingwea viko viwanda viwili, Kiwanda cha Korosho pamoja na Kiwanda cha Kukamua Mafuta lakini Lindi pia imekuwa na rasilimali ya bahari ambayo tukiitengenezea mazingira bado tunaweza tukatengeneza viwanda vidogo kwa ajili ya usindikaji wa samaki. Pamoja na majibu hayo aliyoyatoa je Mheshimiwa Waziri anatuahidi nini katika mpango huu ambao tunaelekea na tukiangalia Mkoa wa Lindi haujaguswa kwa namna yoyote ile? Asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali la nyongeza. Kwa ruhusa yako naomba Mheshimiwa Mbunge tusiwahishe shughuli, bajeti yangu inakuja na mambo mazuri kwa ajili ya Mkoa wa Lindi ikiwemo uanzishaji wa kilimo cha muhogo ambako tutakuwa tuki-*export* nje tani milioni mbili za mhogo nchini China zenye thamani ya dola milioni 300. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Rashid Mohammed Chuachua, Mbunge wa Masasi, sasa aulize swali lake.

Na. 20

**Tatizo la Maji Jimbo la Masasi**

**MHE. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya upanuzi wa mradi wa maji wa Mbwinji ili usambaze maji katika vijiji vyote vya Jimbo la Masasi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Jimbo la Masasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Safi wa Masasi – Nachingwea kutoka chanzo cha Mbwinji unahudumia wakazi wa Miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na baadhi ya Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Nachingwea na Ruangwa. Jumla ya wakazi wapatao 188,250 wanahudumiwa. Mradi huo uliojengwa kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 40 na kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, tarehe 24 Julai, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma za maji katika Wilaya ya Masasi, Mradi wa Masasi – Nachingwea unakusudiwa kuendelea kufanyiwa upanuzi wa miundombinu ili kuunganisha vijiji vingi zaidi na huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Mji wa Masasi inaendelea na kazi ya kuunganisha maji katika vijiji vilivyo katika Jimbo la Masasi ambavyo viko mbali na bomba kuu linalopeleka maji katika Mji wa Masasi ili kuongeza upatikanaji wa maji kupitia mradi wa Masasi – Nachingwea. Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Vijiji vya Nangaya, Nangose, Temeke na Marokopareni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* ili vijiji vingi zaidi ya Jimbo la Masasi vipate maji. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chuachua swali la nyongeza.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali ya nyongeza mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, katika bajeti ya mwaka 2014/2015, Serikali ilitenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuwawezesha Mamlaka ya Usambazaji wa Maji *(MANAWASA)* waweze kusambaza maji ya kutosha katika Vijiji vya Jimbo la Masasi. Pia bajeti hiyo hiyo na kiwango hicho hicho cha fedha kilitengwa 2015/2016 na fedha hizo mpaka sasa hazijatoka. Ni lini Serikali sasa itapeleka fedha hizi ili kusudi wananchi waweze kupata huduma hii ya msingi na ni ya lazima?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba kufahamu, ni lini Serikali itapunguza gharama kubwa za maunganisho ya maji kwa wananchi ambao kimsingi hawamudu gharama hizo na tayari Naibu Waziri alipotembelea Jimbo la Masasi tulimdokeza? Asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza amesema Serikali ilitenga shilingi bilioni moja mwaka wa fedha uliopita na mwaka wa fedha tulionao, ni kweli, fedha hii ilitengwa lakini kutokana na makusanyo ya Serikali kutokuwa mazuri, basi fedha hii haikupelekwa kwenye mradi. Hata hivyo, kwa sasa Serikali imeanza kukusanya mapato vizuri na ninyi wenyewe Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, kwa hiyo, sasa tutaanza kupeleka fedha ili shughuli iliyotarajiwa kufanyika kutokana na hii fedha iweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, gharama za maunganisho, ni kweli nilipokwenda kule nilikuta kuna malalamiko ya gharama za maunganisho. Nilielekeza mamlaka ya *MANAWASA* waweze kupitia gharama hiyo pamoja Bodi na waweze kuja na gharama ambayo itakuwa ni rafiki kwa watumiaji wa maji. Nashukuru wameniletea taarifa kwamba maelekezo yote niliyowapa wameanza kuyafanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndassa!

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Maji ni uhai, ningependa kuiuliza Serikali, kwa sababu iko ahadi ya kupeleka maji katika maeneo ya Sumve, Malya, Mwagini kupitia Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, ningependa Serikali iniambie ni lini hasa mradi huo mkubwa ambao utanufaisha zaidi ya vijiji 40, utaanza kwa sababu ni ahadi ya muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji!

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imeahidi kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka maeneo ya Sumve na maeneo mengine. Naomba nimhakikishie tu kwamba ahadi hiyo ipo pale pale na nitakapoleta bajeti yangu nitaeleza hilo jibu la lini kazi hiyo itaanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda. Kwa hiyo, nitaleta kwenu matangazo, lakini baada ya matangazo haya tutamsikia Waziri wa Fedha akiwasilisha kwetu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016/2017 - 2020/2021.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kuchangia tutaanza asubuhi hii, naomba muanze kujaza zile fomu za kuomba kuchangia halafu mchana tutaendelea.

Naleta kwenu matangazo ya wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, mmoja ni mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika ambaye anaitwa Christopher Kalaja. *(Makofi)*

Wageni wengine kuna wageni wawili wa Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, mmoja anaitwa Mheshimiwa Ahimidiwe A. Riko, Diwani wa Kata ya Mbuguni na mgeni mwingine anaitwa Joseph Mugenyi. *(Makofi)*

Pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge Jimbo la Ukerewe na hawa ni Ndugu Peter Gervas na Ndugu James Misana. *(Makofi)*

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, anaitwa Nestory Kubilu. *(Makofi)*

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mbunge wa Jimbo la Busega, ambaye jina lake halikuwekwa hapa.

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo mengine hapa, kuna tangazo la Kamati ya Katiba na Sheria ambayo Mwenyekiti wake anawatangazia kwamba leo kutakuwa na mkutano yaani tarehe 20 Aprili, 2016 katika jengo la utawala, chumba namba 229. Kwa hiyo, kikao kitakuwa saa saba baada ya Bunge kuahirishwa, mnaombwa kuhudhuria bila kukosa.

Tangazo lingine Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti, wanatangaziwa kuwa kutakuwa na kikao cha pamoja leo Jumatano tarehe 20 Aprili, saa tisa alasiri kwenye ukumbi wa Msekwa. Ajenda ya kikao hicho ni kujadili mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za

Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara, Wajumbe wote mnaombwa kuhudhuria bila kukosa. Katibu!

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mwongozo wa Spika!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Hoja ya Waziri wa Fedha…

**NAIBU SPIKA:** Katibu naomba ukae, Mheshimiwa Nkamia!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) ambayo kutokana na muda nisingependa niisome. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara wakati akiongezea majibu kwenye swali namba 17 amezungumza kauli ambayo pengine nadhani inaweza ikakatisha tamaa Watanzania ambao wanategemea kilimo. Kwa kauli yake amesema kwamba; kwanza naomba ku-*declare interest,* mimi ni mkulima, amesema ili nchi hii iweze kwenda katika uchumi wa viwanda ni lazima bei za mazao ya wakulima zishuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka Mwongozo wako, lakini sambamba na hilo amesema pia kwamba wananchi wa Lindi wajiandae kulima muhogo ambao utauzwa nje. Sasa hizi ni kauli mbili ambazo zinawakatisha tamaa wananchi wengi wa Tanzania wanaotegemea kilimo. Ningeomba tu Mwongozo wako, je, hii ni kauli ya Serikali ya Awamu ya Tano au ni kauli ya Mwijage yeye kama Mbunge? Asante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nitatoa Mwongozo baadaye, Katibu tuendelee!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali, Hoja ya Waziri wa Fedha na Mipango kwamba Bunge sasa lijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 – 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango!

**Hoja za Serikali**

**Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 – 2020/2021**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017-2020/2021.

Mheshimiwa Niabu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Tatu wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuendelea kuwa na imani nami kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango ambayo ina jukumu kubwa la kusimamia uchumi, kupanga na kuratibu utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuliahidi Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kuwa nitaendelea kutumia uwezo wangu wote, uaminifu na uadilifu ili kuhakikisha kwamba Mpango huu unasimamiwa vyema na kutekelezwa ipasavyo. Nitajitahidi kuhakikisha kuwa rasilimali zitakazotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu zinatumika vizuri na kwamba zinasaidia kupunguza umaskini unaowakabili wananchi hususani waishio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa ushirikiano wao. Maelekezo na ushauri waliotupatia wakati wa kujadili mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yametusaidia katika kuandaa hotuba hii na kuboresha Mpango ninaouwasilisha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Kondoa na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Servacius Beda Likwelile kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ninaouwasilisha leo ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 63(3)(c) ambayo inalitaka Bunge kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu na muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango huu wa Pili ninaouwasilisha unatokana na ukweli kwamba Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/2012 mpaka 2015/2016, unafikia ukomo Juni, 2016. Kwa hiyo, Serikali inawajibika kuandaa Mpango mwingine utakaoongoza maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti za kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Mpango unaomaliza muda wake ulijielekeza katika kutanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi na kubainisha maeneo ya kipaumbele kuwa ni miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimaliwatu, huduma za fedha, utalii na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa miaka kumi na tano, 2011/2012 mpaka 2025/2026 wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mpango Elekezi uligawanywa katika Mipango mitatu ya miaka mitano mitano, kila Mpango ukiwa na dhima mahususi kuendana na vipaumbele vyake. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utaongoza jitihada za maendeleo kwa kipindi cha kuanzia 2016/2017 - 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Mpango Elekezi, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ulipaswa kujikita katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda. Hata hivyo, mwaka 2015 Serikali ilifanya uamuzi wa kuunganisha mifumo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA katika mfumo mmoja jumuishi ili kuainisha *agenda* ya kupunguza umaskini katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uamuzi huu ni kuwa na mfumo mmoja wa utekelezaji wa Mipango na hivyo kutanzua changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mifumo miwili. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa vipaumbele vingi vinavyofanana na hivyo kutawanya rasilimali za Taifa kidogo kidogo na kuwepo kwa mfumo dhaifu wa uratibu na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, uamuzi wa kuunganisha mifumo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA unakusudia kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kufanya mabadiliko ya mfumo wa uchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa. Kufuatia uamuzi huo Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umejumuisha masuala ya ukuaji na mageuzi ya mfumo wa uchumi na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utayarishaji wa Mpango umezingatia yafuatayo:-

(i) Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 na Mpango Elekezi wa miaka kumi na tano;

(ii) Mafanikio na changamoto zilizobainishwa katika mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na MKUKUTA II;

(iii) Uamuzi wa Serikali kufungamanisha na kuwianisha mifumo ya Mpango na MKUKUTA;

(iv) Sera na mikakati mbalimbali za Kisekta, Kikanda na Kimataifa ambayo Serikali imeridhia hususan Malengo ya Maendeleo Endelevu ya 2030 *(Sustainable Development Goals)*;

(v) Dira ya Afrika ya mwaka 2063;

(vi) Mpango Kazi wa kuharakisha maendeleo ya viwanda Afrika ya mwaka 2008;

(vii) Sera ya Viwanda ya Afrika Mashariki na mkakati wa utekelezaji wake;

(viii) Mwelekeo wa Maendeleo ya Viwanda wa *SADC* wa 2013 mpaka 2018;

(ix) Mkakati wa Maendeleo wa Viwanda wa *SADC* 2015 – 2063;

(x) Pia Mpango umezingatia; Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015; na

(xi) Hotuba ya Rais ya ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja iliyoweka msukumo na azma ya kipekee ya Serikali ya Awamu ya Tano katika kujenga uchumi wa viwanda na kuzipatia ufumbuzi changamoto za msingi kwa maisha ya Watanzania, hususan maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Mpango yalihusisha ushirikishwaji mpana wa wadau katika hatua zote kwa lengo la kujenga muafaka na maeneo ya kipaumbele na mfumo wa utekelezaji. Baadhi ya wadau walioshirikishwa ni pamoja na Wizara, Idara na Taasisi za Umma, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi za Kiraia, Taasisi za Elimu ya Juu na Utafiti, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Aidha, Bunge lilishirikishwa kupitia semina ya Wabunge iliyofanyika hapa Dodoma mwezi Februari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ulifanyika uchambuzi wa kitaalam ulioongozwa na wataalam elekezi kutoka *Overseas Development Institute, Department For International Development* ya Uingereza na *REPOA (Research on Poverty Alleviation)* lakini pia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango. Pia maandalizi ya Mpango yaliongozwa na Kamati ya Usimamizi ambayo wajumbe wake waliteuliwa kuwakilisha makundi mbalimbali zikiwemo sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa uchumi. Tanzania imeendelea kuwa miongoni mwa nchi zinazokua kiuchumi kwa kasi Barani Afrika. Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, uchumi ulikuwa kwa wastani asilimia 6.7 kwa mwaka na kwa miaka mitatu ya mwisho ukuaji ulizidi kuimarika kufikia asilimia 7.4 mwaka 2013 na asilimia 7.0 mwaka 2014 na 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, wastani wa pato la kila mtu liliongezeka kutoka sh. 770,464.3 sawa na dola za Kimarekani 538 mwaka 2010 hadi sh. 1,997,139.19 sawa na dola za Kimarekani 1006 mwaka 2015. Ukuaji wa Pato la Taifa ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na sekta za madini na gesi, ujenzi, uzalishaji na mauzo nje ya nchi ya bidhaa za viwandani, kuimarika kwa huduma za fedha, hali nzuri ya hewa na kuwepo kwa amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ukuaji huu bado ni mdogo ukilinganishwa na lengo la wastani wa asilimia nane au zaidi kwa mwaka. Vilevile wastani wa pato la mwananchi lililofikiwa bado ni dogo likilinganishwa na lengo la Dira la kufikia dola 3000 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mwenendo wa mfumuko wa bei, thamani ya shilingi na hatua zilizofikiwa kupunguza umaskini, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo yangu yaliyoko katika aya ya 12 mpaka aya ya 16 ya kitabu cha hotuba yangu na yanukuliwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/2012 mpaka 2015/2016 na MKUKUTA II unakadiriwa kufikia asilimia 60 ya malengo ifikapo mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, naliomba pia Bunge lako Tukufu lipokee maelezo yangu kuhusu mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa na MKUKUTA II kama yalivyo katika kitabu cha hotuba yangu aya ya 18 mpaka ya 29 na yasomeke hivyo kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nieleze Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 una dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu kwa kiingereza ni *naturing industrialization for economic transformation and human development*. Msukumo wa Mpango huu ni kuhakikisha kuwa rasilimali na fursa za nchi zinatumika vizuri katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na uwezo wa kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, msisitizo katika maendeleo ya viwanda nchini siyo jambo jipya, tangu uhuru maendeleo yamekuwa yakipewa kipaumbele katika Mipango katika vipindi mbalimbali, japo utekelezaji wake ulikuwa ukitumia mikakati inayotofautiana kwa kuzingatia mfumo wa sera za usimamizi wa uchumi. Kabla ya Azimio la Arusha sekta ya viwanda iliendelezwa na sekta binafsi na Serikali, baada ya Azimio la Arusha, Serikali ilitekeleza Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea ambapo shughuli zote kuu za kiuchumi ikiwa ni pamoja na viwanda zilianza kumilikiwa na kuendeshwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, msisitizo ilikuwa ni kujitegemea ambapo viwanda vililenga kuzalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi nchini na hivyo kupunguza uagizaji wa bidhaa hizo kutoka nje yaani *import substitution*. Viwanda vichache vilijikita katika kuchakata mazao ya kilimo kwa ajili ya kuuza nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha viwanda na soko la ndani vinalindwa sera ya kudhibiti biashara iliwekwa lakini kuyumba kwa uchumi nchini na kuvunjika kwa mfumo wa kisoshalisti duniani ulifanya Tanzania kuachana na mfumo wa uchumi wa ujamaa na kujitegemea na badala yake kufungulia milango kwa wawekezaji binafsi na kuondoa vikwazo vya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya viwanda. Tangu kuanza kwa ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma mwaka 1992, viwanda 106 vimebinafsishwa kwa wawekezaji wa ndani na wa kutoka nje ya nchi. Lengo lilikuwa ni kuongeza ufanisi wa usimamizi wa uzalishaji, ajira, kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa hapa nchini na kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, viwanda 34 vinaendeshwa kwa ufanisi na hivyo kuongeza ajira na mapato ya Serikali. Viwanda 33 vinaendeshwa kwa hasara na viwanda 39 vya bidhaa mbalimbali hususan ngozi, chuma, korosho, zana za kilimo, sabuni na mafuta ya kupikia vimefungwa kabisa kutokana na changamoto za kiutendaji, mitaji, teknolojia, nishati, malighafi au kutokuzingatiwa kwa mikataba ya mauzo. Hatua za uchambuzi kwa lengo la kubainisha mfumo na kuvifufua viwanda

vilivyobinafsishwa zimeanza na zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango yaani mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendelezaji wa viwanda nchini ni jambo la kutiliwa mkazo katika Mipango yetu ijayo, ili kutuwezesha kufikia azma ya kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Maendeleo ya viwanda yanashikilia ufunguo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kutokana na uwezo wake wa kutengeneza ajira nyingi zenye faida na kuchochea maendeleo ya teknolojia. Mifano kutoka nchi mbalimbali inabainisha kuwa maendeleo ya viwanda ndio msingi na chimbuko la ustawi wa nchi hizo kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango huu uzoefu wa nchi mbalimbali umetumika katika kubainisha mwelekeo wa ujenzi wa viwanda nchini. Uzoefu huo unabainisha kuwa Serikali ina wajibu mkubwa katika hatua za awali za ujenzi wa uchumi wa viwanda na hususan kuweka mazingira mazuri ya kibiashara, kuweka mfumo mzuri wa kibenki ikiwa ni pamoja na kuanzisha benki maalum za maendeleo za kisekta za kusaidia upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na gharama nafuu na kuainisha sera na taratibu dhahiri za kuchochea maendeleo ya sekta binafsi, uhaulishaji teknolojia na ukuzaji wa fani za kitaalam zinazotakiwa katika maeneo ya vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatumia taasisi zake za kibiashara kama mkakati wa kuingia ubia na sekta binafsi katika kuvutia viwanda vyenye maslahi makubwa Kitaifa, kibiashara, kiteknolojia au kuzalisha bidhaa muhimu kwa soko la ndani; kusaidia sekta binafsi za ndani kuingia na kujiimarisha katika shughuli za viwanda, hususan viwanda mkakati na shughuli nyingine muhimu na kuwianisha sera za viwanda, biashara, elimu, ufundi, tafiti na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa masuala yatakayopewa kipaumbele katika bajeti, ni utafiti na ubunifu na pia maendeleo ya miji na uendelezaji wa maeneo ya biashara kubwa na ndogo. Halmashauri za Miji, Wilaya na Miji Midogo zina wajibu wa msingi wa kulea maendeleo ya viwanda na biashara katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kulinda maendeleo ya viwanda mkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu uzoefu wa nchi nyingine yapo katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano; Kwanza ni kukuza uchumi na kujenga msingi wa uchumi wa viwanda. Eneo hili linahusisha hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika sekta za uzalishaji

ikiwa ni pamoja na sekta za kilimo, viwanda, madini na utalii. Vigezo vya uteuzi wa miradi ya kundi hili ni pamoja na uwepo wa fursa za kipekee za rasilimali za uzalishaji na masoko ya bidhaa, uwezo wa bidhaa hizo kushindana au kuhimili ushindani wa kibiashara, bidhaa zenye kutumika kwa wingi katika soko la ndani, uzalishaji wa bidhaa zinazotumia teknolojia inayoendana na uwezo wa nchi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi na kwa unafuu, lakini pia, miradi itakayowezesha Tanzania kutumia vizuri fursa yake ya kijografia na mhimili wa biashara ya usafirishaji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati. Mwisho, ni Uendelevu wa Ukuaji wa Mabadiliko ya Uchumi baada ya Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili la kipaumbele ni kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu na hili litahusisha kupanua fursa za upatikanaji wa elimu kuanzia malezi na elimu ya awali, elimu bora kwa wote na fursa za kujiendeleza kitaaluma na ujuzi, kumwezesha mtu kujiajiri au kuajiriwa, kuimarisha na kuboresha afya ya mwananchi kama vile huduma za matibabu, usalama wa chakula na upatikanaji wa viini lishe vya mwili *(nutrition)*, maji safi, mazingira ya kuishi na hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji. Hapa Mpango unalenga kuimarisha mifumo ya kisheria, ili iwe rafiki katika kuvutia wawekezaji wa ndani na nje pamoja na kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za msingi kwa uwekezaji, ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati ya umeme, miundombinu ya reli, barabara, bandari, usafiri wa anga, usafiri wa majini, maji na TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ni kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango na maeneo mahususi ni kutanzua vikwazo vya utekelezaji na kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya mpango. Aidha, eneo hili limeainisha marekebisho yanayopaswa kufanyika ya kisera, kisheria na taratibu za kuongeza ufanisi wa kutekeleza Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya miradi katika Mpango huu imepewa sifa ya kuwa miradi ya kielelezo *(flagship projects)* na miradi hii ni ile mikubwa ambayo matokeo yake yanatarajiwa kusukuma au kuwezesha ufanisi wa utekelezaji na uwekezaji wa miradi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hii ni mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma, mradi wa chuma Liganga, maeneo maalum ya uwekezaji, Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini, ujenzi wa reli ya kati na matawi yake kwa kiwango cha *standard gauge,* Mji wa Kilimo wa Mkulazi, ufufuaji wa Shirika la Taifa la Ndege, kusomesha vijana wengi katika fani na ufundi stadi unaohitajika katika maeneo ya kipaumbele. Miradi hii imefungamanishwa na miradi mingine ya kimkakati katika mfumo wa maendeleo au maeneo maalum ya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu maeneo ya kipaumbele ya Mpango yapo katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ugharamiaji wa mpango; shilingi trilioni 107 zitahitajika kugharamia utekelezaji wa Mpango huu na miradi ya maendeleo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo ambayo ni sawa na wastani wa shilingi trilioni 21.4 kila mwaka. Kati ya fedha hizo Serikali itachangia shilingi trilioni 59, sawa na shilingi trilioni 11.8 kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyojidhihirisha, kuna ongezeko kubwa la fedha zinazohitajika kugharamia mpango wa pili ikilinganishwa na ule wa kwanza. Hii imesababishwa na kuzingatia uzoefu tulioupata katika utekelezaji wa Mpango wa Kwanza na pia ukubwa wa miradi tarajiwa sambamba na nia ya kuchochea upatikanaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa nchi nyingine umebainisha kuwa, mkakati wa ujenzi wa viwanda, aghalabu huvutia misaada kutoka nje. Mantiki yake ni kuwa, nchi haina budi kuwa na mkakati mahususi wa kukusanya fedha kuwezesha utekelezaji wa Mpango kwa ufanisi. Mpango unaainisha maeneo mawili ya vyanzo vya fedha, yani mapato ya Serikali yakihusisha mapato ya kodi na yasiyokuwa ya kodi, mikopo na misaada kutoka nje. Eneo la pili, ni sekta binafsi ya ndani na nje. Ni jambo lililo bayana kuwa kwa kiasi kikubwa, utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo utategemea ushiriki wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika miradi ya maendeleo, Serikali imeweka mikakati ya kujenga na kuboresha miundombinu wezeshi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuhamasisha na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Fedha za Serikali zitatumika kama chambo kuvutia ushiriki wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishaeleza, Mpango huu unabainisha miradi mikubwa ya kielelezo. Naomba nisisitize kuwa, miradi hii itatatekelezwa kwa kiwango kikubwa na sekta binafsi moja kwa moja au kwa ubia na sekta ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu ugharamiaji wa Mpango yapo katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikakati ya Utekelezajii. Mpango wa Pili utatekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka. Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa kila mwaka,

itaelekeza utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kurejea hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi husika na kubaini mahitaji ya rasilimali. Wizara na Taasisi nazo zitafanya mapitio ya mikakati ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusudi la uchambuzi huu ni kuhakikisha vipaumbele vya Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano vinazingatiwa katika miaka yote mitano ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu mikakati ya utekelezaji wa Mpango huu yapo katika Kitabu cha Mpango, Sura ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na Mipango itakuwa na wajibu wa kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na kutoa taarifa katika ngazi zote stahiki kwa wakati. Sura ya Sita ya Kitabu cha Mpango imeainisha viashiria na malengo mahususi kwa ajili ya kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara na taasisi za umma zinazohusika moja kwa moja katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo nazo zitawajibika kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi katika maeneo yao na kuandaa tarifa za utekelezaji kulingana na miongozo itakayotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kina ya utekelezaji wa Mpango katika kipindi cha kati na mwisho vitafanyika kwa kuwatumia watathmini wa kujitegemea nje ya mfumo wa Serikali, ili kuwa wawazi na huru zaidi.

Aidha, tathmini hiyo, itazingatia vigezo na malengo yaliyoainishwa katika maeneo mbalimbali ya Mpango. Wasimamizi wakuu wa miradi watakaothibitika kushindwa kufikia malengo ya Mpango, wawajibike wenyewe au wawajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Mpango. Baadhi ya malengo ya Mpango huu ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kasi ya ukuaji wa uchumi kuongezeka kutoka 7% mwaka 2015 hadi 10% mwaka 2020.

(ii) Pato la wastani la kila mwananchi kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani 1,006 mwaka 2015 hadi Dola 1,500 mwaka 2020.

(iii) Uwekezaji wa moja kwa moja nchini *(Foreign Direct Investment)* kuongezeka kutoka Dola za Kimarekani bilioni 2.14 mwaka 2014 hadi Dola za Kimarekani bilioni tano mwaka 2020.

(iv) Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na kodi kutoka 12.1% ya pato la Taifa mwaka 2014/2015 hadi 17.1% ya Pato la Taifa mwaka 2021.

(v) Umaskini wa mahitaji ya msingi kupungua kutoka 28.2% mwaka 2011/2012 hadi 16.7% mwaka 2020/2021.

(vi) Idadi ya wahitimu kutoka vyuo vya ufundi stadi kuongezeka kutoka 150,000 mwaka 2014/2015 hadi 700,000 mwaka 2020/2021.

(vii) Vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano kupungua kutoka 81 mwaka 2014/2015 hadi 45 mwaka 2021 kwa kila vizazi hai 1,000.

(viii) Vifo vya akinamama wajawazito wakati wa kujifungua kupungua kutoka 432 mwaka 2014/2015 hadi 250 mwaka 2020/2021 kwa kila vizazi hai 100,000.

(ix) Huduma ya maji safi na salama kwa maeneo ya vijijini kuongezeka kutoka 67% mwaka 2014/2015 hadi 80% mwaka 2020/2021.

(x) Uzalishaji wa umeme kuongezeka kutoka *Megawatt* 1,501 mwaka 2015 hadi *Megawatt* 4,915 mwaka 2020 na usambazaji wa umeme kufikia 60% ya Watanzania mwaka 2020 ikilinganishwa na 36% hivi sasa.

(xi) Kuongeza mauzo ya bidhaa za viwandani nje ya nchi kutoka asilimia 24 mwaka 2014 hadi asilimia 30 mwaka 2020 ya mauzo yote nje ya nchi.

(xii) Kujitosheleza katika utengezeji wa sare na viatu kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na katika vyombo vya ulinzi na usalama.

(xiii) Idadi ya watalii kuongezeka kutoka 1,140,156 mwaka 2014 hadi 2,000,000 mwaka 2020 na mapato yatokanayo na utalii kuongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni mbili mwaka 2014 hadi dola za kimarekani bilioni 3.6 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za kimkakati za kuendeleza viwanda nchini na malengo yameelezwa kwa kirefu katika Sura ya Nne ya Kitabu cha Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango utawezesha ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda na kuimarisha jitihada za kukuza uchumi na kuondoa umaskini wa kipato. Pia ustawi wa jamii ya Watanzania utakuwa bora zaidi kutokana na kuongezeka kwa fursa za ajira na biashara kufuatia kuongezeka kwa viwanda nchini. Kwa kujumla, matokeo ya utekelezaji wa mpango huu ni pamoja na kuimarika kwa kasi ya ukuaji mpana wa uchumi kwa manufaa ya wananchi walio wengi ambapo uchumi, kama nilivyosema, unatarajiwa kukua kutoka asilimia saba mwaka 2015 hadi asilimia 10 mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuhitimisha. Mnamo tarehe 9 Disemba 2016, tutaadimisha miaka 55 ya Uhuru wa nchi yetu. Maana yake ni kuwa kiumri nchi yetu si changa tena. Ni nchi yenye umri wa mtu mzima anayepaswa kuwa na familia yake na uwezo wa kujitegemea kimaisha na kiuchumi. Hivyo basi, kama nchi hatupaswi kuwa wategemezi, sharti tujitegemee. Katika hili hakuna njia ya mkato. Tunapaswa kujizatiti kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi kutoka vyanzo vyetu vya ndani na kwa nguvu zote. Aidha, matumizi ya starehe ambayo katika hali halisi ya maisha uchumi wetu na mantiki nzima ya kutaka kuondokana na umaskini na utegemezi wa kibajeti, hatuna budi kuondokana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kuondokana nayo kwa vile yanatubebesha mzigo mzito sisi sote kama Taifa lakini hususani walio maskini na wanyonge zaidi katika jamii yetu. Kazi hii siyo rahisi, ni vita inayohitaji mageuzi ya mfumo wa maisha kwa kuukana kwa dhati utamaduni wa kuishi maisha ya kipato tusichokimudu au tunachokipata visivyo halali au bila kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua baadhi ya watu hasa wale wachache waliokuwa wananufaika zaidi na mfumo huu mageuzi haya yatawauma na watajaribu kuyapinga. Ndiyo sababu Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amekuja na kauli ya kutumbua majipu. Wote tunafahamu kuwa kutumbuliwa jipu kunaambatana na maumivu makali, lakini hii ndiyo njia pekee ya kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nisisitize kuwa Serikali ya Awamu ya Tano haitaona huruma wala kuchoka katika kutoa tiba hii kwa wahusika wote katika jamii yetu. Watu wachache wanaonenepa juu ya migongo ya maskini lazima watumbuliwe. Hakuna kurudi nyuma. Habari ya mjini ni mbele kwa mbele. Huruma yetu na wajibu wetu mkubwa ni kwa wachapakazi na maskini wa nchi yetu ambao wameendelea kuteseka kwa miaka mingi kwa kukosa

malipo stahili kwa jasho lao na hata kukosa mahitaji ya msingi na huduma bora. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa viwanda ndiyo njia ya uhakika katika kufikia maendeleo endelevu. Ilitumiwa na nchi nyingi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi duniani. Kama wenzetu wanatokea hapo, basi ni busara kwetu kupita njia hiyo hiyo lakini kwa kutumia vizuri fursa tulizo nazo hapa nchini na zinazochomoza kikanda na kimataifa, lakini pia kujiandaa kukabiliana na vihatarishi vilivyoko mbele yetu. Tumeamua kujipanga upya kujenga uchumi wa viwanda lakini lililo dhahiri katika njia hii ni kuwa kutakuwa na vikwazo ikiwa ni pamoja na ushindani mkali katika masoko ya mitaji na bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuvuke tunahitaji dhamira ya dhati ya kuibadilisha nchi yetu kuwa sehemu bora zaidi ya kuishi kwa wananchi wetu wote.kubwa kwetu ni kushikamana na kuamini katika njia tuliyoichagua kupita. Nawaomba Watanzania wenzangu tushirikiane ili kumsaidia Rais wetu kutuongoza na kutuvusha kufikia azma yetu ya kujenga uchumi wa viwanda, wenye kutoa ajira na ujira mzuri na hatimaye kila mmoja wetu aweze kufaidi matunda ya uhuru wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya kazi kwa bidii, nidhamu ya hali ya juu, maarifa, uadilifu, kutumia teknolojia na ubunifu na kuzingatia sheria na taratibu za nchi yetu ili kudumisha amani yetu ndiyo misingi itakayotuvusha kutoka hapa tulipo sasa. Kila Mtanzania ni lazima ajitoe kutumikia nchi yake na watu wake. Naamini kabisa, kama tukifanya haya chini ya uongozi shupavu na uthubutu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Jemedari wetu, huu ndiyo utakuwa mwanzo wa Tanzania mpya ambayo wote tunaitamani. Tanzania yenye neema, Tanzania shindani ambayo itakuwa nguvu kuu ya kiuchumi yaani *economic power house* katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwa unyeyekevu nimalize hotuba yangu kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na kitabu cha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021 inapatikana katika tovuti za Wizara ya Fedha na Mipango ya *www.mof.go.tz* na *www.mipango.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021. Mungu ibariki safari yetu ya 'hapa kazi tu' ya kuijenga Tanzania mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO 2016/17-2020/21 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 unaolenga kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu na hivyo kutekeleza azma ya Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 ya kuwa na nchi ya uchumi wa kipato cha kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa mwaka 2011 Serikali ilitoa maamuzi ya kuwa na Mpango Elekezi wa miaka 15 kwa ajili ya kutekeleza Dira ya Maendeleo ya mwaka 2015 kwa utaratibu wa kuwa na vipindi vitatu vya utekelezaji vyenye dhima mahsusi yaani Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano wa 2011/2012 hadi 2015/2016 uliolenga kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 unaolenga kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na mwisho kuwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utakaoanzia mwaka 2021/2022 hadi 2025/2026 utakaolenga kujenga ushindani wa kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango ambapo Serikali ilielezea uamuzi wa kuunganisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA ili kuepuka kutekeleza mipango pacha na kutawanya rasilimali za Taifa kwa vipaumbele vinavyofanana. Kamati imechambua kwa kina mpango huu ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango uliopita wa mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016 ili kutoa fursa kwa Bunge lako Tukufu kupata picha halisi ya utekelezaji wa mipango yetu tunayojiwekea na mwelekeo wake na hivyo kuishauri Serikali ipasavyo. Kaulimbiu ya Mpango huu ni kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu inatoa mtazamo mpya wa kuelekeza nguvu za Kitaifa katika maeneo ambayo yataleta ukuaji wa uchumi kupitia mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umasikini. Katika kipindi cha miaka mitano, uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7. Aidha, toka mwaka 2013 Pato la Taifa limekuwa likiongezeka kwa kiasi cha asilimia saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukuaji wa uchumi ni mawasiliano kwa asilimia 15, utawala wa umma asilimia 12.6, ujenzi asilimia 10.5, huduma za fedha na bima asilimia 10 na uchukuzi asilimia 9.5. Sekta ya kilimo imekua kwa asillimia 3.4 hii ni kasi ndogo kwa ukuaji ingawa inachangia zaidi ya asilimia 25 kwenye Pato la Taifa na kuajiri takribani asilimia 79 ya Watanzania. Aidha, sekta ya viwanda ambayo ndiyo mwelekeo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo imechangia kwa wastani wa asilimia 6.6 tu kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha tarakimu moja kutoka asilimia 6.1 mwaka 2014 hadi asilimia 5.6 mwaka 2015. Mfumuko wa bei unategemewa kuendelea kuwa chini ya lengo la muda wakati la asilimia tano ifikapo Juni 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwenendo wa thamani ya shilingi ya Tanzania umekuwa si wa kuridhisha. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 thamani ya shilingi ilishuka kutoka shilingi 1,401.79 mwaka 2010 hadi shilingi 2,180 Disemba, 2015.

Kamati inaona suluhisho la kudumu la kutengemaa kwa thamani ya shilingi ni kupunguza kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali za nje *(current account deficit)*. Hii itawezekana tu endapo mauzo yetu nje yataongezeka na kuziba pengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la taifa limeendelea kukua na kufika shilingi tirioni 36.39 mwezi Desemba 2015 tofauti na ilivyokuwa 2011/2012 ambapo ilikuwa ni shilingi tirioni 14.4. Kamati inatambua kwamba ili nchi yoyote duniani ipige hatua ya maendeleo ni lazima ikope. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kwamba jambo la msingi la kuzingatia ni kuhakikisha mikopo yote inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo na yenye manufaa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na tathmini iliyofanyika mwezi Septemba 2015 imeonesha kwamba deni la taifa ni himilivu kulingana na vigezo sita vinavyotumika kimataifa ambavyo ni kwanza, uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa pato la Taifa (*GDP*). Ukomo ni asilimia 50 na kwa sasa ni asilimia 20.9. Pili, uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa ya mauzo ya nje ambapo ukomo ni asilimia 200, uwiano wa sasa wa deni letu ni asilimia 104.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha tatu ni uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa mapato ya ndani ambapo ukomo ni asilimia 300, uwiano wetu kwa sasa ni asilimia 157.2 . Kigezo cha nne ni malipo ya deni la nje kwa mauzo ya nje ukomo ni asilimia 25 ambapo kwa sasa uwiano wetu ni asilimia 8.7. Tano, uwiano wa malipo ya deni la ndani kwa mapato ya ndani ambapo ukomo inapaswa iwe asilimia 22 kwa sasa ni asilimia 13. Sita, uwiano wa deni lote la nje na la ndani kwa thamani ya sasa kwa pato la taifa ambapa ukomo inapaswa kuwa asilimia 74 kwa sasa ni asilimia 36.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa vigezo vyote bado deni la taifa linaonekana linahimilika, isipokuwa Kamati inashauri kwamba mikopo inayokopwa ielekezwe katika kutekeleza miradi ya maendeleo. Pia ielekezwe zaidi katika kutekeleza miradi ya maendeleo kuliko kulipia madeni ambayo yapo na Serikali ijikite zaidi kukopa nje kuliko kukopa ndani ili kuiwezesha sekta binafsi na yenyewe kuweza kukopa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikikopa kwenye masoko ya ndani kupitia minada na dhamana ya Serikali na hati fungani na mabenki mengi yamekuwa yakinunua dhamana na hati za Serikali kutokana na faida kubwa (*profit margin)* inayotokana na kuikopesha Serikali. Pia kuikopesha Serikali kumeonekana kwamba hakuna vihatarisha ukilinganisha na ukopaji wa sekta binafsi na kitendo hiki pia kinaongeza riba katika mikopo ya sekta binafsi. Kwa hiyo, Kamati inashauri Serikali ijielekeze kukopa zaidi nje kuliko kukopa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016 ulikuwa wa awamu ya kwanza kati ya awamu tatu ya mpango elekezi wa miaka 15 wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025. Ili kuleta mabadiliko yatakayoifanya Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, malengo ya Mpango huu yalikuwa ni kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii. Malengo haya yote yalielekezwa katika utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele ambavyo vilikuwa ni miundombinu, kilimo, viwanda, madini, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii na miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti ilichambua kwa kina utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele, muda wa kati na muda mrefu wa utekelezaji wa kila kila kipaumbele na uwajibikaji wa wataalam wa sekta husika katika kila kipaumbele. Mchanganuo huo umetoa picha halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo mpaka sasa. Kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inatoa tathmini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya kisekta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miundombinu ya reli, Serikali imefanikiwa kukarabati na kununua vitendea kazi kama vile vichwa vya treni, mabehewa na mabehewa ya *brake*. Vilevile, Serikali imeendelea kukamilisha uchambuzi yakinifu wa reli ya Musoma, Arusha, Mtwara, Songea na Liganga. Hata hivyo, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo uliweka lengo la kukarabati kilometa 2,707 za reli ya kati ifikapo mwaka 2015. Hadi kufikia mwaka 2015 ni kilometa 136 za reli ya kati ndizo zimekarabatiwa. Hii ni sawa na 5.02% tu ya lengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya nishati, Kamati imeipongeza Serikali kwa hatua nzuri iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya nishati ya umeme kama vile ujenzi wa bomba la gesi, miradi ya umeme ya Kinyerezi I na II, usambazaji wa umeme vijijini na kupunguza gharama ya umeme kwa kuondoa gharama za huduma yaani *service charge*. Kamati inaishauri Serikali iongeze juhudi katika kumalizia miradi ya nishati ya umeme ambayo haikukamilika katika Mpango wa Maendeleo wa Kwanza ili iweze kuchochea uchumi wa viwanda. Kamati pia inasisitiza Serikali kutimiza lengo lake la kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka megawati 900 hadi megawati 2,780 kama ilivyokuwa imeainishwa kwenye Mpango wake wa Kwanza wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio ya kuridhisha katika kuboresha na kujenga miundombinu ya barabara iliyounganisha mikoa karibu yote ukiacha Mikoa ya Manyara na Tanga, Ruvuma na Mtwara na Kigoma na Tabora. Serikali pia iliweka lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami kilometa 5,204 ifikapo mwaka 2015. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2014 kilometa 2,775 za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami. Utekelezaji huu ni sawa na 53.3% ya lengo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kulipa madeni ya wakandarasi kwa wakati na kusimamia ubora wa barabara zinazojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mpango wa kununua ndege tatu. Pamoja na mpango huu mzuri, Kamati inashauri Serikali iharakishe kutatua matatizo ya kiutawala, kifedha na kiuendeshaji ya shirika la *ATCL* ili iliwezeshe kujiendesha kwa ufanisi pale ndege zake zitakapopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya bandari Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza juhudi za kushughulikia mizigo bandarini ili kufikia lengo la tani milioni 18 kwa mwaka kama ilivyowekwa kwenye Mpango wa Kwanza kwa miaka mitano. Hadi sasa Serikali imefanikiwa kushughulikia tani milioni 14.7 tu kwa mwaka 2015. Aidha, bado kuna changamoto kubwa katika utoaji wa mizigo katika Bandari za Tanga, Mwanza, Kigoma, Kyela, Lindi, Kilwa na Mafia. Aidha, Kamati inashauri Serikali kukamilisha ujenzi wa gati namba 13

na 14 katika bandari ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia mizigo pamoja na kuboresha Bandari ya Tanga na Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote lililoendelea duniani linahitaji kuwa na nguvu kazi yenye uweledi, ujuzi na taaluma mbalimbali inayokidhi mahitaji ya soko na itakayokuwa na chachu ya kuleta matokeo thabiti katika sekta husika. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia maendeleo ya rasilimali na kufikia takribani ya 70% ya lengo la Mpango. Mifano mizuri inaonekana katika udahili wa vyuo vikuu vya elimu ya juu kutoka wanafunzi 262,376 mwaka 2010/2011 hadi kufikia wanafunzi 362,880 mwaka 2013/2014. Pia ujenzi wa vyuo mbalimbali kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma na *campus* ya Mlonganzila Chuo Kikuu cha Tiba cha Muhimbili. Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kuongeza ubora wa elimu inayotolewa katika shule za msingi, sekondari na vyuo ili kutoa ushindani katika soko la ajira katika Ukanda wa Afrika Mashariki na *SADC*. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mpango wa azma ya utoaji wa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya ni pamoja na kupunguza idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 81 mwaka 2010 hadi 54 mwaka 2013 kwa kila watoto 1000 na vifo vya mama wajawazito kutoka 454 mwaka 2010 hadi 410 mwaka 2014 kwa kila vizazi hai laki moja. Bado juhudi zinahitajika zaidi ili tuweze kufikia lengo la kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kusimamia ipasavyo kupunguza maambukizi mapya na magonjwa mbalimbali ikiwemo UKIMWI, kifua kikuu, ukoma na malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi zote zimeiwezesha Tanzania kuvuka malengo ya milenia. Kamati inaishauri Serikali ijipange vizuri zaidi katika kuongeza bajeti ya afya ifikie 15% kwa mujibu wa Tamko la Abuja. Malengo haya yataisaidia Serikali kuboresha zaidi huduma za afya, upatikanaji wa vifaa tiba na kuongeza watumishi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwepo na mafanikio na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo. Yamekuwepo mafanikio katika sekta ya maji, Kamati inaishauri Serikali kutatua vikwazo vyote ambavyo vimeshindikana kutanzuliwa katika awamu ya kwanza wa Mpango wa Miaka Mitano uliopita ikiwemo sekta ya uvuvi, sekta ya misitu pamoja na sekta ya kilimo ambazo zimeonekana kuwa na changamoto kubwa pamoja na kwamba sekta ya kilimo imekuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepitia na kuchambua Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 hadi

2020/2021. Kamati imepitia na kuchambua Mpango huu ambao umeainisha maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Kukuza uchumi na kujenga msingi wa uchumi wa viwanda;

(ii) Kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu; na

(iii) Kujenga mazingira wezeshi ya uendeshaji wa biashara na uwekezaji, kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepata fursa ya kupitia miradi yote ya kimkakati iliyoainishwa na Serikali kwenye Mpango huu ambayo imegawanywa kwenye maeneo makuu matano yafuatayo:-

(i) *Central Development Corridor;*

(ii) *North West Corridor* ya Tanga;

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome kwa kiswahili, kwanza ni Ukanda wa Kati; Ukanda wa Kaskazini wa Magharibu ya Tanga;) Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara; upatikanaji wa umeme wa uhakika na utoaji wa mafunzo mbalimbali na wataalam maalum katika maendeleo ya viwanda, watu na sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchambuzi ambao umefanywa na Kamati, ili Kanda hizi tano au maeneo hayo matano yote yaweze kufanikiwa katika maendeleo yake, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa *Central Corridor* yaani Ukanda wa Kati suala la kukamilisha ujenzi wa reli ya kati ni la msingi sana ili ukanda huo uweze kufikia maendeleo ambayo tunayakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Ukanda wa Mtwara ili mipango ile ambayo imewekwa katika ukanda ule iweze kufikiwa, suala la ujenzi wa reli ya Mtwara hadi Liganga na Mchuchuma na Mbamba Bay ni muhimu sana na upatikanaji wa gesi katika maeneo ya Mtwara na Ukanda wa Kusini ili kuweza kuendeleza viwanda vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukanda wa Kaskazini, Kamati inapendekeza au inashauri kuharakisha maandalizi ya mazingira ya ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta kutoka Ziwa Albert Uganda mpaka Tanga.

Pia ni vema Bunge likapewa taarifa kamili kuhusu mradi huo kwa sababu kumekuwa na taarifa nyingi za kuleta mkanganyiko. Lakini pia Kamati ingependa *corridor* hiyo pamoja na ujenzi wa bomba la mafuta basi uende na miradi mingine ambayo itafanya *corridor* hiyo kuwa na mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali kutekeleza mradi wa bandari ya Bagamoyo ambapo ujenzi wake unatarajiwa kuanza Januari 2017 na kukamilika mwaka 2020. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wakazi wa Mbegani ili kupisha ujenzi huo. Kamati pia inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za ulipaji wa fidia katika maeneo yote yanayotegemewa kuanzisha na kuendeleza *EPZA* na *SEZ* ili kufungulia fursa ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Mpango wa Pili wa Maendeleo kwa kiasi kikubwa yanategemea upatikanaji wa rasilimali fedha. Ugharamiaji wa Mpango umegawanyika katika vyanzo vikuu vitatu ambavyo ni Serikali Kuu, sekta binafsi na pia mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa Mpango husika unaonesha utaongezeka kwa kiasi cha shilingi trilioni 28 mwaka 2016/2017 hadi kufikia shilingi trilioni 149.3.

Aidha, Mpango umeainisha namna Serikali itakavyovutia wawekezaji wa ndani na nje. Kamati inashauri kuhuisha sheria zote zile ambazo zinakinzana na uvutiaji wa uwekezaji kutoka nje pamoja na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba maoni yote ya Kamati yaingizwe kwenye *Hansard* yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa ushirikiano mkubwa ambao wameipatia Kamati hii. Ni imani yetu kabisa kwamba ushauri huu ukizingatiwa Mpango huu utaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) unaolenga kujenga msingi wa Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya watu na hivyo kutekeleza azma ya Dira ya Maendeleo 2025 ya kuwa nchi yenye uchumi wa kipato cha kati (*Middle income country*).

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kuwa mwaka 2011, Serikali ilitoa maamuzi ya kuwa na Mpango Elekezi wa Miaka 15 (roadmap) kwa ajili ya kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2015 kwa utaratibu wa kuwa na vipindi vitatu vya utekelezaji vyenye dhima mahususi yaani; Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) ***uliolenga kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii***; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) ***unaolenga kujenga msingi wa uchumi wa viwanda***; na mwisho kuwa na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) ***utakaolenga kujenga ushindani wa kibiashara***.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango na kuelezwa kwamba, Serikali imeamua kuunganisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na MKUKUTA ili kuepuka kutekeleza Mipango pacha na kutawanya rasilimali za Taifa kwa vipaumbele vinavyofanana. Kamati imechambua kwa kina mpango huu ikiwa pamoja na kufanya tathmini fupi ya utekelezaji wa Mpango uliopita (2011/12-2015/16) ili kutoa fursa kwa Bunge lako tukufu kupata picha halisi ya utekelezaji wa mipango yetu tunayojiwekea na mwelekeo wake na hivyo kuishauri Serikali ipasavyo. Kauli mbiu ya Mpango huu "**Kujenga Msingi wa Uchumi wa Viwanda na Maendeleo ya watu**" inatoa mtazamo mpya wa kuelekeza nguvu za kitaifa katika maeneo ambayo yataleta ukuaji wa uchumi kupitia mapinduzi ya viwanda.


## 2.0 TATHMINI FUPI YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2011/12-2015/16)

### 2.1. Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi jumla

### a) Ukuaji wa Pato la Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Ukuaji wa Pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini. Katika kipindi cha miaka mitano uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 6.7. Aidha, toka mwaka 2013 Pato la Taifa limekuwa likiongezeka kwa kiasi cha asilimia 7.

**Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Pato la Taifa**





***Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango***

**Mheshimiwa Spika**, sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukuaji wa uchumi ni Mawasiliano (15.0%), Utawala wa Umma (12.6%), Ujenzi (10.5%); huduma za Fedha na Bima (10.4%) na Uchukuzi (9.5%). Sekta ya Kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uvuvi) imekua kwa asilimia 3.4 hii ni kasi ndogo ya ukuaji, ingawa kinachangia zaidi ya asilimia 25 kwenye Pato la Taifa na kuajiri takribani asilimia 79 ya watanzania. Aidha, Sekta ya Viwanda ambayo ndio mwelekeo wa Mpango wa Pili wa maendeleo imechangia kwa wastani wa asilimia 6.6 tu kwenye Pato la Taifa.

**b) Mfumuko wa bei**

**Mheshimiwa Spika,** mfumuko wa bei umeendelea kuwa kwenye kiwango cha tarakimu moja kutoka asilimia 6.1 kwa mwaka 2014 hadi asilimia 5.6 mwaka 2015. Mfumuko wa bei unategemewa kuendelea kuwa chini ya lengo la muda wa kati la asilimia 5 ifikapo Juni 2016. Hii itawezekana endapo kutaendelea kuwepo udhibiti wa bei ya mafuta katika soko la dunia; uwepo wa chakula cha kutosha katika masoko ya ndani na nchi jirani (mfumuko wa bei yake unaridhisha) na udhibiti wa sera ya fedha zinazolenga kutunza thamani ya fedha kwa kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Kielelezo Na.2: Mfumuko wa Bei**




***Chanzo:Wizara ya Fedha na Mipango***

**c) Thamani ya shilingi**.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa thamani ya Shilingi ya Tanzania umekuwa si wa kuridhisha. Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015; thamani ya shilingi ilishuka kutoka shilingi 1,401.79 mwaka 2010 hadi shilingi 2,180 Desemba 2015. Kamati inaona suluhisho la kudumu la kutengamaa kwa thamani ya shilingi ni kupungua kwa nakisi ya urari wa biashara ya bidhaa (balance of trade), huduma na uhamisho mali nchi za nje (*current account deficit*). Hii itawezekana tu endapo mauzo yetu nje ya nchi yataongezeka na kuziba pengo hilo.

**d) Deni la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa limeendelea kukua na kufikia Shilingi trilioni 36.39 mwezi Desemba 2015 tofauti na ilivyokuwa shilingi trilioni 14.4 kwa mwaka 2011/12. Kwa sasa Deni la Taifa limefikia takribani asilimia 44.9 ya Pato la Taifa. Deni limeendelea kukua kutokana na Serikali kuendelea kukopa kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika** Kamati inatambua kwamba ili nchi yoyote Duniani ipige hatua ya maendeleo ni lazima ikope. Hata hivyo Kamati inatoa angalizo kwamba jambo la msingi la kuzingatia ni kuhakikisha kwamba mikopo yote inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye manufaa kwa uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** kulingana na tathmini iliyofanyika mwezi Septemba 2015 imeonyesha kwamba Deni la Taifa ni himilivu kulingana na vigezo sita vinavyotumika kimataifa ambavyo ni;

i. Uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa Pato la Taifa (GDP) ukomo ni asilimia 50 ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 20.9.

ii. Uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa mauzo ya nje ukomo ni asilimia 200 ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 104.4.


iii. Uwiano wa deni la nje kwa thamani ya sasa kwa mapato ya ndani ukomo ni asilimia 300 ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 157.2.

iv. Malipo ya deni la nje kwa mauzo ya nje ukomo ni asilimia 25 ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 8.7.

v. Uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani ukomo ni asilimia 22 ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 13.

vi. Uwiano wa deni lote (deni lanje na deni la ndani) kwa thamani ya sasa kwa pato la taifa ukomo mi asilimia 74 ambapo kwa sasa tumefikia asilimia 36.8.

**Kielelezo Na. 3: Mwenendo wa Deni la Taifa (2010-2015)**





| | Deni la Ndani | Deni la Nje | Jumla ya Deni la Taifa |
|---|---|---|---|
| 2009/10 | 2,254 | 7,858 | 10,112 |
| 2010/11 | 3,707 | 10,735 | 14,442 |
| 2011/12 | 4,076 | 12,430 | 16,506 |
| 2012/13 | 5,775 | 15,634 | 21,409 |
| 2013/14 | 7,144.50 | 19,343 | 26,487 |
| 2014/15 | 9,400 | 25,600 | 35,000 |

**e) Mwenendo wa Huduma za kibenki na viwango vya riba**

**Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha miaka mitano (2011 - 2015), viwango vya riba katika masoko ya fedha vimeendelea kutegemea nguvu ya soko na hali ya ukwasi unaotokana na sera za fedha na kibajeti. Viwango vya riba za dhamana za Serikali umeongezeka kutoka asilimia 8.3 mwaka 2011 hadi asilimia 14.2 mwaka wa fedha 2013 na baadaye kupungua hadi asilimia 12.9. katika mwaka wa fedha 2015. Riba za mikopo kwenye mabenki ya biashara katika kipindi hicho ziliongezeka kutoka asilimia 15.0 mwaka wa fedha 2011 na kufikia asilimia 16.3 mwaka 2014 kabla ya kushuka kidogo na kufikia asilimia 16.1 katika mwaka 2015. Riba za amana ziliongezeka kutoka asilimia 8.4 katika mwaka 2011 na kupanda hadi kufikia asilimia 11.0 katika mwaka 2014 kabla ya kushuka kidogo kufikia asilimia 10.4 katika mwaka wa fedha 2015.

**Mheshimiwa Spika;** Kutokana na mwenendo huu, tofauti kati ya riba za mikopo na amana za mwaka mmoja imekuwa ikipungua mwaka hadi mwaka ambacho ni kiashiria kizuri cha kupungua kwa gharama za fedha kwa wawekezaji katika sekta binfasi;mfano mwaka 2011 tofauti hiyo ilitoka asilimia 6.6 na baada ya hapo imeendelea kuwa chini ya asilimia 3.8 hadi mwaka 2015.

**Kielelezo Na. 4: Mwenendo wa Riba (2011-2015)**




***Chanzo: Benki Kuu***

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa ikikopa kwenye masoko ya ndani kupitia mnada na dhamana ya Serikali *(Treasury Bills)* na hati fungani (Treasury Bonds). Mabenki mengi yamekuwa yakinunua dhamana na hati za Serikali kutokana faida kubwa (profit margin) inayopatikana pia kuikopesha Serikali hakuna vihatarishi *(Risk free)* ukilinganisha na ukopeshaji kwa sekta binafsi. Mwenendo unaonyesha kuwa wakati riba za dhamana ya Serikali zinapanda pia riba ya mikopo binafsi nayo kwenye mabenki inapanda kwa sababu ya riba za dhamana hutumika kama kiashiria cha msingi *(base rate)* kwenye mikopo ya Sekta Binafsi. Jedwali hapa chini linaonyesha kuwa Serikali imekuwa ikikopa zaidi (rollover) kulipia madeni ya ndani kuliko kugharamia bajeti ya Serikali yake. Mwenendo wa dhamana na hati za Serikali zimebainishwa kwenye kielelezo Na.5.

**Kielelezo Na.5: Mwenendo wa dhamana na hati za Serikali**

| **Soko la fedha** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** | **2014/15** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mapato ya Mauzo** | **1518.4** | **1735.2** | **2429.3** | **2602.3** | **2927.0** |
| Hatifungani | 755.9 | 402.8 | 966.7 | 985.7 | 1158.8 |
| Dhamana | 762.5 | 1332.3 | 1462.6 | 1616.6 | 1768.2 |
| **Matumizi ya Mapato** | **1518.4** | **1735.2** | **2429.3** | **2602.3** | **2927.0** |
| Kulipa deni | 720.2 | 1326.9 | 1734.5 | 1528.2 | 2064.8 |
| Kugharamia bajeti | 798.2 | 408.3 | 694.8 | 1074.1 | 862.2 |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kupunguza kukopa katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya Bajeti kwa kupitia dhamana Serikali na hati fungani. Badala yake Serikali ijikite zaidi katika kuongeza udhamini wa wakopaji wadogo (credit gurantee schemes) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenyewe (lease finance). Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi Soko la Mitaji (Liberization of Capital Market) ili kupunguza athari za Serikali kukopa kwenye soko la ndani.

## 2.2 Tathmini ya utekelezaji wa sekta zilizopewa kipaumbele kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Taifa (2011/12-2015/16).

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Maendeleo (2011/12 – 2015/16) ulikuwa ni awamu ya Kwanza kati ya tatu ya Mpango Elekezi *("roadmap")* wa Miaka 15 wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ili kuleta mabadiliko yatakayoifanya Tanzania kuwa nchi yenye hadhi ya kipato cha kati (middle income country) ifikapo mwaka 2025. Malengo ya Mpango huu yalikuwa ni kutanzua vikwazo vya kiuchumi, kupunguza umaskini na kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii. Malengo haya yote yalielekezwa katika utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele ambavyo ni **Miundombinu** (*Reli, barabara, bandari, usafiri wa* anga na nishati); **Kilimo** (*Mazao, Mifugo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi*); **Viwanda; Madini; maendeleo ya rasilimali watu na huduma za jamii** *(Afya, Elimu na Maji)* **na miradi maalum ya kimkakati** *(Flagship Projects).*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilichambua kwa kina utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa kila sekta kwa kuangalia upatikanaji wa fedha kwa kila kipaumbele; muda wa kati na mrefu wa utekelezaji wa kila kipaumbele;na uwajibikaji wa wataalamu wa sekta husika katika kila kipaumbele. Mchanganuo huu umetoa picha halisi ya utekelezaji wa Mpango wa kwanza wa Maendeleo mpaka sasa. Kwa mantiki hii, Kamati ya Bajeti inatoa tathmini yake ya utekelezaji wa vipaumbele vya kisekta kama ifuatavyo:

### 2.2.1. Sekta ya Miundombinu (Reli, Nishati, Barabara, Bandari na Usafiri wa anga)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia malengo makuu yaliyowekwa katika maeneo ya reli, barabara, bandari na usafiri wa anga. Pamoja na kwamba Serikali imepata mafanikio katika utekelezaji wa baadhi ya miradi, hata hivyo Tathmini inaonyesha kuwa miradi mingi ipo chini ya lengo la utekelezaji kwa asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika**, katika **miundombinu ya reli** Serikali imefanikiwa kukarabati na kununua vitendea kazi kama vile vichwa vya treni, mabehewa

na mabehewa ya breki. Vilevile Serikali imeendelea kukamilisha Uchambuzi yakinifu wa reli ya Musoma-Arusha na Mtwara-Songea-Liganga. Hata hivyo, Mpango wa kwanza wa Maendeleo uliweka lengo la kukarabati kilometa 2,707 za Reli ya Kati ifikapo mwaka 2015, hadi kufikia mwaka 2015 kilometa 136 za reli ya kati ndizo zimekarabatiwa hii ni sawa na asilimia 5.02 tu ya lengo.

**Mheshimiwa Spika, Kuhusu Sekta ya Nishati** Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua nzuri iliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya nishati ya umeme kama vile ujenzi wa bomba la gesi; miradi ya umeme ya Kinyerezi I na II; usambazaji wa umeme vijijini (REA); kupunguza gharama ya umeme kwa kuondoa gharama za huduma (*Service charge)*. Kamati inaishauri Serikali iongeze juhudi katika kumaliza miradi ya nishati ya umeme ambayo haikukamilika katika Mpango wa Maendeleo wa Kwanza ili iweze kuchochea uchumi wa Viwanda. Kamati inasisitiza Serikali kutimiza lengo lake la kuongeza uzalishaji wa umeme kutoka 900 MW hadi 2,780 MW kama lilivyokuwa limeainishwa kwenye Mpango wa Kwanza wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa mafanikio ya kuridhisha katika kuboresha na kujenga **miundombinu ya barabara** iliyounganisha mikoa yote Tanzania**.** Serikali iliweka lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami kilomita 5,204 ifikapo mwaka 2015. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2014 kilomita 2,775 za barabara zimejengwa kwa kiwango cha lami. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 53.3 ya lengo. Kamati inashauri Serikali kuendelea kulipa madeni ya wakandarasi kwa wakati na kusimamia ubora wa barabara zinazojengwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuwa na mpango wa kununua ndege tatu. Pamoja na mpango huu mzuri, Kamati inashauri Serikali iharakishe kumalizia kutatua matatizo ya kiutawala, kifedha na kiuendeshaji ya shirika la ATCL ili liweze kujiendesha kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu **sekta ya bandari**, kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza juhudi za kushughulikia mizigo bandarini ili kufikia lengo la tani milioni 18 kwa mwaka kama lilivyowekwa kwenye Mpango wa kwanza wa miaka mitano. Hadi sasa Serikali imefanikiwa kushughulikia tani milioni 14.7 tu kwa mwaka 2015. Aidha, bado kuna changamoto kubwa katika utoaji wa mizigo katika bandari za Tanga, Mwanza, Kigoma, Kyela, Kilwa, Lindi na Mafia. Aidha, Kamati inashauri Serikali kukamilisha ujenzi wa gati namba 13 na 14 katika bandari ya Dar es Salaam ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia mizigo pamoja na kuboresha bandari ya Tanga na Mtwara.

### 2.2.2. Maendeleo ya Rasilimali Watu na Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji)

**Mheshimiwa Spika**, Taifa lolote lililoendelea Duniani linahitaji kuwa na nguvu kazi yenye weledi, ujuzi na taaluma mbalimbali inayokidhi mahitaji ya soko na itakayokuwa chachu ya kuleta matokeo thabiti katika sekta husika. Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia maendeleo ya rasilimali na kufikia takribani asilimia 70 ya lengo la Mpango. Mifano mizuri inaonekana katika udahili wa vyuo vikuu vya elimu ya juu kutoka wanafunzi 262,376 (mwaka 2010/11) hadi kufikia wanafunzi 362,880 (mwaka 2013/14) na pia ujenzi wa vyuo mbalimbali kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma na kampasi ya Mlonganzila (chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili). Kamati inaishauri Serikali kusimamia na kuongeza ubora wa elimu inayotolewa katika shule za msingi, sekondari na vyuo ili kutoa ushindani katika soko la ajira katika ukanda wa afrika mashariki na SADC. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza azma yake ya utoaji elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi Sekondari.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya afya ni pamoja na kupunguza idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 81 kwa mwaka 2010 hadi vifo 54 mwaka 2013 kwa kila watoto 1000; na vifo vya mama wajawazito kutoka 454 mwaka 2010 hadi 410 mwaka 2014 kwa kila vizazi hai 100,000. Bado juhudi zinahitajika zaidi ili tuweze kufikia lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kusimamia ipasavyo na kupunguza maambukizi mapya na magonjwa mbalimbali ikiwemo UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma na Malaria. Hatua hizi zote zimeiwezesha Tanzania kuvuka malengo ya Milenia. Kamati inaishauri Serikali ijipange vizuri zaidi katika kuongeza bajeti ya Afya ifikie asilimia 15 kwa mujibu wa Tamko Abuja. Malengo hayo yataisaia Serikali huduma za afya, upatikanaji wa vifaa tiba na kuongeza watumishi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa miradi ya Maji, Serikali imepata mafanikio yafuatayo; Uboreshaji wa vyanzo vya maji vya Ruvu juu na Ruvu chini; Ukamilshaji waujenzi wa Bomba la maji kutoka Ruvu Chini hadi Dar es salaam; Upatikanaji wa maji vijijini umefikia asilimia 72 na upatikanaji wa maji katika miji midogo umeongezeka kutoka asilimia 53 mwaka 2010 hadi 60 mwaka 2015. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa maji ambao umekuwa na mafanikio makubwa katika kugharamia miradi ya maji.

### 2.2.3 Maendeleo ya Kiuchumi na Sera ya kuondoa umasikini

**Mheshimiwa Spika,** kamati ya Bajeti inatambua kuwa mojawapo ya hatua kubwa ya kupiga maendeleo sio tu kukua kiuchumi (GDP Growth) bali ni pamoja na kuhakikisha umaskini wa kipato kwa wananchi unapungua. Ukifuatilia kwa umakini viashiria vya umasikini yaani; umaskini wa kipato (Income

poverty), pengo la umaskini na tofauti ya kipato (Poverty gap) utagundua kuwa jamii wa watu wanaoishi vijijini ndio inayoathirika zaidi na viashiria hivi vya umaskini. Mfano, takwimu zinaonyesha kuwa umaskini wa msingi **(income poverty)** kwa Dar es Salaam ni asilimia 1.5, maeneo mengine ya mijini ni asilimia 14.4 na maeneo ya vijijini ni asilimia 84.1; pengo la umaskini **(poverty gap)** kwa Dar es Salam ni asilimia 0.8, maeneo mengine ya mjini ni asilimia 5.5 na vijijini ni asilimia 7.9; na kwa upande wa tofauti ya kipato **(poverty inequalities)** ni kubwa mara nne zaidi ukilinganisha kati ya jamii inayoishi mjini na ile ya vijijini. Kwa takwimu hizi utaona kuwa tafsiri ya dhana ya kukua uchumi umesaidia kupunguza umaskini sio sahihi sana ukizingatia kuwa sekta tunazozitegemea katika kukuza uchumi wetu mathalani mawasiliano, ujenzi na huduma za fedha n.k hazijumuishi idadi kubwa ya watu na pia shughuli nyingi za sekta hizi zinafanyika katika maeneo ya mjini ambapo kuna idadi ndogo ya watu. Ni wajibu wa Serikali kuhakikisha katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa maendeleo wa Taifa ukuaji wa uchumi unabebwa na sekta zinazohusisha idadi kubwa ya watu mathalani kilimo na viwanda ili ukuaji huu uweze kutiririka na kuwafikia wananchi walio wengi vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutoa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kwa ajili ya kuchochea maendeleo vijijini na mitaa. Tanzania ina jumla ya vijiji na mitaa 16,164 jumla ya kiasi cha fedha zinazohitajika ni shilingi bilioni 808.2 hivyo kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwaandaa wananchi na namana ya uendeshaji wa fedha hizo ili Serikali ifikie malengo yaliyokusudiwa.

### 2.2.4. Kilimo (Mazao, Misitu, Mifugo na Uvuvi )

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya mafanikio katika Sekta ya Kilimo ni; Taifa kuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula (Food Security) kutoka asilimia 111 mwaka 2010 hadi asilimia 125 mwaka 2014/15 na uanzishwaji wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Pamoja na mafanikio hayo bado Lengo la Mpango wa kwanza wa ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka kutoka asilimia 2.7 ya mwaka 2010 na kufikia asilimia 6 mwaka 2015/16 halijafikiwa, Mpaka mwaka 2015 sekta hii ilikuwa kwa asilimia 3.4 tu.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na mafanikio yasiyoridhisha katika kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji. Lengo la Mpango lilikuwa ni kufikia hekta 1,000,000, lakini hadi mwaka 2014/15 eneo lililokuwa chini ya umwagiliaji ni hekta 461,326 sawa na asilimia 46.1. Kamati inaishauri Serikali kwanza kuhakikisha inatenga asilimia 10 ya Bajeti kwa ajili ya Kilimo, pili kukamilisha skimu zote za umwagiliaji nchini ambazo hazijakamilika ili kuongeza ufanisi katika kilimo cha umwagiliaji na iweke mazingira wezeshi katika Sekta ya Kilimo ili kuvutia Sekta Binafsi kuwekeza katika Sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iliweka lengo la shughuli za misitu na uwindaji kukua kwa asilimia 5.9 ifikapo mwaka 2015. Hata hivyo mpaka mwaka 2014 shughuli za uwindaji na misitu zilikua kwa asilimia 5.1. Aidha, kumekuwa na malalamiko mengi katika eneo la uvunaji wa misitu hapa nchini, hivyo ni vema Serikali Serikali ikasimamia kikamilifu Sera na Sheria za uvunaji na upandaji wa misitu na kuweka utaratibu utakaopunguza au kuondoa kabisa malalamiko haya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2014 Tanzania inakadiliwa kuwa na ng'ombe milioni 24.1, mbuzi milioni 15.0, kondoo milioni 4.4, kuku milioni 36.4 na nguruwe milioni 2.10 na kuifanya kuwa nchi ya tatu kwa wingi wa mifugo Barani Afrika. Mpango wa miaka mitano uliweka lengo la kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 5 kwa mwaka. Hata hivyo, wastani wa ukuaji wa sekta hii katika kipindi husika lilikuwa ni asilimia 1.5.

Kamati ingependa Serikali ieleze mafanikio yaliyopatikana baada ya kuongeza ushuru wa kuuza ngozi ghafi nje kutoka asilimia 60 hadi asilimia 80 na kutoza kodi kwa asilimia 10 kwa ngozi iliyosindikwa kwa kiwango cha kati ili kuongeza mapato na mpaka hivi sasa ni viwanda vingapi vinafanya kazi na vilivyoanzishwa ni vingapi.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonyesha kwamba ukuaji wa sekta ya uvuvi kwa Mwaka 2010 ulikuwa asilimia 0.9 wakati mwaka 2015 ulikua asilimia 2.0. Ukuaji huu ni chini ya lengo lililowekwa kwenye mpango wa miaka mitano uliopita la kufikia asilimia 7 ifikapo mwaka 2015. Mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa umeshindwa kufikia lengo la asilimia 5 kutoka asilimia 1.2 ya mwaka 2010 na kufikia asilimia 1.3 tu mwaka 2014. Aidha, Mpango ulilenga kuongeza ajira za kudumu katika sekta ya uvuvi kutoka wavuvi 170,038 mwaka 2009 hadi 200,000 mwaka 2015, hatua iliyofikiwa inaonyesha kwamba ajira zitokanazo na uvuvi zimefikia Wavuvi 183,800 mwaka 2014 hivyo kushindwa kufikia lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya changamoto zinazoikabili sekta hii ni pamoja na uvuvi haramu, wizi wa vitendea kazi vya wavuvi pamoja na uingiaji holela wa meli za uvuvi za kigeni katika eneo la bahari kuu. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha ulinzi bahari kuu (*Deep Sea)* ili kulinda rasilimali hii muhimu.Pia, Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kuwawezesha wavuvi kuwa na zana bora na za kisasa.

### 2.2.5. Maendeleo ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango wa kwanza sekta ya viwanda ilikua kwa wastani wa asilimia 6.6 chini ya lengo la kufikia wastani wa asilimia 11 mwaka 2015. Mwenendo huu hauridhishi katika

mustakabali mzima wa maendeleo ya viwanda nchini. Pamoja na Kwamba Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki (EAC) na Shirika la Biashara Duniani (World Trade Organisation-WTO) pamoja na kuridhia makubaliano ya biashara na ushuru (General Agreement on Trade and Tarrif) bado kamati inaona kwamba Serikali inatakiwa kulinda viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa na huduma kutoka nje zinazoweza kuua viwanda vyetu.

### 2.2.6. Madini

**Mheshimiwa Spika**, Hakukuwa na mabadiliko makubwa katika mchango wa sekta ya madini kwenye pato la taifa (GDP) ambapo kwa mwaka 2010 ulikuwa asilimia 3.4 na mwaka 2014 ulikuwa huo huo wa asilimia 3.4, chini ya lengo la Mpango la kufika asilimia 3.7. Changamoto kubwa katika sekta hii ni namna bora ya kuwajumuisha wachimbaji wadogowadogo kwenye uchangiaji wa pato la Taifa; kuchakata madini hapahapa nchini; mwingiliano wa leseni baina ya wawekezaji wakubwa na wadogo pamoja na kukosekana kwa mitaji kwa wachimbaji wadogo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa vyombo vya kiserikali vyenye jukumu la usimamizi wa uchimbaji na mauzo ya madini haviwajibiki ipasavyo na hivyo kupelekea kupoteza mapato. Mathalani, hivi karibuni tumesikia kuhusu maamuzi ya Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT), kuhusu kampuni ya Acacia ambayo inamiliki migodi iliyokuwa ya African Barric Gold kujenga mazingira ya kukwepa kodi ya zuio yenye thamani ya dola za Marekani 41,250,426 (Sh bilioni 89) iliyokuwa inatakiwa ilipwe TRA kwa kipindi cha miaka minne mfululizo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17- 2020/21)

### 3.1 Malengo na Vipaumbele vya Mpango wa Pili wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imepitia na kuchambua Mpango huu ambao umeainisha maeneo makuu yafuatayo;

i. kukuza uchumi na kujenga msingi wa uchumi wa Viwanda;

ii. Kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya Watu;

iii. kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa Biashara na uwekezaji;

iv. Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango;

### 3.2. Miradi ya Kimkakati *(Flagship Projects)*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepata fursa ya kupitia miradi yote ya Kimkakati iliyoanishwa na Serikali kwenye Mpango huu, ambayo imegawanyika kwenye maeneo makuu matano.

i. Central Development Corridor;
ii. North - West Corridor of Tanga;
iii. Mtwara Development Corridor;
iv. Upatikanaji wa umeme wa Uhakika; na
v. Utoaji wa mafunzo mbalimbali na utaalamu maalumu katika maendeleo ya viwanda, watu na sayansi na teknolojia. Aidha, orodha ya Miradi itakayotekelezwa katika maeneo tajwa hapo juu imeainishwa katika Sura ya 4 ukurasa wa 62 hadi 63 kwenye Kitabu cha Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa 2016/17 – 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na miradi ya kimkakati ambayo Serikali imepanga kutekeleza kamati ina inapendekeza Serikali iondoe changamoto ya upatikanaji wa gesi mkoani Mtwara ili kuwezesha ujenzi wa viwanda vya mbolea kutokana na masalia ya gesi pamoja na Mtwara Petrochemical economic zone, na ukamilishaji wa maandalizi ya awali ya ujenzi wa Reli ya Kutoka Mtwara hadi Mbambabay kwa kiwango cha Standard gauge.Aidha kwa upande wa Central Corridor Serikali ihakikishe inajenga inakamilisha ujenzi wa Reli ya Kati;

**Mheshimiwa Spika** Kwa upande wa North-West Corridor of Tanga, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha maandalizi ya mazingira ya ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Ziwa Albert (Uganda)- Mpaka Tanga haraka iwezekanavyo. Aidha, ni vyema Kamati na Bunge ikapewa taarifa Kamili kuhusu mradi huo kwasababu kumekuwepo na taarifa nyingi zenye kuleta mkanganyiko

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kutekeleza mradi wa Bandari ya Bagamoyo ambao ujenzi wake unatarajiwa kuanza Januari 2017 na kukamilika mwaka 2020. Kamati inashauri Serikali kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wakazi wa Mbegani ili kupisha ujenzi huo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutenga fedha za ulipaji wa fidia katika maeneo yanayotegemewa kuanzisha na kuendeleza EPZA na SEZ zilizopo ili kufungulia fursa ya ukuaji wa uchumi wa viwanda. Pia Kamati inaishauri Serikali kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda ambalo ndilo litakuwa kitovu cha Mji wa Kilimo wa Mkulazi.

**Mheshimiwa Spika,** umeme ni moja ya nyenzo muhimu katika kuendeleza viwanda, Kamati inashauri majiji ya Mbeya na Tanga yaongezwe kwenye mradi wa kuboresha usambazaji wa umeme kwenye majiji.

### 3.3. Uchambuzi na Vyanzo vya Mapato vya kugharamiaji wa Mpango

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya mpango wa pili wa maendeleo kwa kiasi kikubwa yanategemea upatikanaji wa rasilimali fedha. Ugharamiaji wa mpango umegawanyika katika vyanzo vikuu vitatu; kwanza, mapato kutoka Serikali kuu yatakayotokana na mapato ya kodi, yasio ya kodi;pili, Mikopo (ndani na nje); Tatu; Sekta Binafsi kutoka ndani na ile inayotokana na uwekezaji kutoka nje *(Foreig Direct Investment)*. Kiasi cha shilingi trilioni 107 kinahitajika katika kugharamia utekelezaji wa Mpango na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo Serikali inategemea kuchangia kiasi cha shilingi trilioni 59 kwa muda huo, hii ikiwa sawa na kuchangia trilioni 11.8 kwa kila mwaka, sawa na asilimia 40 ya bajeti ya Serikali ya kila mwaka.

**a. Mchango wa Sekta Binafsi.**

**Mheshimiwa Spika**, mchango wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa Mpango husika unaonyesha utaongezeka kutoka kiasi cha shilingi trilioni 28 kwa mwaka 2016/17 hadi trilioni 149.3 ifikapo mwaka 2020/21. Aidha,Mpango umeainisha namna Serikali itakavyovutia wawekezaji wa ndani na nje *(FDI-Foreign Direct Investment)* kushiriki katika utekelezaji wa mpango; kuhamasisha Sekta Binafsi kushirikiana na Sekta ya Umma kupitia utaratibu wa ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (PPP); na kupendekeza mikakati mahususi itakayowezesha Sekta Binafsi kuwekeza katika miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi.

**b. Mchango wa Sekta ya Umma**

**Mheshimiwa Spika;** Serikali ni mdau Mkuu katika utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano, mchango wake ni lazima uonekane kwenye kuweka mazingira wezeshi katika kutekeleza mpango husika. Aidha, Serikali iongeze juhudi katika ukusanyaji wa mapato yake kupitia vyanzo vya kodi, visivyo vya kodi, misaada na mikopo, hati fungani, kuongezea mitaji taasisi zake za fedha, Mfuko wa Mabadiliko ya Tabia Nchi, pamoja na ushirikiano wa kijumuiya na kikanda. Hatua hizi zitawezesha Serikali kupata fedha za kutosha kiasi cha shilingi trilioni 59 kugharamia miradi ya maendeleo kwa kipindi chote cha miaka mitano cha utekelezaji.

## 4.0 USIMAMIZI, UFUATILIAJI NA UTOAJI WA TAARIFA

**Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha usimamizi, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa, Kamati inasisitiza Serikali ijikite zaidi katika mambo yafutayo:-

i. Ihakikishe kunakuwepo na upatikanaji wa taarifa endelevu za utekelezaji (miradi na bajeti) dhidi ya hatua au malengo ya mpango;

ii. Iwe na utaratibu maalumu wa kuchanganua kwa kina taarifa za utekelezaji zitakazokuwa zinawasilishwa kwa kila kipindi maalumu cha utekelezaji;

iii. Itoe taarifa za utekelezaji kwa kila hatua inayofikiwa kwenye mradi husika ili kusaidia kujua hatua ya utekelezaji inayofikiwa kwa kila mradi husika;

iv. Ianzishe utaratibu wa kutumia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kuhakiki takwimu zote zinazoandaliwa na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa matumizi kwenye Mpango wa Maendeleo.

v. Ihakikishe inatekeleza Mpango huu kulingana na Sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA UJUMLA YA KAMATI KUHUSU MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21)

**5.1. Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuongeza bajeti ya fedha za miradi ya maendeleo hadi kufikia asilimia 40. Serikali inatarajia kutenga asilimia 40 (trilioni 11.8) ya bajeti yake ya mwaka wa fedha 2016/17 kwa matumizi ya maendeleo. Hatua hii ni muhimu kwani itaiwezesha Serikali kutekeleza azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ukuaji wa uchumi na kuondoa umasikini kwa kutumia rasilimali za Taifa.

**5.2. Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza maamuzi ya Serikali ya kuunganisha Mpango pili na MKUKUTA ili kuwianisha ajenda ya kupunguza umaskini kwenye Mipango ya Maendeleo. Kamati inaona hatua hii ni muhimu; kwanza, katika matumizi bora ya rasilimali ya Taifa kwenye vipaumbele vinavyofanana; pili, kuhakikisha kuwa mwenendo wa ukuaji wa uchumi hasa kupitia uchumi wa viwanda unachangia kuondoa hali ya umaskini wa kipato tuliyonayo sasa hasa kwa wananchi walio vijijini.

**5.3. Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kubuni vyanzo vipya na kupanua wigo wa kodi kwa kuijumuisha Sekta isiyo rasmi katika mfumo wa Kodi. Aidha, hatua madhubuti kuziba mianya ya ukwepaji kodi ni lazima zichukuliwe ili kukahikikisha ukusanyaji wa mapato ni wa uhakika. Vyanzo vingine vya mapato ambavyo Serikali inaweza kutumia vyanzo mbadala kama vile mifuko maalum ya serikali, mikopo maalum ya maendeleo, hati fungani za miundombinu na mapato yatokanayo na sekta ya madini utalii na huduma.

**5.4. Mheshimiwa Spika.** Kamati inaishauri Serikali kukamilisha zoezi la kufanyiwa Tathmini ya Uwezo wa kukopa na Kulipa (*Credit Rating)* ili kupanua wigo wa Sekta Binafsi na Serikali kukopa kutoka katika vyanzo vya fedha vya nje kwa gharama nafuu.

**5.5. Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Serikali kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa mitaji kutoka nje (FDI) pamoja na mfumo wa ubia kati ya sekta za umma na binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyoainishwa kwenye Mpango huu.

**5.6. Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kufanyia kazi changamoto zote zilizojitokeza katika Mpango wa Maendeleo uliopita ili tufikie malengo ya kiwango cha ukuaji wa uchumi wa asilimia 8 wa Pato la Taifa na kuelekea kiwango cha asilimia 10 ifikapo 2025 kama ilivyobainishwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa. Hatua hii itasaidia kufikia malengo ya nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025.

**5.7. Mheshimiwa Spika,** hakuna nchi iliyoendelea duniani ambayo hailindi viwanda vyake vya ndani. Kamati inaishauri Serikali kulinda viwanda vyake vya ndani hasa kwa viwanda ambavyo vinazalisha na kutosheleza soko la ndani na la nje kwa kutumia malighafi zinazozalishwa nchini**.** Ni vema Serikali ikaja na sera madhubuti ya kulinda viwanda vya ndani ili kuhakikisha tunajenga msingi imara wa uchumi wa viwanda na maendeleo ya rasilimali watu

**5.8. Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kuwa bado kuna vikwazo vingi vinavyozuia maendeleo ya viwanda nchini wa ushindani wa viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya nje ya nchi. Changamoto nyingine zinazoikabili sekta Binafsi nchini ni ufinyu wa mitaji ya kifedha, gharama kubwa za uzalishaji, uwepo wa miundombinu duni ya uzalishaji (nishati, maji na usafiri) na mlolongo wa taratibu au sheria zinazobadilika mara kwa mara; na uwepo wa uhusiano hafifu kati ya sekta ya viwanda na sekta nyingine za kiuchumi. Ni vema Mpango huu ukajielekeza katika kutatua vikwazo hivi pamoja na kuwa na mkakati maalumu wa kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa viwandani.

**5.9. Mheshimiwa Spika,** ili tuhakikishe kuwa kauli mbiu ya **'kujenga msingi wa uchumi wa viwanda'** inatekelezeka katika Mpango huu, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inasimamia masuala ya msingi yafutayo:-

i. Serikali ihakikishe kunakuwepo na upatikanaji wa malighafi na miundombinu kwa viwanda vilivyopo pamoja na vile vitakavyoanzishwa nchini ikiwa pamoja na kutenga maeneo mahususi (ardhi) ya viwanda kwa mikoa yote;

ii. Serikali ifufue na kukarabati vile viwanda ambavyo sasa havifanyi kazi vizuri na kufufua vile vilivyokufa vyenye uwezo wa kuzalisha kwa gharama nafuu na kuzalisha bidhaa za kiushindani na mahitaji;

iii. Katika utekelezaji wa Mpango wa Kwanza (Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2016/17) wa Utekelezaji wa Mpango wa pili wa miaka mitano Serikali kupitia Msajili wa Hazina ifanye Tathmini ya viwanda ambavyo vilibinafsishwa na havifanyi kazi kama iliyokusudiwa na vile vinavyofanya kazi chini ya malengo yaliyokusudiwa ili kuchukua hatua stahili ikiwa ni pamoja na kuvirejesha vile vilivyokiuka masharti.

iv. Serikali ihakikishe kwamba Tanzania inakuwa na kilimo cha uhakika kisichotegemea mvua tu ili kusaidia upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda vya uzalishaji;

v. Serikali irekebishe sheria, kanuni na taratibu mbalimbali zinazokinzana katika kusaidia utekelezaji wa dhana nzima ya maendeleo ya uchumi wa viwanda ili kutoa fursa kwa Sekta Binafsi inavyoshiriki kikamilifu katika Sekta ya Kilimo;

vi. Serikali iendelee kutoa elimu kwa Watanzania ili kubadili fikra kwamba viwanda ni vikubwa tu na hivyo waanze kujielekeza kwenye uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo *(home based industries)* pamoja na viwanda vikubwa.

vii. Serikali izingatie uboreshaji wa rasilimali watu katika nyanja zote za uchumi wa Viwanda. Hatua ya msingi ni kuandaa na kuboresha mitaala mbalimbali katika vyuo vya ufundi stadi na elimu ya juu ili kuwandaa watanzania kiushindani katika kada mbalimbali kwenye uchumi wa Viwanda.

**5.10. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpago huu kwa kiwango kikubwa unategemea ushiriki wa sekta binafsi katika upatikanaji wa fedha za kugharamia mpango; uwekezaji wa mitaji na uzalishaji wa viwandani; upatikanaji wa ajira na maendeleo ya rasilimali watu. Hivyo, Serikali inabidi itazingatie yatuatayo:-

i) Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ili kupunguza urasimu na gharama kwenye miradi yamaendeleo;

ii) Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kushamiri kwa kuboresha miundombinu muhimu kama vile nishati ya umeme, maji, reli, bandari, barabara na usafiri wa anga na majini, pamoja na Kuondoa mlolongo kodi na tozo zenye kero kwa sekta binafsi;

iii) Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi kuwekeza. Tangu sheria hii imeanzishwa hakuna mradi wowote uliopitia hatua zote za kisheria na ukatekelezwa kwa ubia. Kamati inashauri Serikali kukamilisha uanzishwaji wa kituoa cha PPP *(PPP Centre )* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kushughulikia miradi ya Ubia

**5.11. Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuna haja ya Serikali kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada namba 30 ya mwaka 1974 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2004; Utaratibu wa sasa wa ukopaji unaotumiwa na Serikali ni Mpango wa Ukopaji wa Muda wa Kati (Medium Term Debt Strategy (MTDS) badala ya Mpango wa Mwaka wa Ukopaji (Annual Debt Strategy) ambao umeanishwa kwenye kifungu cha 25 cha Sheria ya Dhamana na Mikopo ya Serikali.

**5.12. Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi (Climate Change) katika utekelezaji wa ujenzi wa viwanda kwa kuzingati Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabia Nchi wa Mwaka 2012 *(National Climate Change Strategy 2012*. Pia, Kamati inashauri Serikali kuhamasisha utunzaji wa misitu ili kuhakikisha mapato kupitia Mfuko wa hali ya Hewa (National Climate Fund) yanapatikana kwa kuwahamasisha wananchi kupanda miti na uvunaji endelevu wa rasilimali ya misitu. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali kubainisha chanzo kimoja cha Mapato ili kielekezwe kwenye mfuko huu wa mazingira kama ilivyofanya kwa Mfuko wa REA, Mfuko wa Barabara na Mfuko wa Reli.

**5.13. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango huu, Serikali imeanisha namna itakavyofanya tathmini kupitia vipindi vikuu vitatu yaani; kila baada ya mwaka mmoja, baada ya miaka miwili na nusu na mwisho baada ya miaka minne na nusu. kamati inakubaliana na mpangilio. Hata hivyo Kamati bado inaona kuwa ni muhimu Serikali ikafanya tathmini ndogo kila mwaka ili kutanzua matatizo yatakayokuwa yamejitokeza wakati wa utekelezaji.

**5.14. Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na utaratibu wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo chini ya Mfumo wa Matokeo Makubwa (Big Results Now-BRN). Matokeo tarajiwa yameonekana katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kimkakati (Flagship Projects) pamoja na mabadiliko ya fikra na mtizamo wa uwajibikaji miongoni mwa watumishi wa umma. Kamati inashauri Serikali kuendelea kutumia mfumo huu wa ufuatiliaji katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21).

## 5.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Mhe. Dkt. Philip Mpango, (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21).

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu mpango husika. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Hawa A. Ghasia, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat S. Kandege, Mb - M/Kiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
5. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
6. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
7. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
8. Mhe. Maria Ndila Kangonye, Mb
9. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
10. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
15. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
16. Mhe. Salma Mohamed Mwassa, Mb
17. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
18. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
19. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
20. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
21. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
22. Mhe. David Ernerst Silinde, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii imefanya kazi kwa kujituma na kwa muda mfupi na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii. Pia, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha

Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri pamoja na Sekretariati ya Idara ya Kamati ya Bajeti kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja**.**

Hawa A. Ghasia, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
20 Aprili, 2016

**NAIBU SPIKA:** Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2011/2012 HADI 2015/2016 NA MWELEKEO WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017 HADI 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5)(a), Toleo la mwaka 2016, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha maoni ya kambi kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017 mpaka mwaka 2020/2021 kama Mpango ulivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuingia kwa undani katika kauli mbiu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa …

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde samahani kidogo, hiyo taarifa imeshatolewa kwa ajili ya kudurufiwa maana hapa Mezani mimi sina, imeshatolewa na Ofisi ya Bunge?

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii taarifa tuliipeleka tangu jana, sisi hatuna shida.

**NAIBU SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuingia kwa undani katika kauli mbiu ya Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa, kuna mambo mengi ya msingi

ambayo tunahitaji kuyajadili ambayo yameshindikana kufikiwa katika awamu ya kwanza ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2020/2025 na inaonekana kuwa ni changamoto. Hoja ya msingi ni je, tunakwenda mbele bila ya kwanza kumaliza changamoto za nyuma ili tuweze kwenda mbele vile inavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hoja ya Serikali ni kwenda kulingana na miaka lakini si kuwa na dhamira ya dhati ya kuhakikisha tunafikia malengo, ni dhahiri watu wote makini hawatakubaliana na hoja hiyo. Aidha, ni ukweli kwamba Bunge linahitaji kujadili na kuishauri Serikali juu ya vyanzo vya mapato vya utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inaonesha kuwa baada ya Uhuru kulikuwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu uliojulikana kama *Three Years Plan* kuanzia mwaka 1961 – 1964 ambao ulikuwa na msisitizo wa ukuaji wa haraka wa uchumi yaani *rapid growth of the economy.* Madhumuni makubwa yalikuwa ni kuwekeza kwenye sekta za ukuaji wa viwanda ili viwe chachu ya kukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa kwa historia ya Tanzania yaani *The First Five Years Plan* ya mwaka 1964 - 1969 uliohitaji kuwa na uchumi wa viwanda na mpango huo ndio ulizalisha viwanda ambavyo Serikali ya CCM chini ya Serikali ya Mheshimiwa Mwinyi na Mheshimiwa Mkapa, walianzisha mkakati wa kuvigawa bure na kuviuza ama kuviuza kwa bei nafuu. Mpango ule ulikuwa na lengo kuu la kuhakikisha Tanzania inazalisha bidhaa zitakazoshindana na bidhaa za kutoka nje na ndipo walianzisha ile *Import Substitutional Policy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukwama kwa Mpango huo wa Kwanza wa Maendeleo kulitokana na kwanza viwanda vilitengenezwa kwa lengo la kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na kiasi kidogo sana kwa ajili ya kuuzwa soko la nje. Pili, uwekezaji kwa ajili ya viwanda kwa takribani 75% ilitarajiwa kutoka kwa wafadhili na sekta binafsi. Tatizo hilo bado linaendelea kujitokeza hadi sasa kwenye Serikali hii ya Awamu ya Tano. Hiki ni kiashiria kwamba mipango yetu tunapanga kwa kutegemea mifuko ya sekta binafsi na wafadhili, uendelevu wa aina hii hauwezi kupatikana kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano 2011/2015. Tunaposema utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano tunaangalia ni kiasi gani cha fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imepangwa katika Mpango wa kipindi husika. Takwimu za Wizara ya Fedha zinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano ya kwanza fedha ambazo zimetolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni wastani wa 26% tu. Hii maana yake ni kwamba Serikali haina nia wala haiko tayari kuwatoa Watanzania katika umaskini na pia Serikali haitembei

kwenye maneno yake na ndiyo maana wanatumia kile kinachoitwa kwa Kiingereza *deal -dull technique* kwa maana rahisi ni kupoteza muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango wa Taifa haukutekelezwa hata nusu tunakuwa na jeuri gani kuingia kwenye awamu ya pili bila kufanya tathmini ya kina iliyopelekea kushindwa kwa awamu ya kwanza. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Bunge kuwa tuwe na mipango yetu kama Taifa inayoendana na mazingira yetu yaani *originated from within Tanzania in our own context* na sio kufuata mipango yote inayoasisiwa na Benki ya Dunia ama Shirika la Fedha Duniani, nchi wahisani ama Mashirika ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uchumi, ukuaji wa pato la Taifa. Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliopita unaonesha kwamba ukuaji wa uchumi umekua kwa wastani wa 6.7%. Hata hivyo, sekta zinazotajwa kukua ni sekta ambazo kwa ujumla wake hazina uhusiano wa moja kwa moja na uzalishaji wa ajira na au kupunguza umaskini kwa wananchi wetu na ndiyo maana kasi ya umaskini wa kipato unaendelea kuongezeka zaidi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango ni kuwa pato la mwananchi limekua kutoka wastani wa shilingi 770,000/= kwa mwaka 2010 hadi kufikia wastani wa pato la shilingi 1,720,000/= kwa mwaka 2014. Hii maana yake ni kwamba kwa mwezi wastani wa pato la mwananchi wa kawaida ni shilingi 143,000/= na ukigawanya kwa siku ni sawa na kipato cha shilingi 4,970/= kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge hili na wananchi kwa ujumla kama shilingi 4,970/= kwa siku zinatosha kuhudumia familia nzima. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kujitapa na kuamini kwamba uchumi umeongezeka wakati kipato cha mwananchi wa kawaida hakitoshelezi mahitaji ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Taifa. Hali ya deni la Taifa ni ya kutisha sana na tunapoelekea kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na wenye jukumu la kusimamia Serikali ambao ni Bunge basi nchi inaweza kufilisika kama ilivyotokea kwa nchi ya Ugiriki. Jambo hili linaweza kutokea hata hapa kwetu japokuwa tuna rasilimali nyingi sana kutokana na Serikali kutokusema ukweli na kuendelea kusema kuwa bado tunakopesheka hii ni hatari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Taifa limekua na kufikia kiasi cha dola za Kimarekani milioni 19,141. Hii ni sawa na shilingi trilioni 41.5 kwa *exchange rate* ya 2,170. Deni limeongezeka mara dufu mwaka 2015 baada ya Serikali kukopa

kiasi cha dola za Kimarekani milioni 3,846 ama shilingi trilioni 8.347 kwa *exchange rate* ya 2,170.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwishoni mwa mwezi Juni, 2010 jumla ya Deni la Taifa lilifikia dola za Kimarekani bilioni 9.9 kulingana na viwango vya kubadilisha fedha katika mwezi huo wa Juni. Kiasi hicho kilikuwa sawa na shilingi trilioni 13.6. Miaka mitano baadaye deni limefikia trilioni 41.5, kama Bunge lazima tushtuke. Maswali ya kujiuliza ni:-

(i) Fedha zilizokopwa kuanzia mwaka 2010 - 2015 zimefanya miradi ipi ya maendeleo?

(ii) Mikopo ya aina hii ina riba kiasi gani?

(iii) Tumewekeza nini kama dhamana ili kupatiwa mikopo hiyo?

(iv) Mkopo mkubwa wa mwaka 2010 ambao ni sawa na 5.9% ya Deni lote la Taifa ulitumika kufanya jambo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya maswali haya yatapatikana tu kama itafanyika *special audit* ya Deni la Taifa. Mkopo huu ni hatari zaidi kama hautalipwa kwa wakati kwani riba itaongezeka mara dufu na kuifanya nchi ifilisike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum *(special audit)* ya Deni la Taifa na kuleta taarifa Bungeni ili ijadiliwe. Kutokulipa madeni ni ghali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miaka ya 1980, Tanzania ilikopa dola za Kimarekani milioni 46 kutoka Brazil ili kugharamia mradi wa ujenzi wa barabara inayounganisha Morogoro na Dodoma, deni hilo halikulipwa. Ilipofika mwaka 2010 deni lilikuwa limeongezeka kufikia dola za Kimarekani milioni 240.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mikopo ya fedha hizo zisipolipwa kwa wadai kama makubaliano yanavyosema, inawezekana kwamba baada ya muongo mmoja fedha hizo zitafikia kiasi ambacho itakuwa vigumu sana kwa Tanzania kuzilipa. Mathalani iwapo mkopo utatozwa riba ya 5% kwa mwaka zinazopaswa kulipwa kila mwezi au mkopo huo usilipwe katika kipindi cha miaka 10 kiasi hicho kitakuwa kimeongezeka kwa 65% na hivyo deni litaongezeka mara dufu katika kipindi cha miaka 15. Kutokulipa deni ni ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wetu mwingine ni iwapo Tanzania itamudu kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati. Kwa sasa

inashindwa kulipa madeni yake yote na kuendelea kukopa kibiashara kunaweza kuliingiza nchi katika hali ngumu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola kwa kipindi cha miaka mitano imekuwa ni jambo ambalo Serikali imeshindwa kulithibitisha na imeendelea kushuka. Kwani kwa kipindi cha Januari, 2015 hadi Februari, 2016 dola moja ya Kimarekani ilikuwa ni sawa na wastani wa shilingi 1,754 kwa Januari, 2015 na shilingi 2,189 kwa Februari, 2016 kwa mfuatano huo. Hii imetokea kutokana na kutokuwa na bidhaa nyingi za kuuza nje ya nchi. Aidha, inaonekana kuwa nchi iliuza mazao na bidhaa nyingi nje lakini ni kweli kwamba mauzo hayo yanafanywa na makampuni ya kigeni na fedha za mauzo zinabaki kwenye nchi yanapotoka makampuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kushuka thamani ya shilingi ni dhahiri kwamba miradi ya maendeleo tunayopanga kwa sasa inaweza kushindwa kutekelezeka kwa sababu gharama inakuwa kubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema hayo yote ni matokeo ya kuendelea kuhamasisha wawekezaji kutoka nje na kuacha kuweka mazingira wezeshi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya vipaumbele katika utekelezaji wa Mpango. Ilipendekewa katika Mpango uliopita kwamba Serikali itenge 35% ya mapato yake ya ndani ili kugharamia bajeti ya maendeleo. Kwa miaka yote mitano Serikali haijawahi kufikia kiwango hicho jambo ambalo limeacha miradi mingi kutokukamilika kutokana na kutegemea fedha za wahisani ambazo haziji kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza bayana namna Mpango utakavyogharamiwa na kuonesha bayana vyanzo thabiti vya mapato ya kugharamikia mpango huo na siyo kuweka ahadi za wahisani ambazo hazina uhakika wa 100% kama vyanzo vya mapato vya kugharamikia Mpango wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio upande wa barabara. Mpango uliopita ulikuwa umeweka lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 5,204 kwa kipindi cha miaka mitano. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka zilitakiwa zijengwe kilomita 1,040 za barabara. Taarifa ya utekelezaji wa Mpango uliopita inaonesha kwamba zimejengwa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 2,775 sawa na 53% kwa kipindi cha miaka mitano ikiwa ni pamoja na ukarabati wa barabara hizo. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka tulikuwa tunajenga kilomita 555 tu kwa kiwango cha lami. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili itatekeleza vipi ujenzi wa barabara zilizosalia katika Mpango uliopita au Mpango huu mpya utakuwa unatekeleza viporo vilivyoachwa na Mpango uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi inapenda kuwakumbusha Watanzania kwamba aliyekuwa Waziri wa Ujenzi wa wakati wa utekelezaji wa Mpango uliopita ndiye Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo aliutekeleza Mpango huo kwa 53% tu katika sekta ya barabara. Je, Waziri wa sasa wa Ujenzi atakuwa na miujiza gani kutekeleza mipango hiyo katika kipindi hiki kingine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta ya nishati, Mpango uliweka lengo la kuzalisha *megawatt* 2,780 za umeme kwa kipindi cha miaka mitano. Maana yake ni kwamba kila mwaka ilitakiwa tuzalishe *megawatt* 556 ili kufikia lengo lililowekwa na Mpango. Utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano zimeweza kuongezeka *megawatt* 496.42 tu katika uzalishaji wa umeme nchini. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka tuliongeza uzalishaji wa wastani wa *megawatt* 100 tu za umeme nchini. Kwa mwenendo huu ili kufikia lengo la kuzalisha *megawatt* 2,780 tunahitaji miaka 13 ili kuweza kufikia lengo Mpango wa miaka mitano ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni kwa nini haikutekeleza lengo la Mpango wa Maendeleo la kuzalisha *megawatt* 2,780 za umeme katika awamu ya kwanza ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya usafiri wa anga, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba hakuna jambo la maana la kiutekelezaji ambalo limefanyika kwani kwa kuweka kumbukumbu sawa, Mwalimu Nyerere aliondoka madarakani mwaka 1984 na aliacha Shirika la Ndege likiwa na ndege 11 lakini mpaka sasa katika Awamu ya Tano Tanzania haimiliki ndege hata moja ilhali shirika likiwa na wafanyakazi wengi wanaolipwa kodi za wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza bayana mikakati ya kufufua Shirika la Ndege la Taifa ili kukuza na kuimarisha soko la utalii nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya reli. Katika Mpango wa Miaka Mitano, Serikali iliweka lengo la kukarabati kilomita 2,707 za reli kwa kiwango cha *standard gauge* lakini hadi sasa imekarabati kilomita 136 tu. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka Serikali ilikarabati kilomita 27.2. Hivyo, ili kutimiza lengo la miaka mitano la kilomita 2,707 itatumia miaka 99.5. Je, kwa mahesabu hayo Serikali itaweza kujenga reli kama tunavyopitisha hapa Bungeni?

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya kilimo. Mpango uliopita ulikuwa umeweka lengo la kukuza sekta ya kilimo ili kiwe kinakua kwa 6% kwa mwaka. Hata hivyo, katika utekelezaji wa Mpango huo sekta hii ilikua kwa wastani wa 3.4% tu kwa mwaka kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa

NAKALA YA MTANDAO

Maendeleo wa Taifa. Je, kwa mwendo huu tutaondoa wananchi wa kawaida wanaotegemea kilimo katika umaskini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango umeshindwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara ambayo tangu uhuru yalikuwa ndiyo mhimili mkubwa katika kulipatia Taifa fedha za kigeni. Mazao kama korosho, mkonge, kahawa, chai na tumbaku. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi inakipeleka wapi kilimo hiki ambacho kimekuwa kikiundiwa kauli mbiu mbalimbali ambazo badala ya kukipeleka kilimo mbele imekuwa ikikirudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika upande wa elimu, Mpango wa mwaka 2011 mpaka 2015 unasema sekta ya elimu pekee ilikuwa inahitaji walimu 900,000 wenye ujuzi ikilinganishwa na walimu wa 238,000 waliopo sasa. Katika sekta ya afya hivyo hivyo, idadi ya wataalam walikuwa wanahitajika 110,000 walitakiwa waongezeke maradufu mpaka kufikia 476,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango umeweka lengo la kufikia mwaka 2015 kuwa na wanasayansi 26,000, wasanifu na wahandisi 88,000, wanasayansi wa afya 22,000, wanasayansi tabibu wa meno na mifugo 64, wataalam wa masuala ya kiuchumi 30,000, wataalam wa uhasibu na usimamizi wa fedha 63,000, walimu 320,000 na wataalam wa ngazi za mameneja 130,000. Je, tunauliza tumefikia malengo haya kama tulivyo yaweka?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa iliyotolewa mwezi Juni, 2015 inaonesha kuwa wanafunzi katika vyuo vya VETA nchini kote walikuwa 164,000 tu, wanafunzi katika vyuo vikuu nchini walikuwa 204,000 na wahitimu mwaka 2015 walikuwa takribani 30,000 tu. Mpango uliweka malengo mahsusi kwa sekta ya elimu, ikiwemo kujengwa kwa *campus* ya Mlongazila ya Chuo Kuu cha Muhimbili utekelezaji wake mpaka sasa umefikia wapi? Taasisi tano za elimu ya juu kukarabatiwa na kuwa na wafanyakazi wenye utaalam wa VETA wapatao 635,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa mipango na vipaumbele vinavyofanana. Hapo awali katika hotuba yetu nilieleza historia inaonesha kuwa kwa Watanzania Mipango hii ya Maendeleo imekuwa ikitayarishwa na malengo ni kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na uchumi wa viwanda na sasa hivi mipango hii ni kuhakikisha viwanda na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kwa kulinganisha na sekta zingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na vipaumbele vya kuanzia mwaka 1961-1964, 1964-1969, 2011-2015 na sasa Mpango mpya wa Pili 2016/2017 mpaka 2020/2021, ukiangalia yote inafanana, lakini baya zaidi ni kwamba ile ya mwanzo imeshindwa kwa kutegemea kujenga viwanda mchango mkubwa

ulitoka kwenye sekta binafsi na wahisani. Kosa hilo la kutegemea asilimia kubwa ya mitaji kutoka sekta binafsi na wahisani ndiyo limeendelea kutugharimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wahisani gani ambao watataka sisi tujenge viwanda vyetu na tuzalishe bidhaa zetu halafu tuanze kushindana nao kwa masoko yao? Hata kama watatusaidia ni dhahiri havitakuwa endelevu kama ambavyo ilitokea huko nyuma. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema Watanzania wanao uwezo wa kutoa mitaji ya uwekezaji mkubwa na wa kati, hoja ni kuwa ni mbinu gani ya kuwafanya waiamini Serikali ambayo imeuza na kufilisi viwanda vilivyoasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kuhamasisha wananchi kujifunga mkanda na viwanda vikasimama kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uwasilishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Awamu ya Kwanza katika Bunge lako Tukufu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliieleza Serikali kuwa imekuwa na mipango na vipaumbele vingi ambavyo mwisho wake italeta changamoto katika utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano. Serikali kupitia kwa Waziri aliyekuwa anahusika na Mipango wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Stephen Wasira alibeza hoja hiyo ya Kambi Rasmi kuwa haina msingi wowote katika utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilitokana na msingi kuwa tayari kulikuwa na mpango wa kukuza na kupunguza umaskini yaani MKUKUTA. Katika hali ya kushangaza Serikali hiyo hiyo baada ya miaka mitano kumalizika mwaka 2013, ikaja na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)* ambayo ni *copy and paste* kutoka Malaysia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo huu wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano katika ukurasa wa kwanza inaonesha kuwa Serikali Mei, 2015 iliamua kuunganisha MKUKUTA na Mpango wa Maendeleo kwa sababu mipango hiyo ilikuwa inafanana na pia ilikuwa ina udhaifu katika uratibu, tathmini na namna ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango huo. Hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani wakati huo ilikuwa sahihi na ndiyo maana Serikali kimya kimya ikaichukua na kuitekeleza kwa vitendo hoja hiyo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali ya CCM kuheshimu na kutekeleza hoja mbalimbali zinazotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa vipaumbele. Mwelekeo wa Mpango kama ulivyowasilishwa unakosa vipaumbele kama ambavyo unaonekana katika nyaraka ya mwelekeo ukurasa wa tatu ambayo inasomeka kama ifuatavyo:-

*"Developing criteria and identifying areas for prioritization and sequencing of particular industries and sub-sectors."*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo huu ulikuwa na vipaumbele ili iwe rahisi kwa Waheshimiwa Wabunge kujadili na kutoa maoni yao ili kuiwezesha Serikali kuwa na vipaumbele vinavyotekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya viwanda. Mwelekeo wa Mpango unaonesha maendeleo ya viwanda nchini pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zinagusa masula yote ya maendeleo ya viwanda toka nchi ilipopata uhuru. Changamoto katika nchi yetu ni nyingi lakini za kitakwimu ndizo zinazochanganya zaidi. Taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu ya mwaka 2016 inaonesha kuwa ukuaji wa viwanda kwa 2015 ulikuwa ni asilimia sita na Mpango wa Maendeleo wa Pili wa Taifa kwa Miaka Mitano, Sura ya Nne unaonesha kuwa uzalishaji kwa viwanda kwa mwaka 2015 ulikua kwa asilimia 6.9. Hii tofauti ya asilimia 0.9 kiuchumi ni kubwa mno.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuitaka Serikali kuwa makini na takwimu zake kwani takwimu hizi ndizo zinapelekea tuonekane tunafanya vizuri kumbe kiuhalisia hali halisi ya wananchi ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa nchi yetu haitapiga hatua kimaendeleo bila ya kuwa na maendeleo ya viwanda. Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo unaonesha kuwa Sera ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji haina mikakati ya kusimamia utekelezaji wake.

Aidha, tathmini ya tija ya maeneo maalum ya uwekezaji hayawezi kukidhi malengo ya uzalishaji wake. Ikumbukwe kuwa maeneo haya ya uwekezaji yamechochea migogoro ya ardhi katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya matatizo makubwa kwenye maeneo ya uwekezaji ni fidia kwa wananchi. Kama Serikali kweli ina nia ya kuwafanya Watanzania wamiliki uchumi wao na wasiwe manamba ama ombaomba, ni kwa nini kupitia Halmashauri zao wasiwe sehemu ya umiliki ya uwekezaji unaotakiwa kufanyika kwenye maeneo husika? Jambo hili linawezekana kama Serikali ina dhamira nzuri na wananchi wake ili wawe sehemu ya kumiliki uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende mwishoni kwenye hitimisho kwa sababu ya muda, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sababu kubwa iliyosababisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa uliopita kushindwa kutekelezwa ipasavyo na hivyo kutofikia malengo yake ni kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa mamlaka kwa Bunge kujadili na kuidhinisha Mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezeka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutunga sharia ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kupitisha mpango bila kutunga sheria utakuwa hautekelezeki kama Mpango uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge lipitishe Azimio ili Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti ilete Bungeni Muswada wa Sheria ya Kusimamia Utekelezaji wa Mpango huo mpya wa Taifa wa Maendeleo ambao utaidhinishwa na Bunge hili, kwani jukumu la kutunga sheria kwa mujibu wa Katiba ni jukumu la Bunge na siyo la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, maneno yote ambayo nimeruka yaingie kama yalivyo katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KWANZA WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2011/2012 HADI 2015/2016 NA MWELEKEO WA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017 HADI 2020/2021 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A: UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 94(5) (a) toleo la mwaka 2016, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu mpango wa pili wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17 hadi 2020/21. Kama ulivyowasilishwa na Mhe Waziri, Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuingia katika kwa undani katika kaulimbiu ya Mpango wa pili wa Maendeleo ya Taifa "Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development", kuna mambo mengi ya msingi ambayo yameshindika kufikiwa katika awamu ya kwanza ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025. Na inaonekana kuwa ni changamoto, Hoja ya msingi ni je tunakwendaje mbele bila ya kwanza kumaliza changamoto za nyuma ili tuweze kwenda mbele?

**Mheshimiwa Spika**, kama hoja ya Serikali ni kwenda kulingana na miaka lakini si kuwa na dhamira ya dhati ya kuhakikisha tunafikia malengo, ni dhahiri watu wote makini hawatakubaliana na hoja hiyo. Aidha ni ukweli kwamba Bunge linahitaji kujadili na kushauri kuhusu vyanzo vya mapato vya utekelezaji wa Mpango ni jambo la muhimu sana ili kukidhi matakwa ya kikatiba.

**Mheshimiwa Spika,** historia inaonesha kuwa baada ya uhuru kulikuwa na mpango wa maendeleo wa miaka mitatu uliojulikana kama (three year plan – TYP 1961 hadi 1964 ambao ulikuwa na msisitizo wa ukuaji wa haraka wa uchumi (rapid growth of the economy). Madhumuni makubwa yalikuwa ni kuwekeza kwenye sekta za ukuaji wa viwanda ili viwe chachu ya kukuza uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, mpango wa kwanza wa miaka mitano wa maendeleo wa Taifa kwa historia ya Tanzania, the first five year plan 1964-1969 uliohitaji kuwa na uchumi wa viwanda na mpango huo ndio ulizalisha viwanda ambavyo Serikali ya CCM chini ya Mwinyi na Mkapa walianzisha mkakati wa kuvigawa bure au kuviuza kwa bei nafuu. Mpango ule ulikuwa na lengo kuu la kuhakikisha Tanzania inazalisha bidhaa zitakazoshindana na bidhaa za kutoka nje, na ndipo walianzisha sera ya ***"import substitution policy".***

**Mheshimiwa Spika**, kukwama kwa mpango huo wa kwanza wa maendeleo kulitokana na; kwanza viwanda vilitengezwa kwa lengo la kuzalisha bidhaa kwa ajili ya soko la ndani na kiasi kidogo sana kwa ajili ya kuuzwa soko la nje, pili uwekezaji kwa ajili ya viwanda kwa takriban asilimia 75 ilitarajiwa kutoka kwa wafadhili na sekta binafsi[1]. Tatizo hilo bado linaendelea kujitokeza hadi sasa kwenye Serikali ya awamu ya tano, hiki ni kiashiria kwamba mipango yetu tunapanga kwa kutegemea mifuko ya sekta binafsi na wafadhili. Uendelevu wa aina hii (sustainability) hauwezi kupatikana kwa mtindo huo.

**B: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MIAKA 5 (2011-2015)**

**Mheshimiwa Spika**, tunaposema utekelezaji wa mpango wa miaka mitano, tunaangalia ni kiasi gani cha fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo kama ilivyokuwa imepangwa katika mpango wa kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu za wizara ya fedha zinaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka mitano fedha ambazo zimetolewa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni wastani wa asilimia 26 tu. Hii maana yake ni kwamba Serikali aina nia wala haiko tayari kuwatoa watanzania katika umasikini, na pia Serikali haitembei kwenye maneno yake ndio maana wanatumia kile kinachoitwa kwa kiingereza kama ***"deal dull technique"*** kwa maana rahisi ni kupoteza muda.

**Mheshimiwa Spika**, kama utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango wa Taifa haukutekelezwa hata nusu, tunakuwa na ujeuri gani wa kuingia kwenye awamu ya pili bila ya kufanya tathmini ya kina iliyopelekea kushindwa kwa awamu ya kwanza?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa tuwe na mipango yetu kama taifa inayoendana na mazingira yetu (originated from within Tanzania in our context) na sio kufuata mipango yote inayoasisiwa na Bank ya Dunia, shirika la fedha duniani, nchi wahisani au mashirika ya kimataifa.

**a. HALI YA UCHUMI**

**i. Ukuaji wa pato la Taifa**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano uliopita (2011 -2015) unaonyesha kwamba ukuaji wa uchumi umekuwa kwa kwa wastani wa asilimia 6.7. Hata hivyo, **Mheshimiwa Spika,** Sekta zinazotajwa kukuwa ni sekta ambazo kwa ujumla wake hazina mahusiano ya moja kwa moja na uzalishaji wa ajira na au kupunguza umaskini kwa wananchi wetu na ndio maana kasi ya umasikini wa kipato unaendelea kuongezeka zaidi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa Mpango ni kuwa pato la mwananchi limekua kutoka wastani wa shilingi **770,464.3** kwa mwaka kutoka 2010 hadi kufikia wastani wa shilingi **1,724,415.6** mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** Hii maana yake ni kwamba, kwa mwezi wastani wa mapato ya mwananchi ni shilingi **143,701.25** na ukiyagawa kwa siku ni sawa na kipato cha shilingi **4,970.04** kwa siku!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulithibitishia Bunge hili na wananchi kwa jumla kama shilingi **4,970.04** kwa siku zinatosha kuhudumia familia nzima. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kujitapa kwa kwamba uchumi umeongezeka wakati kipato cha mwananchi wa kwaida hakitoshelezi mahitaji na ugumu wa maisha unaendelea kuongezeka.

**ii. Deni la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya Deni la Taifa ni ya kutisha sana na tunakoelekea kama hatua madhubuti hazitachukuliwa na wenye jukumu la kuisimamia serikali ambao ni Bunge basi nchi inaweza kufilisika kama ilivyotokea kwa nchi ya Ugiriki. Jambo hilo linaweza kutokea hata kwetu japokuwa tunazo rasilimali nyingi sana, kutokana na Serikali kutokusema ukweli na kuendelea kusema kuwa bado tunakopesheka. Hii ni hatari sana.

**Mheshimiwa Spika,** deni la taifa limekuwa na kufikia kiasi cha Dola za Marekani **19,141.3 milioni** ......hii ni sawa na shilingi **41,536.6 Trilioni** (exchange rate ya 1 usd =sh. 2,170).

**Mheshimiwa Spika,** deni hili limeongezeka mara dufu mwaka 2015 baada ya serikali kukopa kiasi cha Dola za Kimarekani **3,846.7** Milioni au shilingi **8.347 trilioni** kwa (exchange rate ya 1 usd =sh. 2,170).

**Mheshimiwa Spika,** mwishoni mwa mwezi Juni 2010 jumla ya deni la Tanzania lilifikia dola za Marekani **bilioni 9.9** kulingana na viwango vya kubadilisha fedha katika mwezi huo wa Juni, kiasi hicho kilikuwa sawa na shilingi **Trilioni 13.6.** Miaka mitano baadaye deni limefikia **trilioni 41.5** lazima kama Bunge tushituke!

**Maswali ya kujiuliza;**

i. Fedha zilizokopwa kuanzia mwaka 2010 mpaka 2015 zilifanya miradi ipi ya Maendeleo?

ii. Mikopo hii ina riba kiasi gani?

iii. Tumeweka nini kama dhamana ili kupatiwa mikopo hii au ile minong'ono mitaani kuwa Vitalu vya Gesi ndio dhamana ni sahihi?

iv. Mkopo mkubwa wa mwaka 2010 ambao ni sawa na asilimia 5.9 ya Deni lote ulitumika kufanyia jambo gani? Fedha hizi zimetumika kugharamia miradi gani au ndio EPA ya uchaguzi Mkuu wa 2015? Maana kila utawala unapokuwa unaondoka na kuingia utawala mpya tangu mfumo wa vyama vingi hapa nchini pamekuwa na utaratibu wa **'EPA'** za uchaguzi Mkuu. ...

- Mwaka 1995 tulikuwa na EPA ya IPTL (Mwinyi to Mkapa)

- Mwaka 2005 ilikuwa EPA ya BOT (Mkapa to Kikwete)
- Mwaka 2015 EPA ya Deni la Taifa ?(Kikwete to Magufuli)

**Mheshimiwa Spika,** Majibu ya maswali haya yatapatikana tu kama itafanyika 'Special Audit' ya Deni la Taifa. Mkopo huu ni hatari zaidi kama hautalipwa kwa wakati kwani riba itaongezeka mara dufu na kuifanya nchi ifilisike. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Srikali kufanya ukaguzi maalum "Special Audit" ya Deni la Taifa na kuleta taarifa ya ukaguzi huo bungeni kwa ajili ya kujadiliwa.

**Kutolipa madeni unayodaiwa ni ghali!**

**Mheshimiwa Spika**, Katika miaka ya 1980 Tanzania ilikopa dola za marekani milioni 49 kutoka Brazili ili kugharimia mradi wa ujenzi wa barabara inayounganisha Morogoro na Dodoma. Deni hilo halikulipwa. Ilipofika mwaka 2010, deni lilikuwa limeongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 240. Bahati njema kwa Tanzania ni kwamba baada ya mazungumzo ya muda mrefu, viongozi wa Brazili walikubali kulifuta deni hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Endapo Mikopo ya fedha hizo zisilipwe kwa wadai kama makubaliano yanavyosema, inawezekena kwamba baada ya muongo mmoja fedha hizo zitafikia kiasi ambacho itakuwa vigumu sana kwa Tanzania kuzilipa. Mathalan, iwapo mkopo utatozwa riba ya asilimia 5 kwa mwaka, zinazopaswa kulipwa kila mwezi na mkopo huo usilipwe, katika kipindi cha miaka 10 kiasi hicho kitakuwa kimeongezeka kwa asilimia 65% na deni litaongezeka maradufu katika kipindi cha miaka 15. Kutolipa deni unalodaiwa ni ghali.

**Mheshimiwa Spika,** Jinsi muda mrefu unavyopita bila kutimiza wajibu wa malipo ndivyo riba inavyozidi kukua. Deni ambalo Serikali ya Tanzania ilikuwa inadaiwa na Brazili ni mfano dhahiri unaoonesha jinsi hali inavyoweza kuwa mbaya. Hatari hii inajitokeza zaidi katika mikopo ya kigeni inayotolewa kwa masharti ya kibiashara ambayo kwa kawaida haina muda wa unafuu (grace period) wa kufanya malipo na hutoza viwango vikubwa vya riba.

**Mheshimiwa Spika,** Wasiwasi mwingine ni iwapo Tanzania itamudu kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati. Kwa sasa inashindwa kulipia madeni yake yote, na kuendelea kukopa kibiashara kunaweza kuiingiza nchi katika hali ngumu zaidi.

**iii. Kushuka kwa thamani ya shilingi (devaluation)**

**Mheshimiwa Spika,** kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola kwa kipindi cha miaka mitano imekuwa ni jambo ambalo Serikali imeshindwa kulidhibiti na imeendelea kushuka, kwani kwa kipindi cha Januari 2015 hadi februari 2016 dola moja ya kimarekani ilikuwa ni sawa na wastani wa shilingi 1,754.7 na 2,189.1 kwa mfuatano huo. Hili limetokea kutokana na kutokuwa na bidhaa nyingi za kuuza nje ya nchi. Aidha, inaonekana kuwa nchi iliuza mazao na bidhaa nyingi nje lakini ukweli ni kwamba mauzo hayo yanafanywa na makampuni ya kigeni na fedha za mauzo zinabaki kwenye nchi yanapotoka makampuni hayo.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kushuka kwa thamani ya shilingi ni dhahiri miradi ya mendeleo ya maendeleo tunayoipanga sasa inaweza kushindwa kutekelezeka.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inasema hiyo ni matokeo ya kuendelea kuhamasisha wawekezaji toka nje na kuacha kuweka mazingira wezeshi kwa watanzania.

**b. Mapitio ya vipaumbele katika utekelezaji wa mpango**

**Mheshimiwa Spika**, Ilipendekezwa katika Mpango uliopita kwamba Serikali itenge asilimia 35 ya Mapato yake ya ndani ili kugharamia bajeti ya Maendeleo, lakini kwa miaka yote mitano Serikali haijawahi kufikia kiwango hicho jambo ambalo limeacha miradi mingi kutokamilika kutokana na kutegemea fedha za wahisani ambazo haziji kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza bayana namna Mpago utakavyogharamiwa na kuonyesha bayana vyanzo thabiti vya mapato ya kugharamia Mpango na sio kuweka ahadi za wahisani ambazo hazina uhakika wa asilimia 100 kama vyanzo vya mapato ya kugharamia Mpango.

**i. Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango uliopita ulikuwa umeweka lengo la kujenga barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa **Kilomita 5,204** kwa kipindi cha miaka 5. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka zilitakiwa zijengwe Kilomita 1,040.8 za barabara.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya utekeleza wa Mpango uliopita inaonyesha kwamba zimejengwa barabara za Lami zenye urefu wa Kilomita 2,775 sawa na asilimia 53 kwa kipindi cha miaka 5 ikiwa ni pamoja na ukarabati wa wa barabara hizo.

**Mheshimiwa Spika,** hii maana yake ni kwamba kila mwaka tulijenga na kukarabati Kilomita 555 tu kwa kiwango cha Lami. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili itatekeleza vipi ujezi wa barabara zilisoalia katika Mpango uliopita. Au Mpango huu mpya utakuwa unatekeleza viporo vilivyoachwa na mpango uliopita?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuwakumbusha watanzania kwamba aliyekuwa waziri wa ujenzi wakati wa utekelezaji wa Mpango uliopita, ndiye Rais wa sasa wa Jamhuri ya Muugano wa Tanzania ambapo aliutekeleza Mpango kwa asilimia 53 tu katika sekta ya barabara. Je, Waziri wa sasa wa ujenzi atakuwa na miujiza gani kuutekeleza mpango mpya?

**ii. Nishati**

**Mheshiwa Spika,** Katika sekta ya Nishati, Mpango uliweka lengo la kuzalisha 2,780 MW za Umeme kwa kipindi cha miaka 5. Maana yake ni kwamba kila mwaka ilitakiwa kuzalisha 556 MW ili kufikia lengo lililowekwa na Mpango.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji- kwa kipindi cha miaka 5 zimeweza kuongezeka 496.24 MW katika uzalishaji wa umeme nchini. Hii maana yake ni kwamba kila mwaka tuliongeza uzalishaji wastani wa 100 MW za umeme nchini. Kwa mwenendo huu ili kufikia lengo la kuzalisha 2,780 MW tunahitaji miaka 13 ili kuweza kufikia lengo la Mpango wa miaka 5 ya awamu ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa maelezo mbele ya Bunge hili ni kwanini haikutekeleza lengo la Mpango wa Maendeleo la kuzalisha 2,780 MW za umeme?

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kwamba aliyekuwa waziri wa Nishati katika Serikali iliyopita, ambaye alikuwa akitekeleza mpango uliopita, ndiye waziri wa sasa wa Nishati. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Budnge hili, Waziri wa Nishati wa Sasa atakuwa na muujiza gani wenye nguvu za kumwezesha kuutekeleza Mpango huu ikiwa alishindwa kuutekeleza Mpango uliopita?

**iii Usafiri wa anga**

**Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya ufari wa Anga**,** hakuna jambo la maana la kiutekelezaji ambalo limefanyika kwani kwa kuweka kumbukumbu sawa ni kwamba, Mwalimu Nyerere aliondoka mwaka 1984 aliacha shirika la ndege likiwa na Ndege 11, lakini kwa sasa linamiliki ndege zero. Ilhali likiwa na wafanyakazi wengi wanaolipwa kodi za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Hakuna mkakati wowote wa kuhakikisha kuwa watalii hao wataendelea kuja Tanzania miaka ya huko mbeleni. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza bayana mikakati ya kufufua shirika la ndege la taifa ili kukuza na kuimarisha soko la utalii hapa nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina imaani kwamba kama taifa hatuwezi kuimarisha soko la utalii bila kuwa na shirika letu la ndege ***'National Carrier'.***

**iv. Reli**

**Mheshimiwa Spika,** mpango wa miaka mitano, Serikali iliweka lengo la kukarabati kilomita 2707 za reli kwa kiwango cha standard gauge, lakini hadi sasa imekarabati kilomita 136 tu. Maana yake ni kwamba kila mwaka serikali serikali inakarabati kilomita 27.2, hivyo ili kutimiza lengo la miaka mitano ya kilomita 2707 itatumia miaka 99.5. Je, kwa mahesabu haya tutaondoka katika hali hii ya kibiashara tuliyo nayo?

**v. Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango uliopita ulikuwa umeweka lengo la kukuza sekta ya kilimo ili iwe inakuwa kwa asilimia 6 kwa mwaka. Hata hivyo katika utekelezaji wa Mpango huo, Sekta hii ilikua kwa wastani wa asilimia 3.4 tu kwa mwaka kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mpango wa Taifa wa maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo cha umwagiliaji kwa kipindi cha utekelezaji wa mpango inaelezwa kuwa kiliongezeka kutoka Hekta **345,690** kufikia hekta **461,326** na hakikuweza kufikia lengo la hekta **1,000,000**. Aidha, kwa mwendo huu wa kukuza sekta ya umwagiliaji kukua kwa hekta **23,127.2** kwa mwaka , maana yake ni kuwa ili kufikia hekta milioni 1 tutahitaji miaka **43.2** ili tuweze kufikia lengo hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo ambacho kilitegemewa kuchangia asilimia 12.9 kwenye Pato la Taifa kiliishia kuchangia asilimia 7 tu. Aidha, ilitarajiwa kilimo kukuwa kwa wastani wa asilimia 6 kila mwaka hadi 2015. Kuongezeka kwa uongezaji thamani wa bidhaa za mazao ya kilimo kutoka asilimia 30 mwaka 2011/12 hadi asilimia 50 mwaka 2015/16. Na mwisho kuongezeka kwa mapato ya fedha za Kigeni yatokanayo na mazao ya kilimo kutoka dola za kimarekani Millioni 700 mwaka 2011/12 hadi dola za Kimarekani Milioni 1,500 mwaka 2015/16.

**Mshimiwa Spika,** mpango ulihitaji uwekezaji katika kilimo wa jumla ya shilingi milioni 4,361,576/- kwa kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango wa maendeleo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe tathmini ya malengo hayo yaliyowekwa kwenye sekta hiyo ya Kilimo ni kwa kiwango gani yametekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango umeshindwa kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara ambayo tangu uhuru yalikuwa ndio mhimili mkubwa katika kulipatia taifa fedha za kigeni, mazao kama Korosho, Mkonge, Kahawa,Pamba ,Chai na Tumbaku.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi inakipeleka wapi kilimo cha nchi hii ambacho imekuwa ikikiundia kauli mbiu mbalimbali ambazo badala ya kukipeleka kiliko mbele zinakipeleka nyuma.

**vi. Elimu**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa 2011/2012 hadi 2015/2016 unasema " .... Sekta ya Elimu pekee inahitaji walimu 900,000 wenye ujuzi ikilinganishwa na Walimu 238,000 waliopo sasa (2011). Katika Sekta ya Afya, idadi ya wataalam 110,000 waliopo sasa italazimika kuongezeka mara nne kufikia wataalam 476,000.... "(uk 35 ).

**Mheshimiwa Spika**, Mpango unaweka malengo " ... Tanzania inalenga kwamba kufikia Mwaka 2015 kuwa na wanasayansi 26,000; wasanifu na wahandisi 88,000; wanasayansi wa afya 22,000; na wanasayansi tabibu wa meno na mifugo 64,000; wataalam wa masuala ya kiuchumi 30,000; wataalam wa uhasibu na usimamizi wa fedha 63,000; walimu 320,000 na wataalam wa ngazi za umeneja130,000. Ili kufikia Malengo haya ya wataalam ifikapo Mwaka 2015/16, italazimu kuanzia Mwaka 2011 kiasi cha wanavyuo 80,000 wawe wanahitimu kila mwaka kutoka taasisi za Elimu ya Juu.
Wafanyakazi wa 635,000 wenye ujuzi wa ngazi ya VETA watahitajika ifikapo mwaka 2015". (uk. 36)

**Mheshimiwa Spika**, Tujiulize, tumefikia malengo haya?

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa iliyotolewa mwezi Juni, 2015 inaonyesha kuwa; Wanafunzi katika Vyuo vyote vya VETA nchini kote walikuwa 164,077 tu. Wanafunzi katika Vyuo vikuu vyote nchini walikuwa 204,175 na wahitimu Mwaka 2015 walikuwa takribani 30,000 tu. Mpango uliweka malengo mahususi Kwa sekta ya Elimu, ikiwemo:

1. Kujengwa Kwa Kampasi ya Mloganzila ya Chuo Kikuu cha Muhimbili. Utekelezaji wake umefikia wapi?

2. Taasisi 5 za Elimu ya Juu kukarabatiwa na kuwa na wafanyakazi wenye utaalamu wa VETA wapatao 635,000

**Utekekezaji-** Watu wenye ujuzi wa VETA wapo 200,000 tu. Taarifa za ukarabati wa taasisi za Elimu ya Juu haijulikani.

## c. UWEPO WA MIPANGO NA VIPAUMBELE VINAVYOFANANA

**Mheshimiwa Spika,** hapo awali katika hotuba hii nilieleza kuwa historia inaonesha kuwa Kwa Tanzania mipango hii ya maendeleo imekuwa ikitayarishwa na malengo ni kuhakikisha nchi inakuwa na uchumi wa viwanda na sasa hivi mipango hii ni kuhakikisha viwanda viwe na mchango mkubwa kwenye pato la Taifa kwa kulinganisha na sekta zingine za uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika**, mipango na vipaumbele vya kuanzia TYP- 1961-1964, FFYP- 1964-1969, FYP I- 2011/2012-2015/2016 na Sasa FYP II-2016/2017 -2020/2021

ukiangalia yote yanafana lakini baya zaidi ni kwamba ile ya mwanzo imeshindwa kwa kutegemea kujenga viwanda mchango mkubwa ukitoka sekta binafsi na wahisani na kosa hilo hilo la kutegemea asilimia kubwa ya mitaji kutoka sekta binasfi na kwa wahisani.

**Mheshimiwa Spika,** Ni wahisani gani ambao watataka sisi tujenge viwanda vyetu na tuzalishe bidhaa zetu alafu tuanze kushindana nao kwenye masoko? Hata kama watatusaidia ni dhahiri havitakuwa endelevu kama ambavyo ilitokea huko nyuma.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasema watanzania wanao uwezo mkubwa wa kutoa mitaji ya uwekezaji mkubwa na wa kati, hoja kubwa ni mbinu gani ya kuwafanya waiamini serikali ambayo imeuza na kifilisi viwanda alivyoanzisha na Mwalimu Nyarere kwa kuhamasisha wananchi kujifunga mikanda na viwanda vikasimama na kufanyakazi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uwasilishaji wa Mpango wa maendeleo wa awamu ya kwanza 2011/2012- 2015/2016 katika Bunge lako tukufu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilieleza kuwa serikali imekuwa na mipango mingi na vipaumbele vingi ambavyo mwisho wake italeta changamoto katika utekelezaji wa mpango wa miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia kwa Waziri aliyekuwa anahusika na mipango ya serikali Mhe. Stephen Wassira alibeza hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa ilikuwa haina msingi wowote katika utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano wa awamu ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika**, Hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilitokana na msingi kuwa tayari kulikuwa na mpango wa kukuza uchumi na kupunguza umasikini (MKUKUTA). Katika hali ya kushangaza baadaye serikali hiyo hiyo kabla ya miaka mitano kumalizika mwaka 3013 ikaja na mpango wa matokeo makubwa sasa (**BRN- Copy and Paste toka Malaysia).**

**Mheshimiwa Spika**, Mwelekeo (Framework) huu wa mpango wa maendeleo ya miaka mitano 2016/17-2020/21katika ukurasa wa kwanza inaonesha kuwa serikali mwezi Mei mwaka 2015 iliamua kuunganisha MKUKUTA na mpango wa maendeleo kwa sababu mipango hiyo ilikuwa inafanana na pia ilikuwa na udhaifu katika uratibu, tathmini na namna ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani wakati huo ilikuwa sahihi na ndiyo maana serikali kimya kimya ikaichukua na kuitekeleza kwa vitendo hoja hiyo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni inatoa rai kwa serikali hii ya CCM kuheshimu na kutekeleza hoja mbalimbali zinatolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

## d. UKOSEFU WA VIPAUMBELE

**Mheshimiwa Spika**, mwelekeo wa mpango kama ulivyowasilishwa unakosa vipaumbele kama ambavyo inaonekana katika nyaraka ya mwelekeo ukurasa wa tatu ambayo inasomeka kama ifuatavyo***"Developing criteria an identifying areas for prioritization and sequencing of particular industries and subsectors".***

**Mheshimiwa Spika**, mwelekeo huu ulitakiwa uwe na vipaumbele ili iwe rahisi kwa washeshimiwa wabunge kujadili na kutoa maoni yao ili kuiwezesha serikali kuwa na vipaumbele vinavyotekelezeka.

## e. MAENDELEO YA VIWANDA

**Mheshimiwa Spika**, Mwelekeo wa Mpango umeonesha maendeleo ya viwanda nchini pamoja na changamoto mbalimbali ambazo zinagusa masuala yote ya maendeleo ya Viwanda toka nchi ilipopata uhuru.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto katika nchi yetu ni nyingi lakini za kitakwimu ndizo zinachanganya zaidi, taarifa ya liyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2016 inaonesha kuwa ukuaji wa viwanda kwa mwaka 2015 ulikuwa ni asilimia 6 na Mpango wa Maendeleo wa pili ya wamendeleo wa miaka mitano, sura ya nne unaonesha kuwa uzalishaji viwandani kwa mwaka 2015 ulikuwa ni asilimia 6.9. Hii tofauti ya asilimia 0.9 kiuchumi ni kubwa mno.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuitaka Serikali kuwa makini na takwimu kwani takwimu hizi hizi ndizo zinapelekea tuonekane tunafanya vizuri kumbe halihalisi ya wananchi ni mbaya sana.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa nchi yetu haitapiga hatua kimaendeleo bila kuwa na maendeleo ya viwanda. Mwelekeo wa mpango wa maendeleo umeonesha kuwa sera ya maeneo maalumu ya uwekezaji (SEZ/EPZ) hayana mikakati ya kusimamia utekelezaji wake (Ukurasa 19 wa Mwelekeo wa Mpango).

Aidha, tathmini ya tija ya maeneo maalumu ya uwekezaji hayawezi kukidhi malengo ya uanzishaji wake, ikumbukwe kuwa maeneo haya ya uwekezaji yamechochea migogoro ya ardhi katika maeneo mengi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya matatizo makubwa kwenye SEZ ni fidia kwa wananchi, lakini kama kweli Serikali ina nia ya kuwafanya watanzania wamiliki

uchumi wao na wasiwe manamba na ombaomba, ni kwanini wananchi kupitia halmashauri zao wasiwe sehemu ya umiliki wa uwekezaji unaotakiwa kufanyika kwenye maeneo husika? Jambo hili linawezekana kama kweli Serikali ina dhamira nzuri na wananchi wake ili wawe sehemu ya umiliki wa uchumi wa nchi yao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuangalia awamu ya pili ya mpango wa taifa wa miaka mitano ambao kimsingi dhana yake kubwa ni kuwa na uchumi wa viwanda, lakini hii kitu ***Kurasini Trade and Logistics Centre*** ambayo dhana yake ni kuwa na kituo kitakacho warahisishia wafanyabiashara badala ya kwenda China basi bidhaa za kichina zitakuwa zinapatikana hapa kurasini. Na pia kwa wafanyabiashara wa mataifa yanayotuzunguka badala ya kwenda China basi watapata huduma kurasini. Hii maana yake ni kuwa nchi ya **uchuuzi kabisa**. Ni kweli dhana ya kuwa na uchumi wa viwanda unawezekana? Hapa tunaua kabisa hari ya kuzalisha bidhaa zetu wenyewe na kuweza kuwauzia hao wachina.

**Mheshimiwa Spika,** Wachina wanataka waendelee kununua malighafi toka kwetu alafu watuletee bidhaa sisi tuwauzie wananachi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza kwa kufanya hivyo ni kiasi gani cha ajira kinakwenda kwenye viwanda vya Wachina?

**Mheshimiwa Spika**, kama kweli tunapanga kwa kumaanisha kweli bali ujenzi wa Kituo cha Kurasini kimantiki unapingana na dhana pana ya kuwa na uchumi utakaoendeshwa na viwanda vyetu. Yale aliyoyakataa Mwalimu Nyerere na kuanzisha ***sera ya Import substitution*** sasa ndio Tanzania itakuwa **assembly ground** kwa bidhaa za wachina.

**Mheshimiwa Spika**, Ukweli ni kuwa kelele zilikuwa wachina wanafanya biashara za umachinga sasa hicho kituo watajaa Wachina tu kwa ajili ya kazi zitakazokuwepo hapo kwani watahitaji nguvu kazi yenye ujuzi maalum na nguvu kazi ya kwetu watasema haina utaalam unaohitajika. Hoja hapo ni Je, mtawafukuza au mtawaacha waendelee kufanyakazi hizo?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuwasilisha tena marekebisho ya Sheria ya Maeneo maaalumu ya uwekezaji ili kutatua changamoto ambazo zinayakumba maeneo hayo ikijulikana kuwa na sera pekee hakutaipa nguvu ya utekelezaji kwa kuwa sera haina nguvu ya utekelezaji wa kisheria.

## f. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani sababu kubwa iliyosababisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa uliopita kushindwa kutekelezwa

ipasavyo, na hivyo kutofikia malengo yake, ni kukosekana kwa sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa ibara ya 63 (3) (c) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa mamlaka kwa bunge "kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano ***na kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo"*** *hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuupitisha mpango huo bila kuutungia sheria hautatekelezeka kama Mpango uliopita.*

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge lipitishe azimio ili Kamati ya Bunge Kudumu ya Bajeti ilete Bungeni muswada wa Sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huu mpya wa Taifa wa Maendeleo ambao utaidhinishwa na Bunge hili. Kwani jukumu la kutunga sheria kwa mujibu wa katiba ni jukumu la Bunge na sio la Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

**DAVID ERNEST SILINDE (MB)**
**NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI –**
**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**
20April, 2016

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na uchangiaji kama nilivyokuwa nimetangaza, nitasoma majina ya watu watano wa mwanzo watakaoanza kuchangia sasa hivi. Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi. Mheshimiwa Peter Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuomba saa hizi sijajiandaa nitachangia jioni, samahani.

**NAIBU SPIKA:** Katibu, naomba uchukue hilo jina. Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Joseph George Kakunda na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi…

**MBUNGE FULANI:** Mtera hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa Mpango huu ambao ametuletea, Mpango wa Pili wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2016/2017 mpaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimefurahishwa sana na Mpango huu ambao umeletwa mbele yetu. Mpango huu umeeleza bayana vipaumbele ambavyo Serikali inategemea kutekeleza katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vipaumbele hivyo ambavyo ni msingi mkubwa sana wa maendeleo ya nchi yetu mambo yako mengi lakini suala la kwanza ambalo ni la msingi sana ni kuendeleza kilimo. Suala la kilimo inabidi lipewe kipaumbele cha kutosha. Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi yetu, kilimo ndiyo kinachotoa ajira kubwa kwa wananchi wengi katika nchi yetu, zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wanategemea kilimo. Pia tunapotaka kuipeleka nchi kuwa ya viwanda tunategemea zaidi kwamba malighafi nyingi na mazao mengi yatakuwa ni yale yanayotokana na kilimo na hivyo viwanda vingi ambavyo tunavianzisha vitakuwa vile vitakavyochakata mazao yanayotokana na kilimo. Naomba tuongeze jitihada kabisa za kuhakikisha tunakiimarisha hiki kilimo, pembejeo zile zinazohitajika katika kufufua kilimo hiki ziongezeke na bajeti ya kilimo iongezeke ili kwenda kujenga nchi ya uchumi safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba kama tukikifufua kilimo, tukiimarisha viwanda vinavyotokana na mazao ya kilimo, asilimia kubwa sana ya watu wetu wataajiriwa. Nashauri Serikali ihakikishe tunajenga viwanda vitakavyochakata mazao haya ya kilimo. Viwanda hivi vitasaidia sana kutoa ajira na msukumo mkubwa katika kuchangia pato la Taifa.

Kipaumbele cha pili ambacho kinaendana na hicho cha kilimo ni kuimarisha miundombinu mbalimbali ambayo ita-*support* hicho kilimo chetu. Miundombinu ya barabara, umeme na vitu vingine vinavyoendana na hivyo vitasaidia sana kuhakikisha nchi yetu inaendelea. Pia miundombinu hiyo itatoa ajira kwa vijana wetu wengi katika nchi yetu. Kwa hiyo, lazima tuweke nguvu zaidi katika kuimarisha hiyo miundombinu ya reli na vitu vinginevyo.

Nimefarijika sana na jitihada za Serikali za kuamua kufufua Shirika letu la Ndege. Katika ulimwengu huu kila nchi ina shirika lake na Shirika la Ndege ndiyo linatoa mchango mkubwa sana katika kuendeleza nchi. Tumeona nchi mbalimbali jinsi zinavyofanya. Kwa kweli inasikitisha sana kuona shirika letu limekuwa likisuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi jitihada ambazo Serikali ya Awamu ya Tano imeamua kuzichukua katika kulifufua shirika hili lazima tuziunge mkono kwa udi

na uvumba ili kuhakikisha linakua na linatoa ajira nyingi kwa vijana wetu lakini pia tuweze kulitumia katika kuharakisha kuchochea maendeleo katika sehemu mbalimbali. Shirika letu sasa hivi lina ndege moja au mbili …

**WABUNGE FULANI:** Hamna.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hizi ndege ambazo tumepanga kuzinunua zikinunuliwa naamini zitachochea sana maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, tuongeze hizo jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuleta maendeleo ya kweli lazima huduma mbalimbali zikiwemo huduma za masuala ya fedha ziimarike. Hivi sasa mabenki mengi yamekuwa yakifanya biashara maeneo ya mijini hayakuweza kwenda vijijini. Sasa hivi Benki ya Wakulima imeanzishwa lakini bado iko Dar es Salaam. Nashauri kama ni Benki ya Wakulima ianzishwe mikoani ili wakulima wapate nafasi ya kwenda kukopa huko na tuweze kufufua kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mabenki yetu mengi yalikuwa yanafanya biashara kwa kutegemea fedha za Serikali. Kwa hiyo, naomba niunge mkono jitihada za Serikali, sasa hivi za kuhakikisha fedha zote za Serikali zinakuwa Benki Kuu ili mabenki haya yaende sasa kutafuta wateja huko vijijini na hii itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo, wakati Serikali inachukua jitihada za kubana matumizi na hivyo kuondoa fedha nyingi za Serikali kwenye mabenki maana yake sasa mabenki nayo lazima yafanye jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba riba za mikopo zinashuka. Sasa hivi riba ziko juu sana, wananchi wakikopa baada ya miaka miwili, mitatu unakuta deni ni mara mbili ya kile ambacho alikuwa amechukua hali ambayo haisaidii kuchochea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kwa kuangalia riba zile za kukopa na riba ambazo wanazitoa kuna *spread* kubwa ambayo nafikiri Serikali pamoja na mabenki yachukue hatua zinazostahili kuhakikisha kwamba yanarekebisha hiyo hali ili kusudi benki hizi zichochee maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mpango huu umejikita katika utoaji wa huduma za jamii hasa suala la elimu. Suala la elimu limepewa uzito mkubwa na naunga mkono kwani bila kuimarisha elimu hatuwezi kuwa nchi ya kipato cha kati. Elimu hii ndiyo itakayotuwezesha tupate watalaam wazuri, tupate watalaam wa kati wanaohitajika katika viwanda vyetu. Lazima mitaala ya elimu zetu kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu ipitiwe upya

ili iendane na mahitaji halisi ya wakati tulionao. Hilo naamini linawezekana kwa kutumia watalaam na uwezo uliopo tunaweza tukafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vyetu vinahitaji wataalam, sasa hivi vijana wengi wamekuwa wakikimbilia sana kwenda kusoma kwenye vyuo vya elimu ya juu wanakuwa ni ma-*engineer*, lakini nadhani kuna haja ya kuimarisha elimu ya mafundi wale wa kati na hasa vyuo vyetu hivi vya *VETA* na vyuo vinginevyo. Hivi ndivyo vitakavyoweza kuchukuwa vijana wengi na kuwapa ujuzi unaohitajika katika viwanda vingi. Kwa hiyo, hizi jitihada lazima ziungwe mkono kwa hali na mali ili tuhakikishe kwamba tunafika kule tunakokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kupongeza Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kwamba elimu yetu inakuwa bure kwenye shule za msingi na sekondari mpaka kidato cha kumi na mbili. Kwa kweli hili ni suala zuri sana lazima tuipongeze Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tumeanza kuitekeleza hii sera imeonyesha matumaini na matunda makubwa kwani watoto wengi wameweza kwenda shule na kuandikishwa. Sasa lazima tuhakikishe kwamba tunaunga mkono jitihada hizi na tunashirikiana na Serikali ya Awamu ya Tano ili kuhakikisha hii azma inatekelezeka. Zipo changamoto ambazo tutakabiliana nazo na ni kitu cha kawaida. Unapoamua kuanzisha kitu chochote lazima ukabiliane na changamoto ambazo naamini tutashinda na tutafika mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia suala la afya. Jitahada za Serikali ya CCM sasa hivi ambazo tumejikita nazo na tumeiweka kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi kwamba kila kijiji kuwe na zahanati na tunataka kila kata kuwe na kituo cha afya lakini vituo hivi vya afya vinahitaji pia viwe na wataalam. Jitihada ambazo wananchi wameanza kuonyesha kwa kujenga zahanati na vituo vya afya, Serikali iongeze mkakati wa kuhakikisha inawaunga mkono na pale ambapo wamekamilisha vianze kufanya kazi kama ambavyo inakusudiwa. Wananchi wamejitoa sana kuhakikisha wanajenga hivi vituo vya afya na zahanati, Serikali itekeleze wajibu wake pale ambapo tunaona kwamba panatakiwa kutekelezwa ili kusudi maendeleo yapatikane haraka kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Mpango huu ni mzuri, mpango wa kuimarisha reli ya kati, mpango wa kujenga reli kwa *standard gauge* ni wa muhimu sana kwani utatusaidia sana kuchochea maendeleo katika mikao yote. Hii ndiyo njia pekee itakayotusaidia nchi yetu kuweza kuunganishwa na hizo nchi zingine na kupunguza gharama za uendeshaji

ambazo sasa hivi zimekuwa ni kubwa sana. Sasa hivi barabara zetu zinabeba malori makubwa ambayo yanasababisha barabara zetu zisidumu kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tukiimarisha reli hii naamini itakuwa limesaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe shukurani kwako wewe kwa kunipa nafasi ili niwe mchangiaji mmojawapo asubuhi hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwenye Mpango huu ni kama ifuatavyo; Serikali yetu hii ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ni Serikali ya kupanga mipango mizuri sana. Hii ni mara ya pili nalisema hili ndani ya Bunge lako Tukufu, lakini tatizo letu kubwa liko kwenye utekelezaji wa ile mipango tunayoipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui hizi takwimu mnazokuja nazo, hizi za ku-*copy* na ku-*paste* zinaletwa kwa sababu ipi? Tunakuwa tumedhamiria nini tunapoleta takwimu ambazo hatuna uhakika nazo na wala hazitekelezeki. Hatuwezi kuwa na mipango na ikatekelezeka iwapo hatuna mikakati iliyowazi ya kuonyesha namna gani tutatekeleza mipango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano takwimu ambayo imetolewa na Mwenyekiti wa Kamati, anasema sera ya nchi yetu ilikuwa kuunganisha mikoa yetu na imekamilika na akaitaja baadhi ya mikoa na akasema ni mikoa michache tu ambayo imebaki haijaunganishwa. Hata hivyo, nashangaa Mkoa wa Lindi - Morogoro haijatajwa katika mikoa ambayo haijaunganishwa. Kwa sababu Mkoa wa Morogoro unapakana na Mkoa wa Lindi kupitia Wilaya ya Liwale lakini hakuna barabara. Mkoa wa Lindi unapakana na Ruvuma katika Wilaya ya Liwale hakuna barabara lakini takwimu hapa zinaonyesha kwamba mikoa hiyo tumeshaunganishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Sera ya Taifa inasema kila kata kuwe na kituo cha afya na kila kijiji kiwe na zahanati. Lengo hili halijafikiwa kama ambavyo Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani amesema, tunadiriki vipi kwenda na mpango wa pili wakati hii mipango yetu ya kwanza haijakamilika, tena imekamilika kwa asilimia 26 tu. Katika Jimbo langu tuna kata 20 lakini tuna kituo cha afya kimoja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hapa tunajitapa kwamba tunao uwezo wa kutekeleza mipango hii kwa kutumia rasilimali zetu ambazo nina hakika kabisa hazisimamiwi kama inavyotakiwa.

Ubadhirifu wa rasilimali zetu umekuwa ni mkubwa sana. Tunavyo viwanda, hivyo ambavyo sasa tunasema tunataka kuvifufua, Mkoa wa Lindi kulikuwepo na viwanda vya korosho vikabinafsishwa na havifanyi kazi mpaka leo lakini leo hii tunapokuja kufufua viwanda napata wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Lindi sasa hivi unazalisha ufuta na korosho lakini kama nilivyosema tuna matatizo ya barabara. Hivi ni mwekezaji gani atayekuja kuwekeza Lindi mahali ambapo hakuna barabara, mahali ambapo hatujajiandaa na miundombinu yoyote? Nitoe mfano halisi, sasa hivi barabara ya Jimboni kwangu imeshafungwa, huwa inapitika kiangazi tu lakini sisi Mkoa wa Lindi ndiyo tunaoongoza wa kuzalisha korosho na ufuta lakini hatuna kiwanda hata kimoja. Mimi siwezi kumvutia mwekezaji yeyote aje kuanzisha kiwanda Liwale wakati ambapo hatuna barabara, umeme wala miundombinu yoyote, huku ni kudanganyana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sijajua Serikali inavyokuja na hizi takwimu au maelezo ya juu juu wanakuwa wamedhamiria nini kwamba tupitishe tu ili mradi siku ziende au kweli tuko *committed* na hayo tunayoyaongea au tunayoyadhamiria? Kwa mfano, hapa tumesema malengo yamekamilika kwa asilimia tano, hivi ni kweli? Yaani mpango wa kwanza umetekelezwa kwa asilimia tano au asilimia 26 tunaingia kweli kwa kifua mbele kwa mpango wa pili, mimi sijaelewa na wala sishawishiki kuona kama tuko *serious* na jambo hili. Hivi tunawezaje kwenda na Mpango wa Pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kikao kilichopita nilisema hapa kwamba hatuko *serious.* Mpango ule wa kwanza wa kujenga reli tulitekeleza kwa asilimia 5 tu na nikawaambia hapa kwamba hii haifanywi kwa bahati mbaya ila kwa makusudi kwani kuna watu wanataka wafanye biashara za malori, nikasema hapa wakaanza kulalamika. Mipango hii tunayokwenda nayo haiwezi kwenda kama hatuko *serious.* Mimi naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama hamko *serious* na nchi hii mtuachie na watu wako tayari kutuachia lakini ninyi hamtaki kutoka. Kwa mipango hii hatuwezi kwenda. Tumekuwa wepesi sana wa kuainisha vipaumbele lakini si watekelezaji wa vipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande wa kilimo, tangu Uhuru tumekuja na sera nyingi za Kilimo Kwanza, Kilimo Uti wa Mgongo lakini hivi kweli hiki kilimo kinaweza kikaimarishwa kwa njia hii na hakuna mkakati wowote wa kuimarisha masoko. Leo hii Waziri anakuja hapa anasema kwamba anataka kushusha bei mazao ya kilimo ina maana wakulima waendelee kuteseka, hiyo ndiyo mipango ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Mtuachie nchi hii kwa

sababu mimi ninavyofahamu huwezi kuimarisha kilimo kama haujaimarisha masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu tunapata shida, nitolee mfano wa Jimboni kwangu, tunalima korosho na ufuta lakini wananchi wangu wanahangaika kila mwaka. Mwaka huu wakivuna korosho, ufuta unapanda bei, mwakani wanavuna ufuta, korosho zinapanda bei hawajui kinachoendelea.

Leo hii tunakuja hapa na Mpango kwamba tunaanzisha viwanda hatujui hivyo viwanda vilivyokuwepo awali vilienda wapi, wale walioharibu viwanda hivi wamechukuliwa hatua gani hatujui, tunakuja tunavurugana vurugana hapa tu ndani kwamba tuna mipango endelevu.

Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze, utekelezaji wa Mpango huu hizo hela anazipata wapi? Kwa sababu mipango iliyopita, Serikali ni hii hii, watu ni wale wale imetekelezwa kwa asilimia tano, leo hii mnakuja kutuambia kwamba mnaweza kutekeleza angalau asilimia 50, huo uwezo mnaupata wapi? Au ndiyo kama nilivyosema jana hapa tupo tu kwa ajili ya kuonekana kama sisi tupo Bungeni tunajadili mustakabali wa nchi yetu ili mradi siku ziishe lakini *seriousness* mimi sijaiona. *Seriousness* ya Chama cha Mapinduzi kuwahudumia watu wake sijaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaambieni Jimboni kwangu tungekuwa tumepakana na nchi mojawapo ningeshawishi lile Jimbo tuliondoe Tanzania. Hata hivyo, kwa sababu tuko katikati hatujapakana na nchi yoyote tutaendelea kubaki kisiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi nikiwa na maana halisi. Mimi kwangu hakuna barabara, Kituo cha Polisi, hospitali, maji na nikisema hakuna maji namaanisha. Liwale tumerithi Kituo cha Polisi tulichukua jengo la benki. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji anajaribu kujenga hoja yake na anaruhusiwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge letu, lakini si jambo la kizalendo kwa kiongozi kusema kwamba kama Jimbo lake lingekuwa

karibu na nchi yoyote ile ya mpakani basi angependa lihamishiwe huko kwa sababu hakuna kilichofanyika. Nadhani ni kuwakosea wananchi wa Jimbo lake waliomchagua na kumuamini kwa uzalendo mkubwa na kuja hapa akadharau kazi iliyofanyika. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka naomba usubiri taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya mambo mengi sana. Nafahamu Mheshimiwa Mbunge anatokea Jimbo lililopo kwenye Mikoa ya Kusini na kule jambo moja tu la kumbukumbu ili kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge ni kwamba zaidi ya miaka kumi iliyopita akitaka kwenda kwao huko kijijini alikuwa anachukua zaidi ya siku kumi kufika lakini Serikali ya Awamu ya Tatu ikajenga Daraja kubwa la Mkapa ambalo leo hii unakwenda mpaka Jimboni kwake kwa masaa manne. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo sio taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo *seriousness* tunayoizungumzia leo. Kwa hiyo, naomba apokee taarifa hiyo kwamba Serikali iko *serious* na inafanya kazi ya maendeleo kuiunganisha nchi yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka unapokea Taarifa hiyo?

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba ulinde muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Muda wako unalindwa, naona kuna taarifa nyingine.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pili naikataa taarifa kama ifuatavyo. Nimesema Wilaya ya Liwale haina barabara, mimi kila tarehe 15 Septemba na tarehe 15 Julai wananchi wa Liwale wanatoka kwenda Mahenge kwa miguu wanasindikizwa na askari wa wanyamapori na wanatembea muda wa siku tatu mpaka siku nne. Nimesema Liwale hakuna barabara, nimesema Liwale kama ingekuwa vita ile ya mwaka… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka, naomba ukae kuna taarifa nyingine.

**TAARIFA**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mimi nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri baada ya Taarifa yake kwa Mheshimiwa Kuchauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kigoma tulitengwa ikafikia hatua tukasema jamani tuambieni Kigoma ni Tanzania au Burundi, Serikali ikaanza ku-*act*. Kwa hiyo, ni haki yake Mheshimiwa kusema maneno hayo ili Serikali isikie ipeleke huduma hizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuwe tunafuata utaratibu, taarifa anapewa anayetoa hoja.

Sasa ukitoa taarifa juu ya taarifa nyingine kidogo inaweza ikaleta shida. Mheshimiwa Kuchauka, tafadhali endelea. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa hiyo, nakataa Taarifa yake kama ifuatavyo; nimesema na naendelea kusema Liwale sisi hatuna hospitali inayoitwa Hospitali ya Wilaya, nashukuru aliyenipa taarifa ni Naibu Waziri wa Afya atalichukua akitaka kuthibitisha. Sasa hivi katika Wilaya nzima ya Liwale tuna *Clinical Officers* watatu tu, siyo Madakatari Bingwa ni *Clinical Officers* watatu tu mahitaji ni *Clinical Officers* 40, nasema kwa takwimu. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aibu.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda uniambie unapotaka kuunganisha mikoa ina maana kwamba tutoke Lindi - Dar es Salaam - Dodoma - Iringa, twende Songea, labda kuunganisha kwa namna hiyo. Nikisema nina hali hiyo ya kusema, nawasemea wana Liwale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, narudi kwenye Mpango. Kama nilivyotangulia kusema kwamba sisi shida yetu ni uhakika wa masoko. Serikali haionyeshi mahali ambapo wananchi hawa watasaidiwa vipi kwa upande wa masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwa upande wa maliasili, sisi Liwale tuko kwenye Mbuga ya Selous lakini Liwale haina hoteli ya kitalii, barabara wala kiwanja cha ndege, hatunufaiki kwa chochote sisi kupakana na mbuga za wanyama zaidi ya kuendelea kupigwa na kunyanyaswa. Nimeshamletea Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili taarifa ya mgogoro uliopo Wilaya ya Liwale na Mbuga ya Selous. Sasa anapokuja Naibu Waziri akaniambia kwamba sina haki ya kuiondoa Liwale Tanzania sijamuelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunanufaikaje na maliasili? Sisi tunapakana na mbuga za wanyama lakini vilevile tulikuwa na uwanja wa ndege enzi zile za Mzee Kawawa, Mwenyezi Mungu amrehemu, tangu Mzee Kawawa amekufa na Liwale imekufa, ule uwanja wa ndege haupo tena pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo hii Serikali hii kwenye Mpango wake huu, labda Waziri atakapokuja kuniambia kama ana mpango wowote, kama kuna mpango wa kuufufua uwanja wa ndege Liwale, kama kuna utaratibu wowote ule wa maliasili, kama wanajenga hoteli au kama wanatutengenezea barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetembea vijiji vyote vya Jimbo langu sijakuta hata choo kilichochangiwa na Selous, sijakiona! Sasa unategemea wananchi wa Liwale na Lindi wa-*support* mpango huu kwa kipaumbele gani ambacho wamepewa au kwa sehemu gani ambayo wamekumbukwa? Labda Waziri atakapokuja kwenye kujumuisha atakuja kunieleza kwamba Liwale au Mkoa wa Lindi kwa ujumla ameuweka katika mpango huu katika maeneo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Liwale bado watumishi hawataki kukaa kule, mawasiliano hakuna siyo ya barabara wala simu. Ndiyo maana nikasema hapa nahitaji *Clinical Officers* 40, siyo kwamba hawapangwi, wanapangwa lakini hawakai kwa sababu mazingira ya Liwale siyo rafiki. Jamani Chama cha Mapinduzi mtuachie hii nchi. Tuachieni hata miaka mitano tu muone nchi inaendeshwaje. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo tu ya kusema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Omary Massare atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kakunda halafu Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipia nafasi hii kwa asubuhi ya leo na mimi niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimimwa Naibu Spika, nianze tu kwa kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri iliyofanya katika masuala mazima ya huduma za jamii lakini suala la miundombinu, kilimo na mengine mengi likiwemo kubwa la umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango huu ambao umewasilishwa tulipokuwa Dar es Salaam na leo Mheshimiwa Waziri hapa, maeneo mengi yameguswa lakini barabara nyingi zilishatengenezwa na sasa ni wakati mzuri

katika miaka mitano hii kuangalia maeneo yale machache ambayo bado Serikali haijayafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kukumbusha kwamba kuna barabara ambazo zimekuwa zikisemewa sana na viongozi wetu wakuu, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, lakini Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na hadi sasa Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli wa hapa kazi na juhudi zake zimeonekana katika barabara ya kutoka Mkiwa, Rungwa hadi Makongorosi. Serikali katika Mpango wa mwaka huu imeonyesha kwamba inajenga barabara kutoka Chunya hadi Makongolosi lakini niombe sana katika mipango endelevu barabara hii katika kipindi hiki cha miaka mitano ionwe na ikiwezekana iishe. wananchi wa Majimbo yanayopitiwa na hii barabara likiwemo la Mheshimiwa Kakunda na Jimbo langu mimi lakini ni barabara kubwa inayounganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya kupitia Mkoa wa Tabora. Kumekuwa na ahadi nyingi, sasa si vibaya safari hii basi na sisi tukaonwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ahadi nyingine ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alikuwa afungue barabara ya kutoka Mkoa wa Singida inapita katika Wilaya ya Chemba inakwenda Kiteto na hadi Handeni. Barabara hii ina fursa nyingi za wajasiriamali, maeneo ya wakulima wakubwa wa nchi hii wanaolisha Mikoa ya Dar es Salaam na hata Tanga wapo maeneo yale lakini sisi wakulima wa Mkoa wa Singida barabara ile kama itafunguliwa itakuwa na tija sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo, nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, kijana wetu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alipiga kazi sana wakati wa uchaguzi, alitembea nchi nzima na sasa juhudi zake zinaonekana. Nataka nimkumbushe tu kitu kidogo kwamba wafugaji wa maeneo yetu hususan katika Jimbo la Manyoni Magharibi wana shida kidogo ya maeneo ya malisho. Jimbo langu sehemu kubwa ni Hifadhi ya *Rungwa Muhesi Game Reserve* ambayo ina eneo kubwa. Kuna wafugaji wanaopakana na maeneo yale na kwa sababu maeneo yale sasa hivi wafugaji wanaotoka Mkoa wa Shinyanga wamekuwa rafiki zetu na wamekuwa wengi pale na mifugo imekuwa mingi, si vibaya tukaliona hili katika mipango yetu ijayo tukawapa fursa nao malisho kidogo yakawa yamekaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na timu yake, Mheshimiwa Kalemani yuko hapa, amekuwa msikivu sana. Amenipa maeneo mengi, anafanya jitihada za kunipatia za umeme lakini naomba utekelezaji uwe wa haraka. Wataalam wamefika ila sijaona vizuri kwenye randama ya bajeti ya Mpango huu kama wamelizingatia hilo lakini naamini ananisikia na atalifanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizopo katika Jimbo langu ni pamoja na shida kubwa ya maji. Sisi mikoa ya katikati hatuna mito lazima tuchimbe maji. Katika Mji Mdogo wa Itigi kuna visima vikubwa sana vya maji na vizuri vimechimbwa na Serikali katika bajeti hii inayoisha. Niombe katika Mpango ujao wa Miaka Mitano basi tuwekewe miuondombinu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya, tunazo changamoto, kuna zahanati zilijengwa na *TASAF* ambazo zina shida ya Waganga Wasaidizi ambazo ni pamoja na Gurungu, Njirii, Ipande, Kitopeni, Ukimbu na Kintanula. Sasa wakiziangalia hizi kwa macho mawili naamini Serikali ya hapa kazi hawa wanaolaumu baadaye wataacha kulaumu kwa sababu Serikali imefika kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze juhudi za Mheshimiwa Waziri wa Viwanda aliposema kwamba nchi hii itakuwa ya viwanda. Moja ya eneo ambalo nitapenda kuona juhudi za Serikali zinachukuliwa ni pamoja na kuwa na kiwanda kwa Mkoa wa Singida na mikoa yote ya katikati. Jimbo langu lina malighafi nyingi ya *gypsum* itakuwa vizuri kutengeneza ajira kwa ajili ya vijana wetu kwa sisi kupatiwa kiwanda cha malighafi inayopatikana pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maliasili, kumekuwa na changamoto nyingi, hatujafika mahali pazuri kuvuna maliasili zetu. Tumekuwa tunaweka vikwazo matokeo yake kunakuwa na wezi wa mbao misituni kwa sababu hatuko rafiki sana katika kuhakikisha zile mali ambazo zime-*mature* kwa ajili ya uvunaji. Tumekuwa tuna-*ban* sana lakini pia tumekuwa na tatizo kubwa la uwekezaji katika kuhakikisha kwamba kuni hazitumiki nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaiomba Serikali ije na mpango mzuri wa gesi. Nchi yetu imegundua gesi, sasa gesi imefika Dar es Salaam si vibaya kukawa na mpango wa gesi ile iende Mwanza ipite Mkoa wa Singida na sisi tunufaike kama wananchi ambao ni walipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mitamba alizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri lakini bado hata mimi nasema bei zile ni kubwa si vibaya zikaboreshwa ili baadaye na wafugaji wetu nao wakanufaika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kabla sijaanza kuchangia kumsifu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kuratibu kazi hii ya kuandaa Mpango wa Miaka Mitano na hatimaye ameuwasilisha leo mbele ya Bunge hili.

Natoa shukrani nyingi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi ambazo imefanya mpaka sasa hivi. Ni kazi nyingi na nyingi zinaonekana kwa macho sio lazima kuambiwa.

Kwa hiyo, napongeza sana kazi ambazo zimefanyika mpaka sasa hivi. Kuanzia Awamu ya Kwanza, ya Pili, ya Tatu na sasa hii Awamu ya Tano ya hapa kazi tu naamini inajenga matumaini makubwa kwamba tuendako sasa kutakuwa na mafanikio na maendeleo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili viwanda vijengwe, viendeshwe kwa mafanikio na vistawi nchini, vinahitaji sana miundombinu ya barabara kuu za lami, za Mikoa, za Wilaya, za Kata hadi kwenye Kijiji ili malighafi iweze kufikishwa kiwandani au viwandani unahitaji miundombinu hiyo iweze kupitika muda wote wa mwaka. Kwa hiyo, kwenye Mpango nimesoma, nimeona kuna mipango mingi imepangwa mle, nachohitaji ni kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti ili tuweze kufanikiwa. Kama usimamizi utalegalega itakuwa ni taabu, bidhaa haziwezi kufika sokoni vizuri na bei inaweza ikawa kubwa kama miundombinu hai-*support* bidhaa kufika sokoni kwa urahisi. *(Makofi)*

Nataka nikumbushe tu eneo moja ambalo liko kwenye Mpango ambalo linahitaji macho mengi kuangalia na kujua. Kati ya Chunya hadi Mkiwa, wapo takribani watu 1,500,000 ambao wanafanya shughuli nyingi sana za kiuchumi katika maeneo hayo. Ile barabara iliamuliwa tangu mwaka 2005 kwamba ijengwe kwa kiwango cha lami. Imechelewa na mimi nahitaji umadhubuti mkubwa katika kusimamia na kukumbuka. Nilikuwa nataka nipaze sauti kali ili Mheshimiwa Profesa Mbarawa huko aliko asikie lakini kwa sababu atakuja kusoma kwenye *Hansard* basi siwezi kupiga kelele hapa. Naomba sana hiyo barabara ikumbukwe kwa sababu kuna kazi nyingi sana za kilimo na maliasili nyingi sana katika maeneo hayo ambazo zikivunwa na zikafikishwa viwandani zinaweza kusaidia sana uchumi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia yoyote ile wataalam wa barabara wanatumia aina mbili za *models* kwa ajili ya kuamua barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami au isijengwe. Wanatumia *HDM (Highway Development Model)* au wanatumia *RED (Road Economic Decision)*. Zote hizi ukizifanyia ukaguzi utagundua kwamba barabara hii inafaulu kwa *model* zote mbili.

Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waziri wa Ujenzi mwongeze jicho lenu kwenye hii barabara ili kusudi watu wa maeneo hayo waweze kupata unafuu. Miundombinu mingine ambayo inahitajika kwa ajili ya viwanda na umeme mijini na vijijini; vijijini unahitajika zaidi umeme, tuwashukuru *REA* kwa kazi wanayoifanya. Awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu naomba ikamilike kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pesa ambazo zimepangwa kwenye Mpango ziwe zinafika kwa hawa watu wa *REA* ili kusudi utekelezaji ufanyike kwa wakati. Bila kufanya utekelezaji kwa wakati, hatutafanikiwa malengo yetu. Kwa sababu hata kama utajenga kiwanda halafu kikakosa umeme, hakitazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana hiyo miundombinu wezeshi itiliwe mkazo kweli kweli katika kuisimamia na hii ni pamoja na mitandao ya simu. Katika maeneo yetu mengi hasa kwenye Wilaya yangu ya Sikonge, tuna-*coverage* ya asilimia 45 tu ya mitandao ya simu. Sasa watu watapashana vipi habari? Watapeana vipi habari za masoko? Watauza vipi bidhaa zao bila kuwasiliana? Kwa hiyo, hili la mitandao ya simu nalo naomba liwekewe mkazo sana katika usimamizi ili kusudi tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ambacho ndiyo kiwezeshi kikubwa kinachohitajika kwa ajili ya viwanda; kazi ya Serikali popote duniani huwa ni tatu. Kwanza, ni utafiti wa mbegu, miundombinu ya mazao na kadhalika; ya pili ni huduma za Ugani; na ya tatu ni kumlinda mkulima apate haki ya jasho lake. Hizo kazi ndiyo kazi za msingi za Serikali popote duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mpango yameandikwa mengi, lakini naomba sana mkazo utiwe kwenye hayo maeneo matatu. Ni lazima utafiti ufanyike kuanzia Mtwara huko kwenye korosho mpaka kwenye tumbaku; kuna kilio kuhusu uwekezaji mdogo kwenye utafiti. Naomba sana Serikali ikumbuke suala la utafiti ni kazi yake ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni huduma za ugani. Viko vijiji vingi havina Maafisa Kilimo ambao wanawajibika kuwashauri wakulima kuhusu kilimo bora. Sasa hili nalo linahitaji umakini wa hali ya juu wa Wizara ya Kilimo ili kusudi wananchi waweze kusaidiwa walime kilimo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, ni kumlinda mkulima apate haki ya jasho lake na hapo ndipo kuna matatizo makubwa. Mifumo ya pembejeo ina matatizo makubwa; wakulima wanapata madeni makubwa. Naomba sana Serikali ifanyie kazi suala la mifumo ya upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na kwa njia rahisi kusudi watu wetu waweze kulima bila usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo ya masoko nayo ni tatizo kubwa ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi. Wakulima wanapunjwa bei na kuchelewa kulipwa. Hayo inatakiwa yafanyike ili kusudi kilimo chetu kiweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa elimu kwa ajili ya kusaidia viwanda, tunahitaji shule maalum za kilimo na ufundi stadi zirejeshwe au zirejeshewe makali yake kama ilivyokuwa zamani. Zirejeshewe hadhi yake na

zijengwe na nyingine mpya kwenye maeneo mbalimbali. Hii ni pamoja na kila Wilaya kuwa na *VETA,* hiyo itasaidia kupatikana nguvu kazi ambayo inahitajika viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo ningependa nizungumzie hapa, limetajwa kwenye  Ilani ya Uchaguzi, lakini kwenye Mpango sijaliona vizuri; suala la vikundi kazi vya kijamii vya vijana; vikundi kazi vya ujenzi, mafundi seremala na vya uzalishajimali. Tunajua Mipango ipo lakini ni muhimu sana tusisitize hili kusudi hivi vikundi kwanza vipate kazi kwenye Halmashauri zetu, vijiimarishe kiuchumi ili baadaye vyenyewe viweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo napenda kulizungumzia ni ufuatiliaji na tathmini. Ufuatiliaji na tathmini unaanzia kwenye mapato na matumizi. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Tano, inafanya kazi nzuri sana ya kufuatilia mapato ili kuhakikisha kwamba Serikali inapata kile ambacho inastahili kukipata kutoka kwenye kodi na vyanzo vingine ambavyo siyo vya kodi. Ni muhimu sana suala hili liendelee kutiliwa mkazo isijekuwa baada ya miaka mitatu tukarudi kule kule tulikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la kudhibiti matumizi; ilipoanzishwa *MTEF* mwaka 1999 ilikuwa matumizi yanaruhusiwa tu kwenye vile vipengele ambavyo vilipitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kadri ambavyo tumeendelea mpaka sasa hivi, matumizi yamekuwa yanabadilika, baada ya miezi sita watu wanaomba *reallocation* nyingi Wizara ya Fedha. Sasa matumizi lazima yadhibitiwe kwenye vifungu ambavyo vimepitishwa na Bunge kusudi baadaye tuboreshe mipango yetu ili izingatie uhalisia. Hapo tunaweza tukafanikiwa vizuri kutekeleza malengo yetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mianya ya wizi, mikataba na usimamizi wake iendelee kudhibitiwa ili kusudi yale ambayo yamepangwa kwenye mkataba yaweze kutekelezwa kama yalivyopangwa. Vile vile *flow* ya fedha inatakiwa isimamiwe vizuri ili kusudi fedha ambayo imepangwa kwa ajili ya mkataba fulani ifike kutekeleza huo mkataba. Nadhani tukifanya hayo, huu Mpango wetu utatekelezeka vizuri na tutapata mafanikio makubwa na nchi yetu itafikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, yangu yalikuwa ni hayo tu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi!

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2016/2017. Kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ambao walinipa kura za kishindo ili niweze kuwawakilisha vyema katika vikao hivi vya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawashukuru sana wanawake wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kuwashukuru wapigakura wote wa Mkoa wa Ruvuma ambao wamehakikisha kwamba Chama cha Mapinduzi kinashinda Majimbo yote ya Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye suala la umeme. Kwa kuwa kwenye Mpango huu kimsingi tumejipanga kuhakikisha kwamba tunakua kiuchumi hasa kupitia viwanda; na kwa kuwa viwanda vyetu haviwezi kuendeshwa bila kuwa na umeme wa uhakika; sijaona mpango mzuri ambao umewekwa kuhakikisha kwamba umeme wa *grid* ya Taifa kutoka Makambako kuelekea Songea unasimamiwa vizuri ipasavyo na kuhakikisha kwamba mradi huu wa umeme unatekelezwa kwa haraka ili kurahisisha ujenzi huu au Mpango huu wa Viwanda ambao Taifa kwa ujumla limejipanga hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mashaka yangu ni kwamba, inawezekana kabisa Mkoa wa Ruvuma tukaachwa nyuma kwa kuwa bado umeme huu wa *grid* ya Taifa haujafika huko. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati ahakikishe kwamba katika bajeti hii, suala la kuhakikisha kwamba umeme wa *grid* ya Taifa unafika Mkoani Ruvuma ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba nizungumzie suala la maji. Kwa kuwa suala la maji ni muhimu sana katika ustawi wa maisha ya binadamu hasa wananchi wetu na kwa ujumla nchi nzima, naomba leo niongelee eneo moja la shida ya maji ambayo inaukumba Mkoa wa Ruvuma. Katika Wilaya ya Tunduru, Namtumbo, Songea Mjini, Songea Vijijini, Madaba, Wilaya ya Nyasa pamoja na Wilaya ya Mbinga, kiukweli kuna shida kubwa sana ya maji. Katika Mpango huu wa utekelezaji wa mwaka 2016/2017 sijaona mkakati madhubuti ambao utapelekea kupunguza adha ya maji kwa wanawake wa Mkoa wa Ruvuma.

Kwa hiyo, nadhani ni vizuri Wizara hii ya Maji ione umuhimu katika kuhakikisha kwamba endapo hakutakuwa na uwezekano wa kupata maji ya mtiririko kwa mwaka huu, basi wanawake wale waweze kuchimbiwa hata visima virefu wakati wanaendelea kusubiri mpango wa maji ya mtiririko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kimsingi Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma zina shida hiyo na wanawake wa Mkoa wa Ruvuma ni wanawake

ambao ni wajasiriamali, lakini pia ni wakulima. Kwa hiyo, wanatumia muda mwingi sana kwenda kufanya shughuli ya kutafuta maji badala ya kwenda kufanya shuguli zao za kilimo na hata nyingine za ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia suala la bandari kama Mpango ulivyoainisha suala la kuboresha bandari. Katika Wilaya ya Nyasa tuna ziwa Nyasa lakini pia kuna gati la Ngumbi. Zabuni ya ujenzi wa Gati ya Ngumbi ulikamilika tangu Januari, 2015, lakini ujenzi mpaka sasa hivi haujaanza na wala hakuna matumaini yoyote. Katika Mpango huu sijaona kama kuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya mwendelezo huo, ni maneno tu yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba Mpango huu wa ujenzi wa Gati hii ni wa muda mrefu sana takribani miaka 20 sasa. Kwa kuwa katika Mpango huu pia bado halijaingizwa hili suala, ni mashaka yangu kwamba inawezekana tunaingiza vitu kwa maana ya mpango lakini utekelezaji unakuwa sivyo. Naomba sana, Gati hili la Jimbo la Nyasa litengewe fedha kwa ajili ya utekelezaji na siyo maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la kilimo. Mkoa wa Ruvuma ni Mkoa ambao unashika nafasi ya nne Kitaifa kwa suala la kilimo. Pamoja na mazao mengi yanayozalishwa katika Mkoa wa Ruvuma, lakini leo naomba niongelee zao ambalo linazalishwa katika Wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma ambalo ni zao la mahindi. Hili ni zao la chakula katika Mkoa wetu lakini pia ni zao la biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mpango Mzuri wa Serikali wa kuhakikisha kwamba unatoa Ruzuku ya Serikali kwa ajili ya pembejeo za kilimo kwa maana ya *voucher,* niseme tu kwamba *vouchers* hizi kimsingi hazimnufaishi mwananchi wa kawaida wa pato la chini. Badala yake kumekuwa na vurugu, yaani kutokuelewana baina yao wenyewe; wananchi wao kwa wao pamoja na wanaosimamia. Tatizo ni kwamba *voucher* ni kidogo na hitaji ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiria kwamba ni vizuri basi Mpango huu wa Serikali ungekuja na Mkakati maalum namna gani unamwezesha mwananchi ili aweze kupata pembejeo za kilimo kwa bei nafuu baada ya kuondoa kodi ili kila mwananchi aweze kuchukua pesa yake kununua pembejeo za kilimo kwa bei nafuu badala ya kuwa baadhi wanapata *voucher* na wengine hawapati. Matokeo, mnatusababishia ugomvi ambao siyo muhimu kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani Mpango huu ungekuja na Mkakati wa kuona namna gani kodi inaondolewa na wananchi wale waweze kufikiwa, mmoja baada ya mwingine aweze kujikimu mwenyewe kununua pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Mpango Mzuri wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wananchi wanawezeshwa kwa maana ya Shilingi milioni 50 kila Kijiji na kila Mtaa, ni mpango mzuri sana wa kuhakikisha kwamba uchumi wa mwananchi mmoja mmoja unakua. Naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mpango huu pia sijaona mkakati madhubuti ambao umewekwa kuhakikisha pesa hii inayoenda kwa ajili ya kumwinua mwananchi mdogo, inatengeneza mazingira ya kumwondolea kodi zisizokuwa za lazima au ushuru usiokuwa wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hii inalenga kabisa kuwainua watu wafuatao: kwa mfano, vijana, mama lishe, bodaboda, wauza matunda na wauza mboga mboga. Sasa ushuru ambao wanatozwa kwenye masoko yao ni ushuru mkubwa. Haiwezekani mtu ana fungu tano za nyanya anatozwa Sh. 1,000/= kutwa! Hiyo ni shida! Kwa hiyo, Mpango huu uende na mkakati wa kuona ni namna gani wataondoa huo ushuru usiokuwa na umuhimu ili kumfanya mwananchi huyu, kweli kile anachokipata aweze kukizungusha na kujikimu katika maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Benki ya Kilimo. Ni jambo jema Serikali kuanzisha Benki hii ya Kilimo, lakini ndani yake nimeona kuna vitu ambavyo siyo sahihi. Benki hii imeanzishwa kwa madhumuni ya kumwinua mkulima, lakini kwenye utekelezaji iko ndivyo sivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma vizuri kwenye mapendekezo ya Mpango huu na nimeona kwamba kuna baadhi ya mikoa ambayo imetengwa kwa ajili ya majaribio na imeshaanza kupelekewa fedha. Baadhi ya hiyo Mikoa ni Iringa; sina shida, wananchi wa Iringa wanalima, lakini pia Mkoa wa Njombe sina tatizo nao, wanalima vizuri tu; Mkoa wa Morogoro nao pia ni wakulima wazuri; hata Pwani, wanalima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vitu vya kushangaza sana eti Mkoa wa Dar es Salaam nao umepangwa kwa ajili ya watu kupata pesa ya kilimo. Jamani, tuseme ukweli, hivi Dar es Salaam kuna mashamba ya kulima? Mbona hatujaona hayo mashamba, wanalima wapi? Ina maana kuna mashamba Mikocheni, Oysterbay na hapo Sinza Mori? Haya ndiyo mambo ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayataki na ndiyo anayamulika. Haya ni sehemu ya majipu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli Serikali imejipanga kumwinua mkulima wa kawaida wa hali ya chini, ni vizuri basi malengo haya yakaenda moja kwa moja kwenye maeneo ambayo wananchi wapo na wanalima kweli,

badala ya kwenda kuwanufaisha tu watu wamekaa tu maofisini, wengine wamekaa kwenye magari yao, *full* viyoyozi, wanapata pesa za kilimo ilhali hawalimi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niongelee kuhusu suala la Uwekezaji. Mpango wa Serikali juu ya suala la uwekezaji naona ni mzuri, lakini pia nadhani uende sambamba na kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yalikuwa yamechukuliwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza viwanda kwa maana ya ardhi ya wananchi ambayo imechukuliwa, basi Mpango huu wa Serikali wa kuendeleza viwanda uende sambamba na kulipa fedha za fidia kwa wananchi ambao wamechukuliwa maeneo yao, ikiwemo eneo la Mwenge Mshindo katika Wilaya ya Songea Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sana wawekezaji hawa *EPZ* wamechukua maeneo makubwa sana ambayo mpaka sasa hivi inakaribia miaka 15 au 16 wananchi hawajalipwa pesa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba kwenye suala la miundombinu, barabara inayotoka Makambako kwenda Songea…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani!

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Nayo pia ifanyiwe marekebisho ni mbaya sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngonyani, muda wako umekwisha.

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naipongeza sana Serikali kwa kazi

kubwa na nzuri wanayoifanya na hasa hii dhana ya kuwajibika Serikalini, ni dhana muhimu sana. Haya majitu yasiyowajibika wala msirudi nyuma, yaendelee kutumbuliwa ili yapotee kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea, napenda nimrudishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa ukurasa wa 28. Ukurasa wa 28 kuna mambo ya nyongeza ambayo Mheshimiwa Waziri ameyasoma, kwenye kitabu hayapo. Yapo kumi nimeyasikia; moja mpaka kumi. Ulikwenda moja, tisa, kumi. Naomba yale kumi ya namna ya utekelezaji wa mkakati, ayaandike tuyapate. Ni ya msingi sana, nilimsikia vizuri sana kwa sababu nilikuwa hapa. Hilo ni ombi katika hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ya haraka haraka, la kwanza naomba nijielekeze ukurasa wa 15 ambapo Tanzania imekuwa ikipoteza uwezo wake wa kushindana kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia zile takwimu, zinatisha kidogo, kwamba kuanzia mwaka 2012 tumekuwa tunashindwa kuvutia mitaji ya ndani na ya nje na mbaya zaidi mwaka 2016 inatarajiwa tutakuwa nchi ya 139 katika nchi 186 katika kuvutia mitaji ya ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri, katika mkakati mzima wa kutekeleza Mpango wetu mzuri wa miaka mitano inayokuja, ni muhimu sasa Serikali na Wizara tukajua ni kwa nini hasa tumeshindwa kuvutia wawekezaji? Ni kwa nini hasa tumeshindwa kuvutia mitaji ya ndani? Tatizo ni nini? Ni urasimu kwenye vyombo vyetu huko *TIC* au tatizo ni nini hasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima iwepo sababu ambayo inafanya nchi yetu ishindwe. Katika nchi 186 kwa mujibu wa vigezo vya *World Bank,* tunapokuwa nchi ya 140, ni sawa na kuwa nyuma kabisa. Kwa hiyo, *nawiwa* kusema kwamba ni vyema Serikali yote ikae kuelewa kwa nini tumeshindwa kuvutia mitaji ya ndani na nje na ukizingatia mpango mzima kwa kiwango kikubwa, umetamka kwamba utashirikisha sekta binafsi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kusema ni kilimo ambalo wenzangu wamelisemea, lakini niseme eneo dogo tu, kwenye Benki ya Kilimo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakubaliana nami kwamba kama kweli tunataka kuwa nchi ya viwanda kwa dhati kabisa, ni lazima tuweke nguvu kubwa sana kwenye Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya nyenzo za kukuza Sekta ya Kilimo ni pamoja na Benki hii ya Kilimo. Kwa mujibu wa hotuba hii, Benki ya Kilimo haina mtaji na kama inao ni kidogo sana. Ina Shilingi bilioni 60 tu, ukiachilia mbali kwamba Benki hiyo iko Dar es Salaam na wamekuja kwenye Kamati yetu

tumewashauri kwamba wajitofautishe ili ikibidi sasa wahamie katika maeneo ya uzalishaji ili iwe Benki ambayo kweli ni kioo, ni Benki ya Wakulima na hakika isiwe Benki iliyoko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri mmoja kwa Serikali na hasa Wizara ya Fedha, hatuwezi kuendelea kama ilivyokuwa mwaka wa 2015 kwamba Benki ya Kilimo haina mtaji, lakini wenzao wa *TIB, Alhamdullah* wana angalau Shilingi bilioni 212. Benki ya Kilimo ambayo tunaitarajia isaidie wakulima ili wazalishe, hatimaye nchi iingie kwenye nchi ya viwanda na viwanda vingi viwe vya kuchakata mazao ya kilimo, bado Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuna haja kubwa kama Serikali mwangalie namna nzuri ya kuwezesha Benki hii ya Kilimo iweze kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo njia nyingi. Kwa mfano, kama wenzetu wa *DANIDA* waliweza ku-*support CRDB* na mnaona ilipofika, kama wenzetu wa *DANIDA* waliweza ku-*support PASS* kule Morogoro na mnaona *PASS* ilipofika, kwa nini Mashirika rafiki na nchi rafiki pengine zenye masharti rafiki msizihusishe katika mkakati mzima wa kuiwezesha Benki ya Kilimo kupata mtaji unaoeleweka? Nina hakika mkifanya hivyo Benki hii itasambaa katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niweke angalizo; hatuwezi kuzungumza nchi ya viwanda kama hatuwezi kuwezesha Sekta ya Kilimo. Hilo ni lazima tukubaliane kabisa na bado kuna matatizo makubwa hata kwenye bajeti ya Sekta ya Kilimo. Mheshimiwa Waziri unajua kwamba bajeti ya pembejeo iko chini sana. Sasa kama bajeti ya pembejeo ipo chini sana kwa maana ya mbolea, mbegu, viatilifu, tafsiri yake ni kwamba hiki kilimo tunachotaka baadaye iwe ndiyo nguvu ya kujenga viwanda vya ndani, hiyo azma inaweza ikashindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu *sincerely* kabisa ni kwamba lazima tuangalie namna nzuri ya kutoa fedha za kutosha kwenye eneo la pembejeo na hasa mbolea. Kwa takwimu za wenzetu wa Wizara ya Kilimo ni kwamba hata uzalishaji wa chakula mwaka 2015 ulishuka kwa takribani tani 500,000. Ni dhahiri tukienda katika mfumo huu ambapo hata fedha za pembejeo za kilimo zimeshuka, tafsiri yake ni kwamba uzalishaji wa mazao ya kilimo utakuwa chini *and consequently* itakuwa ni ngumu sana kupata mazao ya kutosha kumudu viwanda vyetu vya ndani na hatimaye tuweze kuboresha maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limenivutia sana ni hii miradi ya kipaumbele hasa reli ya kati. Naomba Serikali ifahamu kabisa tukisema reli ya kati, maana yake ni reli inayoanzia Kigoma inaishia Dar es Salaam, ndiyo reli ya kati na ndiyo jina lake. Mwanzo wa reli ni Kigoma na mwisho wa reli ni Dar es Salaam. Msingi wake ni mmoja tu, kwamba hii reli kule

Kigoma itakuwa ni mkakati wa ku-*tape* kutoka nchi ya Kongo Mashariki ambako kuna shaba nyingi sana, *zinc* nyingi sana na mbao nyingi sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kwamba mzigo ulioko Mashariki ya *DRC* ni takribani tani milioni nne na hizo zinaweza kufika kwenye bandari na kwenda kwenye masoko nje ya nchi kupitia reli ya kati. Reli ya kati maana yake ni Kigoma - Dar es Salaam. Matawi yake ndiyo Tabora - Mwanza, Tabora – Kaliua – Mpanda na sasa hii mpya ya Uvinza – Msongati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo tafsiri ni muhimu sana ili tuelewane vizuri. Kwa sababu bila kuwa na tafsiri hiyo, tafsiri yake ni kwamba ule mkakati wa tani milioni nne za Kongo ya Mashariki, hautaweza kupita Bandari ya Dar es Salaam. *Sincerely* nashauri hata ujenzi wa reli ya kati kwa *standard gauge* uanzie Kigoma kwa ku-*tape* mali iliyoko *DRC* halafu reli hiyo itoke Kigoma ndiyo ijengwe kuelekea Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la mwisho ni utafiti. Nimesoma kwenye kitabu cha hotuba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha umeanisha vizuri sana umuhimu wa utafiti, lakini liko jambo moja linahitaji uelewa tu wa jumla. Kwa nini Taasisi zetu za Utafiti, ili zipate fedha za Utafiti lazima eti zikashindanie *COSTECH?* Ni mambo ya ajabu kabisa haya! Nina hakika haya mambo ndiyo Mheshimiwa Magufuli hataki hata kuyasikia!

Mheshimiwa Naibu Spika, watafiti wako Ilonga, Uyole, Mlingano, lakini eti fedha za utafiti zinapelekwa *COSTECH* wakazishindanie ndiyo ziende kwenye Taasisi za Utafiti, kwa nini? Hivi unahitaji kwenda shule kulijua hili? Kwa nini pesa hizi zisiende kwenye utafiti moja kwa moja? Kwanza itapunguza urasimu na itapunguza muda wa fedha kutoka Hazina na kufikia Vyuo vya Utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, nakualika Mheshimiwa Waziri wa Fedha, utembelee Kituo cha Utafiti cha Cholima kilichoko Dakawa. Hicho ndiyo kituo ambacho ni *known* kwa utafiti wa mpunga. Waheshimiwa Wabunge, kama tukiendelea hivi bila utafiti kwenye Kituo hicho nchi hii tutakosa mchele kwa miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yetu tumekwenda pale, tumekuta mambo ya ajabu sana! Hawa watu wana miaka mitatu hawajapata fedha kwa ajili ya utafiti. Fedha kidogo waliyoipata, eti wanashindanishwa na *COSTECH!* Mimi sielewi! Wala haikuingia kwenye kichwa changu hata kidogo, kwamba watafiti, wasomi wazuri, Watanzania hawa wanaanza tenda, ku-*lobby* kule *COSTECH* ili wapate fedha kuendesha utafiti kwenye Vyuo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali mjue wazi kabisa kwamba Vyuo vya Utafiti hasa kwa mazao ya kilimo vinajulikana; vipo Uyole, Naliendele,

Ilonga, Ukiriguru, Mlingano, Seriani na kadhalika. Wapelekeeni fedha hao moja kwa moja, ni wataalam na wasomi wazuri katika jambo hili. Kupitisha hizi fedha *COSTECH* ni kupoteza wakati tu na kuweka urasimu ambao hauna sababu. *(Makofi)*

Mwisho kabisa naomba nami kwa namna ya pekee niwashukuru wapigakura wangu wa Kasulu Mjini kwa kuniwezesha kurudi Bungeni, maana haya mambo ni mazito!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwashukuru, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. Mkakati ni mzuri na msonge mbele. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya michango ya wenzetu, wengine wataendelea mchana kwa maana ya saa 11.00 tutakapoanza tena. Sasa kwa sababu majina yanaenda kuchapwa, inakuwa ngumu, lakini kwa wale niliokuwa nimewataja lakini hawakuwepo, ndio watakaoanza mchana.

Kuna matangazo mawili hapa; Tangazo la kwanza, Kamati ya *PAC* wanaombwa na Mwenyekiti wao wakutane saa saba katika ukumbi Na. 227. Nadhani hiki chumba kiko jengo la Utawala.

Tangazo lingine tunarudia tena tangazo tulilotoa asubuhi, ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Uongozi, yaani Mheshimiwa Spika, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti wakutane saa 9.00 alasiri kwenye ukumbi wa Msekwa kwa ajili ya kujadili mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka niliombwa Mwongozo asubuhi, kwa hiyo, nitaongea mambo mawili; nitaongea kuhusu Mwongozo, lakini pia nitaongea kuhusu jambo lililojitokeza wakati Mheshimiwa Kuchauka akichangia.

Kwanza kuhusu Mwongozo; uliotolewa kwamba: Je, alichokuwa amesema Mheshimiwa Mwijage ni msimamo wa Serikali au ni msimamo wake yeye kama Mheshimiwa Mwijage ambaye ni Waziri wa Viwanda? Mambo yaliyozungumziwa yalikuwa mawili; kuhusu bei ya mazao kuwa chini na pia kuhusu watu wa Lindi kujiandaa kulima mihogo kwa ajili ya kupeleka nje.

Waheshimiwa Wabunge, kesho Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, atapewa muda mahususi kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa hoja hizo mbili alizokuwa amezitoa. Kwa kifupi, ni kwamba bei za mazao kuwa chini pengine ni huo msamiati ambao utaelezewa vizuri kesho, lakini kimsingi ulimaanisha ni uzalishaji wa tija badala ya bei ya mazao kwa maana ya kwamba ukiwa na

uhakika wa zao lako kuuzwa, unakuwa huangalii sana bei unayouzia, lakini unaangalia kwamba una uhakika wa soko. Kwa hiyo, kesho utatolewa ufafanuzi zaidi, kama kutakuwa na mengine, basi yatashughulikiwa wakati huo.

Kuhusu watu wa Lindi kujiandaa kulima mihogo, hoja hii haikumaanisha waache kulima wanavyolima vingine, ni kwamba hii ni fursa sasa imejitokeza ili mihogo hiyo itakapolimwa soko liko tayari linasubiri, China. Kwah iyo, ni fursa nzuri Waheshimiwa Wabunge, nadhani tuipokee kwa namna hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nimesema nitatoa maelezo kuhusu mambo yaliyojitokeza wakati Mheshimiwa Kuchauka akitoa maelezo yake kuhusu Mpango wa Miaka Mitano ambao umewasilishwa na Serikali. Mheshimiwa Kuchauka alipewa taarifa na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, lakini pia ikatokeza taarifa nyingine ya Mheshimiwa Sungura.

Mheshimiwa Kuchauka alisema hivi, si kwa kunukuu, kwamba Liwale ingekuwa mpakani angeweza kushawishi wananchi wa Liwale kujiondoa Tanzania na kujiunga na nchi jirani, kwa namna anavyoona Liwale ni kama imesahaulika.

Waheshimiwa Wabunge, ukisoma Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Ibara ya 28, inaongelea Ulinzi wa Taifa. Nitaisoma ili tuweke kumbukumbu sawasawa; Ibara ya 28(1) "Kila raia ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa Taifa." Ibara ndogo ya (2), "Bunge laweza kutunga sheria zinazofaa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kutumikia katika majeshi na katika ulinzi wa Taifa."

Ibara ndogo ya (3), "Mtu yeyote hatakuwa na haki ya kutia sahihi kwenye mkataba wa kukubali, kushindwa vita na kulitoa Taifa kwa mshindi wala kuridhia au kutambua kitendo cha uvamizi au mgawanyiko wa Jamhuri ya Muungano au wa sehemu yoyote ya ardhi ya eneo la Taifa na bila ya kuathiri Katiba hii na sheria zilizowekwa, hakuna mtu atakayekuwa na haki ya kuwazuia raia wa Jamhuri ya Muungano kupigana vita dhidi ya adui yeyote anayeshambulia nchi."

Waheshimiwa Wabunge, Ibara ndogo ya tatu, inanitaka nitoe maelezo haya, kwa maana ya kwamba ni taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Sungura ya kuuliza swali kwamba je, Kigoma ni sehemu ya Tanzania au ni sehemu ya Burundi? Ni tofauti na ukisema Liwale kama ingekuwa mpakani, ingeweza kushawishi ijiunge na nchi nyingine, kwa sababu kauli hiyo inakuwa imekwenda kinyume na Katiba, kwa sababu hii Ibara ya 28(3) inakataza kugawa ardhi ya Tanzania. Kwa hiyo, ukitoa kauli kama hiyo inaonekana kama unafanya uchochezi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba wakati wa mijadala hii tuangalie kauli zetu tunazozitoa zisije zikatafsirika kwamba tunavunja Katiba ambayo tumeapa kuitetea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. John A. Chenge) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na katika wachangiaji, wa kwanza kabisa tunaye Mheshimiwa Msigwa, Mbunge wa Iringa Mjini. Karibu Mheshimiwa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami naona nijaribu kushauri na kutoa mchango wangu kuhusiana na *agenda* iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali kadhaa ambayo napenda kumuuliza Waziri wa Fedha kwamba katika Mpango huu, ni kwa namna gani mambo haya ameyazingatia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu toka tumepata uhuru, ni Taifa ambalo limekuwa tegemezi. Tumekuwa tukiendesha bajeti yetu na masuala mbalimbali ya kimaendeleo kwa kutegemea Wahisani au Wafadhili. Takwimu nilizonazo mpaka sasa ni kwamba kwa kipindi cha miaka 40, Jumuiya ya Ulaya imetoa zaidi ya *Euro* bilioni tatu kusaidia shughuli za kimaendeleo ambazo zimekuja kwa mfumo wa Kiserikali. Ukiacha mashirika kama *Maria Stops* na mashirika mengine kwa mfano kutoka Uingereza, hivi vyote vimekuja kuchangia na vimesaidia sana kukuza maeneo ya elimu, miundombinu na afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye eneo la afya, Marekani na mashirika yake mengi sana yamesaidia sana Sekta ya Afya kusaidia wauguzi wetu namna ya kutatua kero mbalimbali za afya. Vile vile Kiserikali, mashirika kama *DFID* kutoka *UK*, *USAID, UNFPA* inayoshughulika na idadi ya watu duniani, haya yote yametoa michango kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka Taifa ambalo linajitegemea na tumekuwa tukijinasibu sana kwenye vyombo vya habari kwamba tunataka Taifa liwe la kujitegemea, kitu ambacho ni kizuri. Napenda Waziri wa Fedha aniambie, ni namna gani mpango wake una-*reflect* kuachana na huu

utegemezi wa muda mrefu ambapo toka tumepata uhuru tumekuwa tukiwategemea hawa watu? Katika kipindi cha miaka kumi tumepoteza watoto zaidi ya 600,000 ambao wamekufa kwa utapiamlo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu sasa hivi kila saa moja mama mmoja mjamzito anakufa. Maana yake ni kwamba kwa mwaka tunapoteza akinamama wajawazito 9,000. Ni namna gani Mpango huu una-*reflect* kwamba tutahama kutoka kwenye hii hali ambapo tunapoteza watoto na akinamama wajawazito? Huduma ya afya kwa kiwango chote tunaitegemea kutoka nje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Taifa hili asilimia karibia 50 ya watoto wanaozaliwa ni *stunts.* Kuna *mental retardation* ya kutosha katika nchi; na wanasema pale anapokuwa mtu mmoja amedumaa, kuna watu wengine ambao wana *mental retardation* watano. Ni namna gani Mpango huu una-*reflect* kujaribu kuliokoa Taifa hili kwenye maeneo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo Kambi ya Upinzani imezungumza, ni jinsi ambavyo Mpango uliopita ulitekelezwa kwa asilimia 26 tu. Mheshimiwa Waziri, kabla hatujaenda mbele, *you know speed is useless if you don't know where you are going or if you lost*. Kabla hatujaenda mbele unapotuletea huu Mpango, ni kwa nini Mpango uliopita tumeshindwa, ulitekelezwa kwa asilimia 26? Vitu gani vilisababisha tushindwe? Ni hatua gani zimechukuliwa? Kwa nini tulishindwa? Kwa nini hatutashindwa katika Mpango huu? Ni namna gani yale ambayo yalitushinda miaka iliyopita tutayarekebisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya kabla hatujaenda mbele ni lazima tuwe na majibu ya kutosha. Kabla hatujaparamia huu Mpango tuanze kuupitisha, tuambiwe ni kwa nini tulishindwa na kwa nini hatutashindwa kwenye Mpango unaokuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani imezungumza kwamba tunapopanga mipango lazima iwe inaendana na mazingira, kuna mipango mingine ni kweli huwa inakuwa *imposed,* haiendani na uhalisia wetu. Huu Mpango wako unasema nini kuhusu kuendeleza Sekta ya Utalii ambayo inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni? Vile vile asilimia 17 zisizo na kodi, yaani *GDP* Mpango wako unasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani? Kumekuwa na uvamizi na nashukuru sasa hivi Waziri wa Ardhi amekuja; kumekuwa na uvamizi wa mifugo, wafugaji wamevamia maeneo mengi ambayo ndiyo yanakuza Sekta ya Utalii ambayo kimsingi ndiyo yanatuletea pesa nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tena na Waziri wa Mifugo yupo hapa! Nchi yetu ina asilimia 10 kwa ajili ya ufugaji. Kwa bahati mbaya haya mashamba makubwa mengi ambayo tulitenga asilimia kumi kwa ajili ya ufugaji yamehodhiwa na watu wachache ambao kimsingi hayatumiki. Sasa maeneo haya yamesababisha hawa wafugaji waanze kuondoka sehemu ambazo tumezipima. Sasa zinaathiri kwenye *hunting industry*, zinaathiri kwenye *National Parks* wakati hii ardhi ipo, haijapangwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa juzi Waziri wa Maliasili anahangaika na tumbili wale waliokamatwa *KIA*. Ni kweli sikubaliani wanyama wasafirishwe ovyo ovyo, lakini ukiangalia tumbili na athari zinazopatikana kwa wavamizi wafugaji wanaopeleka kwenye maeneo ya uhifadhi, ni athari kubwa sana kuliko tumbili ambao tunahangaika nao pale *KIA*. Ni sawa na nyumba inaungua moto, watu badala ya kuokoa vyombo, vinateketea, wewe unamshangaa binti aliyevaa sketi fupi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo Serikali yenu! Hatuna *priorities!* Hii Sekta ya Utalii ndiyo inaiingizia Taifa asilimia 25 ya fedha za kigeni. Wafugaji najua wanapiga kelele sana, sio kwamba siwapendi, najua wengine watainuka hapa! Ufugaji katika nchi hii unachangia *one point seven* ya *GDP*, halafu mnaleta mchezo na inayochangia asilimia 17, hapa *balance* iko wapi? Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anipe majibu, mmejipangaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Iringa Mjini kwenye Sekta ya Utalii, hii *Southern Circuit* mlituambia katika Bunge hili kwamba tunataka na *Southern Circuit* kuwe na utalii, lakini Iringa Mjini pale ni mahali ambapo pamekaa kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamika sana miaka mitano hapa kwamba ule uwanja wa ndege uharakishwe, ujengwe vizuri na barabara ya lami ijengwe mapema iwezekanavyo kwenda kwenye Mbuga ya Ruaha ya *National Park* ambayo kimkakati ni hii Sekta ya Utalii. Sasa kumekuwa na maneno mengi, mara mnawapiga mkwala hawa wafadhili ambao wanatusaidia; Mheshimiwa Mpango umesema tunaweza kujitegemea, mmekejeli hata zile fedha za *MCC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekwambia hii ni nchi ambayo watoto wanakufa kwa utapiamlo. Tuambieni hii mikakati yote kwa miaka 40 tumetegemea fedha za kutoka Ulaya, mmejipangaje kujiondoa kwenye eneo hili? Naunga mkono tujitegemee, lakini tuwe *realistic,* tunaachanaje na kujitegemea? Tunatoa elimu ambayo ni *spoon feeding!* Ni elimu ya watu ambao wanamaliza shule lakini hawana mchango! Tunasomesha wachumi ambao hawana uchumi, wanataka wafundishe uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwenda kujifunza uchumi, bora niende kwa Mangi kwenye kaduka kake atanifundisha uchumi kuliko nimpate mchumi mwenye *degree* kwa sababu hana uchumi yeye mwenyewe, hawezi kuleta chakula mezani. *What kind of economics is that?* Huo Mpango wako ni lazima tuwe na majibu haya, ni namna gani tutapunguza vifo vya akinamama wajawazito? Huu Mpango tunataka utupe majibu ni kwa kiwango gani tumeshidwa miaka mitano iliyopita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 26 ni ndogo sana. Utupe majibu ya kutosha! Nami najua, tulikwambia mapema kabisa, wewe sio mwanasiasa, lakini sasa hivi naona siasa imeanza kuingia, unatoa majibu ya kisiasa. Tunataka utupe majibu ya uhalisia! Kama kweli tunajifunga mkanda, tujue tunajifunga mkanda kwa kiwango kinachotosha. Tuambiane ukweli! Zama za kudanyanyana hazipo, tuambiane ukweli kwamba hela hii walikuwa wanatusaidia Wamarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema ukifuatilia hizi hela, afya ya nchi hii tumeikabidhi kwa Wamarekani, hatuna uwezo huo! Nimetaja haya mashirika yote ya Kiserikali, achilia mbali hizi *NGOs* ambazo zote zinaleta pesa kusaidia akinamama. Haya ndiyo mambo ambayo Bunge tunatakiwa tujadiliane na tuambiane ukweli hapa! Kinachonishangaza kikubwa, ni kwa kiwango gani tunacheza na Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutengeneze Mpango *in our context.* Utalii ndiyo unaotuletea pesa nyingi katika nchi yetu, lakini matokeo yake, tunacheza na mifugo. Bahati mbaya wenzetu wa Kanda ya Ziwa, *they speak a lot,* wana *influence.* Akina Musukuma hawa wanaongea sana, wangependa hata hifadhi zile zote waingie wanyama tu. Nakubaliana kwamba mifugo ni ya muhimu katika Taifa letu, lakini hatuwezi! Hii inachangia *one point seven GDP,* tukaua inayochangia *seventeen.* Yaani tunaua uhifadhi kwa kiwango kidogo kwa sababu ya kufurahisha watu kisiasa. Naomba Mpango huu u-*reflect* ni namna gani tuta-*boost* uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunataka tuwe na uchumi wa kati, lakini ukiangalia idadi zote mlizotupa, wasomi tunaowaandaa katika sekta mbalimbali, kwa mfano, utalii una-*boom* katika nchi yetu. Sioni wale wanaohusika na *industry* hii tumewaandaa kwa kiwango gani; wale wanaohusiana na gesi tumechukua sababu za makusudi kiasi gani kuwaandaa kwa ajili ya uchumi wa baadaye badala ya kuleta siasa?

Mheshimiwa Waziri naomba haya maswali yangu niliyokuuliza kwenye Mpango wako, ina-*reflect* kiasi gani ili tuwe wahalisia, tusifanye vitu vya kubahatisha na siasa? Sasa hivi tumemaliza uchaguzi, hebu tuingie kwenye uhalisia, tusiende kwenye siasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninavyozungumza, bandari kwa taarifa zenu wenyewe, imeshuka kufanya kazi kwa kiwango cha asilimia 50. Wateja wengine kutoka Kongo wameondoka, wanakimbilia Beira. Haya mambo tutawezaje kuyafikisha kwenye uhalisia kama hatuambizani ukweli? Nasi kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi tulisema angalau *one third* ya bandari ndiyo yangekuwa mapato ya Taifa. Sasa hivi tumeshashusha asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uchumi pamoja na siasa mnazozifanya, hebu tu-*balance* kuwe na uwiano kati ya *business* na *politics.* Naona mizania ya siasa inapanda zaidi kuliko uchumi. Hebu tu-*balance,* kwa sababu mwisho wa siku, huu ni mtumbwi, tumepanda wote. Kama mwenzetu umeanza kutoboa, tutazama wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya majibu yasawazishwe ili kwa pamoja turidhiane, tuishauri Serikali. Waziri wa Ardhi unanisikia, Waziri wa Mifugo unanisikia, bahati mbaya Waziri wa Maliasili hayupo, naomba m-*balance* haya mambo; kwa sababu siku moja nimemsikia Waziri wa Maliasili na Waziri wa Mifugo, kulikuwa na sintofahamu kidogo katika eneo hili. Mimi wale tumbili hata mngeacha waende, hakuna shida. Ingekuwa tembo au faru, hiyo sawasawa. Wale Tumbili si sawa na Kweleakwelea! Wapo wengi tu, tungeuza tupate hela; lakini mnaacha uhifadhi, ng'ombe wanakwenda kule, wanaharibu uhifadhi! Hii ni kwa ajili ya vizazi vyetu vya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu machache, nimejaribu kusaidiana kidogo katika hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mheshimiwa Stephen Ngonyani akifuatwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. Mheshimiwa Ngonyani, hayupo, haya tunaendelea. Mheshimiwa Esther Matiko na baadaye Mheshimiwa Mussa Zungu. Mheshimiwa Matiko naye hayupo, tunaendelea. Mheshimiwa Zungu! Nilimwona! Haya, tunaendelea Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli! Karibu.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kushukuru kwa kupewa nafasi hii, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa kuwasilisha Mpango mzuri ambao unaonesha mwanga wa maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, ili tuweze kuendelea na kufikia uchumi wa kati, tunahitaji mipango mizuri kama ilivyooneshwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/2017 na 2016 - 2020. Katika Mpango huu kuna sehemu moja ambayo nitaiongelea sana hasa miundombinu ya barabara. Ili tuweze kuendelea kama nilivyosema, ni lazima

tuwe na barabara nzuri ambazo wakulima wengi wanazitegemea, lakini pia hata viwanda vinategemea barabara au miundombinu. Barabara nyingi zinazokwenda vijijini ambako ndiko tunakoweza kupata malighafi za kuendeshea viwanda vyetu ambavyo tunasema kwamba tunataka tuingie kwenye uchumi wa viwanda, ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na barabara nzuri, tunapokuwa na barabara za lami inakuwa rahisi kwa wakulima hawa kuweza kusafirisha mazao yao ambayo ndiyo malighafi za viwanda na hatimaye wakaweza kuuza mazao yao kwa haraka zaidi na yakapata bei nzuri zaidi; lakini siyo bei tu, hata ubora wa mazao yao na ubora wa bidhaa ambazo zitatokana na haya mazao zitakuwa bora zaidi na hatimaye kuweza kupata faida kubwa au kupata *products* ambazo zinaweza kuuzwa hata nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyo sasa hivi, *products* zetu nyingi zinakataliwa, haziwezi kupata soko la nje kwa sababu tu hazina ubora na inaonekana kwamba ubora huu unakosekana kwa maana ya kwamba bidhaa nyingi zinafika kiwandani zikiwa zimechelewa au zimeharibika. Kwa mfano, kama bidhaa za matunda, zinafika kiwandani zikiwa zimeharibika. Kwa hiyo, hata zao lake au lile zao linalokuja kutoka kiwandani linakuwa halina ubora na hatimaye zinakataliwa kwenye masoko mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba pia Mpango uweze kuboresha miundombinu ya barabara. Kwa mfano, katika maeneo ya uzalishaji, mimi natoka Jimbo la Lupembe ambapo sehemu kubwa tunazalisha chai, lakini tunazalisha matunda, mananasi, tunazalisha matunda mengine kama parachichi na mengineyo. Barabara za kule hazipitiki kwa hiyo, wakulima wanashindwa kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Waziri hasa Waziri wa Ujenzi, ukienda kuangalia jinsi gani wananchi wanavyomwaga haya mazao, jinsi gani chai inavyomwagwa kila siku, utawaonea huruma na utatamani kulia. Kwa hiyo, tuombe miundombinu hasa ya maeneo haya ambayo yana uzalishaji mkubwa, barabara zitengenezwe vizuri ili hatimaye wananchi waweze kuuza mazao yao na hatimaye kupata faida na kama Taifa kuweza kuongeza uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu kwa mfano nikisema hii ya Lupembe, ilishaingia kwenye ilani ya mwaka 2010 kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami na mara moja kwenye Bunge la Bajeti fedha zilishakadiriwa kwamba tutapewa, lakini fedha hazikutoka. Nashangaa mwaka huu pia sijaiona kwenye Mpango kama itaaanza kutekelezwa hasa huu Mpango wa mwaka 2016/2017 wakati tayari ilishaahidiwa kwamba hii barabara itatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Kwa hiyo, nakuomba Waziri wa Ujenzi nafikiri unanisikia vizuri sana na ni msikivu, hebu tujaribu kuingiza au tuingize kwenye Mpango ili sasa mazao haya ya chai na chai ya Lupembe mnaifahamu ni chai bora na ilikuwa ni moja ya chai bora duniani, ilikuwa na soko kubwa sana na zuri sana. Waliokuwa wanafuatilia mambo ya soko la chai wanajua jinsi gani ile chai ilivyokuwa na soko zuri duniani, lakini leo imepotea kwa sababu pengine ya ubovu wa njia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika Mpango wetu naomba tuangalie sana maeneo yale ambayo wakulima wanazalisha mazao mbalimbali hasa mazao ambayo yanaweza kuuzwa nchi za nje na yakatuingizia fedha za kigeni. Kwa hiyo, tukifanya hivyo, tutawawezesha wananchi hawa kwanza kuuza mazao yao, lakini pia hata bidhaa zetu ziwe na ubora na kwa kupitia hivyo tutaweza kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara zinapokuwa nzuri, tunawavutia wawekezaji. Tunasema tunaenda kwenye uchumi wa viwanda, wawekezaji hawawezi kwenda kuwekeza kwenye maeneo kama ya Lupembe ambapo barabara haipitiki wakati wa kifuku; maana yake ni kwamba, watapoteza kwa maana ya kwamba watazalisha lakini hizo bidhaa zao au mazao yao ambayo wamezalisha, hawataweza kuyauza yakiwa na ubora wake kwa sababu ya ubovu wa barabara. Kwa hiyo, maeneo haya ya uwekezaji ni lazima tuhakikishe kwamba barabara zinapitika muda wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, viwanda tunavyovifikiria, ni lazima viwekezwe au twende tukaviwekeze kwenye maeneo ambayo yana uzalishaji. Inakuwa haipendezi wala haina tija kwa mkulima kama kiwanda kinakuwa mbali na maeneo ambayo hawa wakulima wanazalisha. Inapokuwa hivyo ni kwamba, wananchi, wale wakulima wanakosa bei nzuri ya mazao kwa sababu hapo katikati wanacheza wale *middlemen,* wananunua bidhaa kwa wakulima kwa bei ya chini na wanawauzia wamiliki wa viwanda kwa bei ya juu. Kwa hiyo, tayari wakulima wetu wanapoteza soko la bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuweze kuwahamasisha wakulima, lakini pia wakulima wetu waweze kupata tija ya mazao wanayozalisha, ni lazima tuwavutie hawa wawekezaji wa viwanda mbalimbali kwenye maeneo ambako hawa wakulima wanazalisha, ndipo hapo utaweza kuwasaidia wakulima wakapata tija kwa kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda peke yake na barabara peke yake haitoshi. Ni lazima huduma za msingi hasa huduma za afya kwa maana ya Hospitali, Zahanati na Vituo vya Afya vijengwe kwenye maeneo haya ambayo kuna uzalishaji mkubwa, lakini pia kuna viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Njombe haina hospitali hata moja. Sasa hutegemei maeneo kama hayo wawekezaji watakuja kuwekeza kwa kuwa huduma ya afya haipo. Ni lazima tuangalie upande mwingine. Tunapotaka kuwekeza tuangalie na *factors* nyingine ambazo zinaweza zikasababisha wawekezaji waweze kuwekeza au inaweza ikasababisha viwanda vyetu viweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyo sasa hivi ukiangalia hata kwenye Mpango, viwanda vingi vimeelekezwa mijini. Sasa vinavyoelekezwa mjini tunawanyima asilimia zaidi ya 80 ya wakulima wanaoishi vijijini au watu wa vijijini. Kwa hiyo, tukitaka kufungua fursa za ajira, ni lazima tufikirie sasa kuanza kuwekeza kwenye maeneo ambako wakulima wapo na vijana wengi wanaishi ili tufungue ajira huko vijijini, watu wabaki vijijini kuliko sasa hivi wote wanavyokimbilia mjini. Sasa kama watakimbilia mjini, nani atakayezalisha huko vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kwamba tunafungua viwanda kule Ludewa, sasa bidhaa nyingine ambazo zinategemea hivi viwanda, watapata wapi kama hatutaweka mazingira rafiki ya kuwawezesha vijana wetu waweze kubaki vijijini? Kwa hiyo, tunaomba kwenye Mpango pia tuweke vizuri ili hatimaye tuweze kuhakikisha kwamba tunaweza kufanikiwa hasa kuingia kwenye uchumi huu wa kati ambao ni uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishati, nalo ni suala ambalo linaendana pamoja. Tukitaka tuvutie wawekezaji wa viwanda hivi vya kati na vikubwa, ni lazima tuhakikishe kwamba maeneo yetu mengi yanakuwa na nishati ya kutosha; yanakuwa na umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyo sasa hivi, kwa mfano, eneo langu ni la uwekezaji; kuna mazao mengi ambayo yana tija ambayo watu wengi wanaweza wakapata faida, lakini wawekezaji wanashidwa kuwekeza kwa sababu umeme siyo wa uhakika. Kwa hiyo, naomba Waziri wa Nishati pia katika Mpango huu tujaribu kulifikiria kuhakikisha kwamba tunasambaza umeme katika maeneo ya uzalishaji hasa maeneo ya Lupembe ambako kuna wawekezaji wengi wazuri, wanakuja lakini hawawezi kuwekeza kwa sababu hakuna nishati ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nijaribu kulisema kidogo juu ya Mpango huu, tujaribu kujadili juu ya kuhakikisha kwamba hawa vijana au wananchi ambao tumesema tutawezesha kwa kuwapa Shilingi milioni 50 kila Kijiji, ni lazima tutengeneze mpango mzuri hasa kwanza, kutoa elimu ya ujasiriamali; elimu ya matumizi ya hii mikopo ambayo tunaipanga iende kwa wananchi kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi walioko vijijini hawana elimu ya kutosha ya ujasiriamali, hawana uelewa wa kutosha wa ku-*generate* mkopo na mwisho wa siku wapate faida. Ni lazima tuweke mpango ni jinsi gani tutatoa elimu kwa wananchi wa vijijini ili mkopo huo wakiupata waweze kuutumia vizuri na mwisho wa siku waweze kupata faida na ile faida iweze kurudishwa na hatimaye tuweze kuongeza uchumi wa kila mmoja na hatimaye uchumi wa Taifa zima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tujipange kuhakikisha ni jinsi gani tutatoa elimu na siyo kutoa elimu tu; jinsi gani tutawasaidia katika kuwatafutia masoko ya bidhaa ambazo pengine watakuwa wanazalisha ili ule mkopo uweze kuleta tija? Tukiwaacha tu hivi hivi tukapeleka tu zile fedha, itakuwa kama ilivyokuwa yale mamilioni ya Kikwete. Zitaenda fedha nyingi na mwisho wa siku kitakachorudi, hakuna. Kwa hiyo, tutakuwa tumepoteza mamilioni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo nafikiri inatosha. Nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Namwona Mheshimiwa Stephen Ngonyani!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kuniona. Vile vile naanza kwa kuwapongeza Wabunge wenzangu kwa kazi nzuri ya kutoa michango katika hii hoja ya Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyokuwa Dar es Salaam nilisema huu Mpango wa Serikali ni mzuri sana. Ni mzuri sana kwa Watanzania wote! Nilivyokuwa Dar es Salaam nilisema sitaunga mkono hoja. Ni kwa nini sitaunga mkono hoja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mpango umeelekeza kwa Tanzania nzima jinsi itakavyopanga Serikali yetu ambayo tunaipenda sana ya Awamu ya Tano. Nataka tu Mawaziri watakapokuja waniletee majibu ya sehemu hizi ninazotaka kujua. Maana ya viwanda, maana ya reli na maana ya bandari. Unaposema kwamba tutaimarisha Bandari za Tanzania, moja ya bandari ni bandari ya Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Tanga toka nimeanza kuisikia kwenye vyombo vya habari na toka nimeanza kuisikia hapa ndani ya Bunge hili kwamba kutajengwa Bandari ya Mwambani, tutarekebisha bandari zilizopo sasa hivi, lakini cha kushangaza, inayong'ang'aniwa ni Bandari ya Dar es Salaam peke yake. Hizi bandari nyingine zina matatizo gani? Fedha inayotumika ni ya Serikali, siyo kwa ajili ya Bandari ya Dar es Salaam peke yake! Ni bandari zote za Tanzania zirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukaa meli sana Dar es Salaam siyo faida! Kuna Bandari ya Mtwara ambayo unaweza kupeleka meli na ikatoa mizigo ya aina yoyote. Kuna Bandari ya Tanga unaweza kutoa meli ukatoa mizigo yote, lakini tunang'ang'ania tu Bandari ya Dar es Salaam, meli zinakaa pale mwezi, wakati kuna bandari nyingine zenye kina kirefu, hakuna chochote kinachoendelea! Hii hatutendewi haki! *(Makofi)*

Tunapozungumzia reli, reli zote ni kwa faida ya Watanzania, lakini unaponiambia kwamba barabara zitatengenezwa na zitaimarika; zitaimarika namna gani kama reli zenyewe ambazo tumeanza kuziongolea toka sijaingia Bunge hili mpaka leo hii hazitengenezwi? Hiyo barabara itakayokuwa nzuri ambayo mabasi yatakuwa yanapita na magari madogo bila kuumia ni ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu Tukufu, sikivu, hebu jaribu kuiangalia na reli inayotoka Tanga, kupitia Kilimanjaro, kupitia Arusha na kwenda mpaka Musoma. Mwaka 2012 tumeijadili hii reli kwamba itajengwa lakini tunashangaa zinajengwa reli ya kati tu, lakini huku kwingine zikikorofisha kidogo zinarekebishwa. Reli hii ya Tanga mpaka Arusha mpaka Musoma, hata kuisikia kwenye vyombo vya habari, hatuisikii! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania haijengwi na reli ya kati peke yake, Tanzania haijengwi na mikoa ya kati pekee, Tanzania inajengwa na mikoa yote ya Tanzania ili mtutendee haki. Serikali hii ambayo ni sikivu inayoendelea kutumbua majipu, hebu angalieni na mikoa hii mingine ambayo mlituahidi wenyewe na tukaunga mkono kwa dhati kwamba tunachohitaji ni maendeleo. Maendeleo haya hayatapatikana kwa reli ya kati peke yake! Barabara zinazotoka Arusha kwenda Dar es Salaam, kila siku zinakarabatiwa, kwa nini? Kwa sababu reli ya Tanga haifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri katika mipango yake yote, hebu jaribuni kurekebisha hizi reli nyingine ambazo hamzipi kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye viwanda. Siku za nyuma, mikoa mitatu ndiyo ilikuwa na viwanda vingi sana hapa Tanzania; Mkoa wa Dar es Salaam, Morogoro na Tanga. Cha kushangaza, tunasema tutajenga viwanda vipya, hatukatai. Ni mambo mazuri ya Serikali kwa sababu ya kuwasaidia Watanzania ili wapate kazi. Je, viwanda ambavyo vimekufa mnaviweka wapi? Kwa mfano, kuna kiwanda cha *General Tyre* Arusha, Kiwanda cha Kahawa pale Moshi na viwanda vilivyoko katika Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga kulikuwa kuna viwanda vyenye msimamo! Kuna Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha Mbolea, Kiwanda cha Foma, Kiwanda cha Mablanketi, Kiwanda cha Mashati, kulikuwa na Kiwanda

vilevile cha kutengeneza Mbao, *Sikh Saw Mills*, kulikuwa na kiwanda pale Mkumbara cha kutengeneza *chipboard*, kulikuwa kuna Viwanda vya Chai ambavyo mpaka leo hii havijafunguliwa. Serikali imeahidi itavifungua, kwa mfano kiwanda cha Mponde, lakini hakuna! Sasa tukifanya haya mambo, tunafanya mambo tu, halafu sisi tukirudi huko nyuma ndiyo tunahukumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hapa leo tunaongea sana lakini Wabunge wakirudi nyuma watakiona chamoto. Naomba Serikali sikivu, mviangalie hivi viwanda. Leo hii tunaambiwa Kilimo Kwanza, nimekubali lakini nataka mniambie hawa wananchi wa Mkoa wa Tanga watalima wapi, wakulima wa Moshi watalima wapi, wakulima wa Morogoro watalima wapi; kwa sababu maeneo mengi yamehodhiwa na watu wachache na hao watu wachache waliohodhi hayo mashamba hawayaendelezi badala yake ni ya kukopea mikopo kwenda kununua magari ya kisasa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama watu wanakopa mikopo kwa ajili ya kununua magari ya kisasa na wamekopa kwa ajili ya kuendeleza kilimo, kilimo hicho hakiendelezwi, wananchi wanaambiwa kilimo kwanza, wakati mashamba yale ambayo wangeyategemea wananchi wa chini kulima, yamehodhiwa. Ukilima pale, mtu anakuja nyuma yake, anakupeleka Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni rafiki yangu na nampenda, anafanya kazi kwa dhati. Bahati nzuri Mawaziri wote mlioingia safari hii, hakuna Waziri mwenye shida. Wote mmeamua kumsaidia Mheshimiwa Magufuli. Haya mambo tunayoyaongea ni ya msingi sana ili kuiona Tanzania siyo tegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia masuala ya umeme, ni kitu muhimu sana kwa Watanzania, lakini nataka niulize, huu umeme wa mafuta wenye gharama kubwa tunaoukazania, kwa nini msiendeleze kituo cha Hale, Kihansi na pale Achemka ambapo ni umeme wa maji? Maji yapo! Ni lini mmesikia Mto Ruvu umekwisha maji? Kama tatizo ni maji, Mto Ruvu ni lini umekauka maji? Kwa sababu tunategemea tu kwamba tutumie mabilioni ya pesa! Hawa watu wa *Symbion* wanaokuja kutupa masharti magumu, tumshukuru Mheshimiwa amesema safari hii hatutegemei wafadhili, tunajitegemea sisi wenyewe. Sasa kama tunajitegemea sisi wenyewe tujaribu kupunguza gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hivi vituo vya nguvu za umeme ambavyo vinatoa nguvu za umeme kwa kutumia maji ambayo gharama yake ni nafuu. Tungeviongezea *engine*. Kama ni mashine, basi ziongezewe mashine kuliko kutumia umeme unaotokana na mafuta ambapo hao watu wanatupiga bei mara mbili. Watanzania wanakaa katika wakati mgumu kwa kuwalisha watu

wachache ambao wanataka kuja kutuhukumu leo kwamba hawatatupa misaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, vitu muhimu sana ambavyo tunaweza kufanya; wananchi wa Tanzania wanategemea sana kilimo, lakini hivi leo ninavyokwambia, hakuna sehemu ambayo Watanzania wanaweza kulima. Siyo kwamba nchi hii haina ardhi, ipo; lakini ardhi hii inakuwa ya masharti kama tuko Kenya. Imehodhiwa na mtu kwa manufaa yake. Nashukuru safari hii Waziri wa Ardhi, unafanya kazi nzuri sana, lakini usiangalie mikoa ya huko tu, angalia na Mikoa ya Mashariki yako. Anza Morogoro, njoo Pwani, nenda Tanga, nenda Kilimanjaro, nenda mpaka Arusha, ili ukitoa maamuzi, utoe maamuzi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, wengine wakati wa nyuma walikuwa hata ukiwapigia simu hawapokei, lakini wewe unapokea. Sasa kama unapokea, umefanya kazi nzuri kwa muda mfupi. Njoo uangalie mashamba, misitu ya kule Tanga ambayo wananchi wanalalamika sana kwamba, hawana mahali kwa kulima, lakini mashamba hayo yamekopewa fedha. Ukienda ukilima, kesho mtu anakuja kupanda zao lake, anakwambia hapa siyo kwako. Sasa kama siyo kwangu, nimekaa miaka 50 hapa siyo kwangu kivipi? Eti kwa sababu ni mtu ambaye ana uwezo. Sasa hawa waganga wa kienyeji wasiokuwa na uwezo watalima wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuangalie, naamini kabisa Serikali ya safari hii ni sikivu. Mawaziri mnafanya kazi nzuri sana nami naendelea kuwapongeza. Ukimwona mtu anamsema vibaya Waziri ana matatizo ya akili, kwa sababu Mawaziri mko wachache na nchi ni kubwa, hamwezi kwenda kila kona kwa muda mfupi. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba, tushirikiane nasi Wabunge hapa wote, usijali itikadi ya mtu; twendeni mkaone mazingira ya Majimbo yetu na mtoe maamuzi kama anavyotoa Mheshimiwa Lukuvi pale kwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niliseme hili, kwa sababu sisi kule Tanga na Mikoa ya Mjini huku tunapata shida sana. Kama tunapata shida sana, hakuna mahali kwa kuongelea masuala haya ila ni hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Waziri wa Barabara ajue kwamba Jimbo langu barabara zote zimefungika, watu wamekaa kwenye visiwa na maji yameingia kwenye nyumba za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali Tukufu hii iende ikaangalie Mkoa wa Tanga ulivyopata mafuriko makubwa. Wabunge usione tumekaa hapa, tumekaa kwa ajili ya kuchangia hoja hii tusije tukaonekana Wabunge wa Mkoa wa Tanga ni watoro. Siyo watoro lakini kwetu huko kumeingiliwa, hakuna

mahali kwa kuwatetea Waheshimiwa Wakulima wetu, pamoja na Wajumbe wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu awasaidie sana na amsaidie sana Spika wa Bunge hili kwa kazi nzuri aliyotufanyia safari hii. Meza tunayokaa utafikiri tupo Ulaya, kumbe tupo Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, lakini umesahau kusemea Ruvu, Muruwazi. Anayefuata ni Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**KATIBU MEZANI:** Ameomba kesho.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Anayefuata ni Mheshimiwa Salma Mwassa, hayupo. Haya, tunaendelea, anayefuata ni Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, karibu!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naomba nitoe sehemu ya mchango wangu kwenye Mpango huu. Kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa mchango wake wa kuitetea nchi hii katika kufanikisha azma nzima ya kuwaletea maendeleo Watanzania wote. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tumwombee aweze kufanya kazi hii na tuweze kusogea kutoka hatua hii tuliyonayo tuweze kwenda mbele. *(Makofi)*

Pili, nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi kubwa wanayofanya. Nawaalika njooni Mbulu, msinitafute mimi, nendeni Mbulu. Mnahitajika sana. Mbulu tuna mahitaji makubwa, tuna kero nyingi. Nakupongeza sana Mheshimiwa Lukuvi kwa jinsi ulivyoshughulikia suala lililokaa miaka 10, sasa limetatuliwa, Wanambulu wana amani, wanakuombea. Waheshimiwa Mawaziri wengine baada ya Mkutano huu tunawaomba njooni Mbulu mtusaidie kwa jinsi ambavyo tuna matatizo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuungana pia na Waheshimiwa Wabunge wote na kuwashukuru kwa jinsi walivyochangia Mpang huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tusimamie mapato. Azma nzima ya Rais wetu kusema Tanzania inastahili kusaidia siyo kusaidiwa, ni ya kweli kabisa. Tusimamie mapato, tusimamie huu Mpango, ifike mahali Mpango huu uletwe tena mbele yetu, tuujadili jinsi ambavyo unahitaji kurekebishwa na kuondoa dosari zinazokinzana na mafanikio ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mpango wowote unapoletwa mbele ya Bunge hili tukiujadili, tukaupitisha, baadaye ukirejeshwa tunaweza kufanya marekebisho yanayohitajika katika Mpango kwa kufanyia utafiti kupitia kwa wataalam wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kulizungumzia ni mahitaji makubwa ya wananchi kuliko uwezo wa Serikali. Hii itaondolewa pale ambapo mahitaji makubwa yanatokea ya kutazama tena upya Mpango huu ili uweze kuleta tija katika huduma za umma na sehemu mbalimbali kwa jinsi ambavyo umewasilishwa kwetu na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana Waziri wa Fedha na wadau wote waliohangaikia Mpango huu ambapo ni dira ya Taifa letu kwa mmwaka huu katika kuleta maendeleo kwa Watanzania wote. Umuhimu mkubwa wa Mpango huu unamgusa kila mdau hasa yule wa chini. Kwa jinsi ambavyo tunahangaika wakati wote na Bunge letu linahangaika na sisi Wabunge kule Majimboni tumeahidi mambo makubwa sana, rai yangu kwetu sote ni kila mmoja atimize wajibu wake katika Mpango huu na aone ni kwa jinsi gani atahangaikia suala hili ili pengine Mpango huu kwa miaka mitano uweze kutoa matokeo makubwa sana yenye kuweza kufanyiwa kazi hasa katika maeneo yenye changamoto nyingi ambapo kwa namna yoyote ile kila mmoja wetu anastahili kutimiza wajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuone changamoto inayotokana na pato la Taifa kuwa dogo na jinsi ambavyo mahitaji yanakuwa makubwa, mengine yanaingia baada ya mahitaji ya dharura kutokea kama vile mafuriko, baa la njaa na mambo mengine kama magonjwa. Kwa hiyo, tunapopanga mpango tukienda miaka mitano bila kuwa na muda wa tathmini na muda wa kati na muda mrefu wa kuutazama Mpango huu umekinzana na mambo gani katika kufanikisha jambo lile ambalo limetokea na yale yaliyotokea katika Mpango, kwa kweli tunahitaji sana Bunge lipate kutazama upya na vikao vya tathmini vifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia eneo la Mkoa mzima wa Manyara jinsi ambavyo hatuna kiwanda, hatuna reli, hatuna pia miundombinu ya barabara ambazo zinaunganisha mkoa wetu hasa eneo la juu la bonde la ufa ikiwemo Wilaya ya Mbulu na Wilaya nyingine ya Hanang jinsi ambavyo tunahangaika kutafuta namna gani tunaweza tukanufaika na hali hii ya miaka mitano katika kufanikisha azma hii, ambapo kila mwananchi anahitaji afanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, kwa jinsi ambavyo tunahangaika na kwa jinsi ambavyo mahitaji ni makubwa, basi rasilimali zile nyingine za miundombinu zinavyotekelezwa, kwa mfano, miundombinu ya

vyuo, viwanda na miundombinu ya mbalimbali, tupate na sisi tulio pembeni na tulioko juu ya bonde la ufa hasa maeneo magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nalilia barabara ya Mbuyuni - Magara – Mbulu. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na Wizara yake waje Mbulu waone jinsi tunavyoteseka na barabara hiyo ambayo ina jiografia ngumu na wananchi wanapoteza maisha mara nyingi, lakini barabara hiyo na udogo wake, haishughulikiwi. Tunaomba katika hii miaka mitano ufumbuzi wa barabara ile ya Karatu - Mbulu - Haydom na hii ya Mbuyuni – Magara – Mbulu na ile ya Dongobesh - Manyara kule Manyara – Dongobesh - Babati ipate basi namna ya kufanyiwa utatuzi ili wananchi wakae kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa eneo hili unahitaji wadau wakubwa wa maendeleo, tusiisahau sekta kubwa binafsi ambayo ndiyo mhimili unaochochea maendeleo kwa nchi yetu hasa katika viwanda na katika ulipaji wa kodi na jinsi ambavyo Serikali inahitaji mapato ili iweze kutatua changamoto na matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niweze kuzungumza eneo hili kwa kufanya maandalizi ya Wataalam, miundombinu na fedha kwa ujumla katika ushauri wa jumla, lakini tusisahau kutoa nafasi kubwa katika uwekezaji kwa wazawa wa nchi yetu. Eneo hili linahitaji sana Watanzania ambao wataendesha shughuli nzima ya uzalishajii katika Sekta ya Viwanda na sekta mbalimbali ili tuweze kupata manufaa makubwa na Watanzania waweze kumiliki uchumi wa nchi kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta hii binafsi, unahitaji zaidi uchocheaji na uwekezaji katika wale wazawa ambao wanahitaji kufanya hivyo na kufanikiwa katika hali sahihi. Katika eneo hili la kukejeli kutumbua majipu; kutumbua majipu tuendelee kutumbua majipu kwa sababu ndio waliotufikisha katika hii hali ambayo tunakuwa tegemezi sana. Ili tuepukane na utegemezi ni lazima tusimame imara katika kuhakikisha eneo hili tunafanikiwa kwa jinsi ambavyo tunaweza tukaenda mbele katika ile hali ya kudhibiti ubadhirifu, ufisadi, hujuma za nchi na mambo mbalimbali. Kwa ujumla Mheshimiwa Rais ana azma nzima, Wabunge tuwe na azma nzima na Mawaziri mpate nafasi pekee ya kumpa ushirikiano Mheshimiwa Rais wetu ili tuweze kufanikiwa.

Kwa hivyo basi, katika harakati za pamoja, ushirikiano wa jumla unahitajika. Wanaokejeli shughuli za utendaji wa Serikali kwa sasa katika muda huu mfupi ni kama wameanza vibaya. Hatuna sababu yoyote ya kukejeli Serikali, bado ni mapema sana. Safari hii tunayoanza ni ya miaka mitano; tuko ndani ya miezi mitatu, minne, mitano hadi sita, tukianza kukejeli, matokeo yake ni hatujajua chombo hiki kinaendaje na kwa jinsi gani tunahitaji mafanikio na siyo kukejeliana au kukatishana tamaa katika mwelekeo wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa nafasi ya pekee katika Mpango mwingine utakaowasilishwa hapo baadaye, tutazame upya hali ya Watanzania kwa jinsi ambavyo wanahitaji ushuru na kero mbalimbali ya tozo uondolewe kwa Watanzania wadogo. Wafanyabishara wadogo wana wakati mgumu! Tunapohitaji kuwadai ushuru na tozo mbalimbali, wao wanahitaji zaidi waweze kufanya mambo yao ya biashara ndogondogo ili wakue waje kwenye hatua ya wafanyabishara wa kati. Kwa hiyo basi, eneo hili litazamwe, lakini katika ile hali ya kulisaidia kundi hili la walioko chini sana katika maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mkubwa unaotolewa na Mawaziri, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge kwa ujumla, unaweza kuchochea mafanikio makubwa na Mungu akitujaalia katika miaka hii mitano, Tanzania itasonga mbele na itakuwa nchi ya pato la kati na Watanzania wengi watanufaikia mapato ya nchi yao na watafurahia mafanikio ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nachukua hatua za makusudi kabisa za kututaka sisi Wabunge wote bila kujali itikadi; tumetoka kwenye Vyama mbalimbali, Majimbo mbalimbali lakini sisi wote ni Watanzania, tumeletwa na Watanzania katika Ukumbi huu ili tuweze kuzungumzia matatizo ya Watanzania, haijalishi ni wa eneo gani, lakini lengo kubwa ni kwa namna gani tunafanikiwa kutatua matatizo ya Watanzania wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa yote lakini niseme kwa ujumla naomba ushirikiano kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Hata huyu anayekejeli Serikali ataihitaji Serikali hii imhudumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kutumia muda vizuri. Anayefuata ni Mheshimiwa Maftaha Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Waitara Mwita Mikwabe.

**MHE. ABDALLAH N. MAFTAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia mpango huu kwa niaba ya wananchi wa Mtwara Mjini. Nianze tu moja kwa moja kuangazia huu Mpango kwa sababu Mpango kwa kiasi kikubwa unaonesha namna gani nchi yetu sasa hivi inaingia katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la msingi sana ambalo sijaliona katika Mpango huu, ni usimamizi wa hivyo viwanda. Kwa masikitiko makubwa

kabisa, hivi sasa tuna baadhi ya viwanda ambavyo vimejengwa katika nchi yetu na wawekezaji mbalimbali kutoka nje ya nchi. Kwa mfano, ukija pale Mtwara Vijijini kuna Kiwanda kinaitwa Kiwanda cha Dangote, lakini ukiangalia katika kiwanda hiki unaweza kuona kuna changamoto nyingi sana ambazo Serikali imeshindwa kuzisimamia na kuzitatua, lakini tunaleta Mpango ambao unasema kwamba Tanzania itaondoa umaskini kupitia Sekta hii ya Viwanda wakati hivyo viwanda vichache tunashindwa kuvisimamia na kuleta tija kwa wananchi wetu ili kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana, niliweza kuzungumza suala hili katika mwelekeo wa Mpango kwamba Kiwanda cha Dangote kilichopo Mtwara kimeajiri Watanzania ambao wanatoka sehemu mbalimbali ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kuna Makampuni mle matatu ambayo ni ya kigeni yanayosimamia uendeshaji. Ipo Kampuni ya Kichina, kuna Kampuni kutoka India na Kampuni nyingine kutoka kule Nigeria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi kampuni zilizopo katika Kiwanda hiki cha Dangote zinanyanyasa kwa kiasi kikubwa sana wananchi wa Tanzania. Sasa swali langu katika Mpango huu ni kwamba, kama tumetengeneza utaratibu wa kuhakikisha kwamba viwanda vinatatua changamoto za umaskini wakati tunashindwa kusimamia viwanda hivi; na pale nilizungumza katika mwelekeo wa Mpango huu kwamba malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa Tanzania ambao ni wazalendo ni midogo na hata hiyo midogo yenyewe wanapunjwa. Badala ya kulipwa Sh. 12,000/= kwa siku ambazo zinaandikwa kwenye makaratasi, wanapewa Sh. 7,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilizungumza katika mwelekeo wa Mpango hapa Bungeni lakini mpaka leo hii tunapotaka kupitisha huu Mpango, bado marekebisho hayajafanyika katika Kiwanda cha Dangote. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara aunde Tume Maalum iweze kutembelea Kiwanda hiki cha Dangote kwa sababu kinanyanyasa Watanzania walioajiriwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze suala zima la bandari. Kwa mujibu wa mwelekeo wa Mpango huu, umesema tutaboresha uchumi wa nchi kwa kujenga bandari mbalimbali na Mheshimiwa Profesa Maji Marefu kazungumza hapa kwamba, bandari siku zote tunaangalia Bandari ya Dar es Salaam na sasa hivi tunaenda kujenga Bandari mpya ya Bagamoyo wakati Mwenyezi Mungu ametubariki, Mtwara tuna bandari ambayo ina kina kirefu Afrika Mashariki na Kati, Bandari ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia wala haihitaji kuchimba, lakini tunaenda kujenga bandari mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa, wakati Serikali hii ina mpango wa kuhakikisha kwamba inabana matumizi, lakini tunaenda kujenga bandari mpya ambayo itatumia Dola za Marekani bilioni karibu 22.5, wakati Bandari ya Mtwara ambayo Mwenyezi Mungu ametubariki ilikuwa ni kuboresha tu kidogo na iweze kutumika kuinua uchumi wa nchi hii. Sasa mipango hii, ni kweli lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunaondoka hapa tulipo ili kuwa na maendeleo ya nchi hii wakati tunatumia pesa bila mpango ambao kimsingi unastahiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, kama kweli tunahitaji kuboresha uchumi wa nchi hii, tuboreshe Bandari za Mtwara, tuboreshe Mtwara *Corridor,* tuboreshe Tanga na maeneo mengine. Tusifikirie tu Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala zima la elimu. Sasa hivi tunasema kwamba Serikali imeweka sera ya kutoa elimu bure, lakini kwa masikitiko makubwa kabisa, ukitembelea mashuleni huko, hii sera ya elimu bure imekuja kudumaza usimamizi wa elimu. Tunaangalia fedha za uendeshaji wa hizi shule, kwa mfano, Shule za Msingi; nilitembelea baadhi ya shule kama tano, sita pale Mtwara Mjini katika Jimbo langu, ukipitia fedha zilizoingia shuleni kwa miezi hii mitatu, ni jambo la kusikitisha sana. Kwa mwezi Sh. 27,000/= pesa za maendeleo halafu tunasema kwamba tunahitaji kuinua elimu kwa Sera ya Elimu Bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kwa namna ya kipekee kabisa, Serikali iweke utaratibu wa kupeleka fedha mashuleni kama kweli tunahitaji kusimamia elimu na elimu ndiyo chachu ya maendeleo katika dira ya nchi yoyote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa kifupi kilimo na uvuvi. Mpango huu umeelekeza kwamba tutainua kilimo kwa kuboresha mazao ya biashara na mazao ya chakula kwa wakulima, lakini nikizungumzia kwa mfano suala zima la zao la korosho Tanzania, tuna Bodi ya Korosho Tanzania, Bodi ambayo inasimamia Sekta hii ya Korosho Tanzania, lakini kwa masikitiko makubwa kabisa, hawana mkakati hata mmoja kuhakikisha kwamba huyu mkulima anayelima zao la korosho anapewa pesa ambazo zinastahiki pale anapouza mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu kabisa, ukiangalia katika uuzaji wa mazao haya, zao la korosho kwa mfano, mkulima amewekewa tozo nyingi sana, mpaka tozo ya gunia ambalo Mhindi anakuja kusafirishia korosho kutoka Tanzania kwenda India anabebeshwa mkulima, halafu tunasema tunahitaji kuinua kilimo wakati mpaka leo tunavyozungumza bado bei ya korosho iko chini sana. Korosho inauzwa Sh. 1,800/= hadi Sh. 2,000/=. Ni jambo la kusikitisha kwamba Serikali inashindwa kumtafutia mkulima masoko ya zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho ni zao ambalo mwaka 2015 na mwaka 2014 limeingiza pesa nyingi Serikalini. Ukiondoa tumbaku, zao linalofuata ni korosho, lakini tunashindwa kuweka mikakati ya uhakikisha kwamba tunainua zao hili na mkulima anaweza kunufaika na kilimo hiki cha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mungu ametubariki Tanzania tuna Bahari ya Hindi kuanzia kule Mtwara mpaka Tanga, lakini cha ajabu ni kwamba Serikali katika Mpango huu sijaona kwamba imeweka utaratibu kuona inaboresha namna gani Wavuvi wetu wa Tanzania ili waweze kununuliwa vifaa, kupewa vifaa vya kisasa vya uvuvi ili waweze kuwa na uvuvi wenye tija na mwisho wa siku waweze kuondokana na umaskini. Leo tunakuja tunasema tunataka kuboresha kilimo na uvuvi wakati mipango yetu haioneshi namna gani tunaweza kuondoa umaskini kupitia Sekta hii ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazungu wanasema kwamba Tanzania Mungu ametubariki na hasa upande huu wa Kusini, tunasema ni *vision sea*, ni bahari ambayo ina samaki kedekede huko chini lakini Serikali haina mpango wowote wa kuinua Sekta hii ya Uvuvi ili Watanzania tuweze kuondokana na umaskini. Tunapiga danadana tu! Ooh, tutajenga Chuo cha Mikindani, wakati hatuna utaratibu, hatujaweka mkakati wowote wa kuhakikisha kwamba tunanunua maboti na vifaa vya uvuvi ili tuweze kuwasaidia wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo suala zima la maendeleo. Maendeleo yoyote yanategemea amani na utulivu wa nchi, lakini kwa masikitiko makubwa kabisa, kwa mfano ukija Mtwara Mjini tangu mwaka 2013, 2014 mpaka leo hii 2015, Serikali iliweza kuchukua ardhi ya wananchi, maeneo ya Tanga na maeneo ya Mji mwema. Nimezungumza hili jana hapa kwenye *briefing* na hii ni mara yangu ya tatu nazungumza; Mtwara kuna mgogoro mkubwa sana wa ardhi. Wananchi wamenyang'anywa ardhi zao na Serikali wakasema kwamba wataenda kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 2013 mpaka leo hii, hakuna senti yoyote iliyotolewa na Serikali. Cha ajabu Serikali ukiiuliza, inasema tutafanya, tutafanya. Wananchi hawana sehemu za kulima, halafu tunakuja na Mpango wa kusema kwamba eti tunataka kuondoa umaskini Tanzania, wakati wananchi wananyang'anywa ardhi na hawapewi fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu, kwa sababu Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi yupo hapa, atembelee Mtwara, akaangalie changamoto za ardhi ambazo zinaelekea sasa kuleta mpasuko wa Kitaifa na mtengamano wa Kitaifa kwa sababu wananchi wanasema tutafika wakati tumechoka na mwelekeo huu utakuwa hauna maana,

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la amani na utulivu ni jambo la msingi sana. Kama tunahitaji kweli kuhakikisha tunaleta tija katika Taifa hili, umaskini unaondoka, ni lazima tuvutie uwekezaji. Huwezi kuvutia uwekezaji kama hakuna amani na utulivu. *Issue* ya Zanzibar nayo ni ya msingi sana, siyo *issue* ya kubeza. Tunahitaji kukaa pamoja ili kujadiliana namna gani tunaweza kuleta amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Mikataba ya Tanzania, kwa mfano Mikataba ya Uwekezaji, mingi haina tija katika Taifa hili. Kwa mfano, kuna Mkataba wa Mlimani *City*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliingia mkataba na Mwekezaji kutoka Botswana, Mkataba ambao kimsingi Serikali ya Tanzania inakusanya kwa mwaka asilimia 10% tu ya mapato yanayopatikana pale, wakati kuna mamilioni mengi ya pesa yanakwenda kwa Mwekezaji. Kwa hiyo, tunahitaji sasa kama Taifa tuingie kwenye Mikataba na huu Mpango uoneshe ni namna gani Bunge linaweza kupitisha Mikataba yote ya Tanzania ili tuweze kuwa na uwekezaji wenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze angalau kwa kifupi suala zima la afya. Afya ni jambo la msingi sana. Hatuwezi kusema kwamba tunahitaji maendeleo kama Watanzania wengi wanakufa kwa sababu ya afya. Ukija Mikoa ya Kusini, nilizungumza hili wakati wa kikao cha pili kwamba Kanda zote Tanzania tayari zimekamilika kuwa na Hospitali za Rufaa. Kanda ya Kusini mpaka hivi sasa, ujenzi wa Hospitali hii, jengo moja tu, unasuasua ambalo Mheshimiwa Waziri hapa alizungumza kwenye Bunge lako Tukufu kwamba iko katika hatua za umaliziaji ujenzi wa *OPD,* lakini mpaka hivi sasa ujenzi huo unasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hospitali ya Mkoa ya Mtwara hakuna *X-Ray*, Hospitali ya Wilaya hakuna *X-Ray,* halafu leo tunasema tunataka kuondoa umaskini, tunapitisha Mpango huu. Naomba kwa namna ya kipekee kabisa, kama kweli tunahitaji kuondoa umaskini Tanzania, ni lazima tujali afya za Watanzania, ni lazima tuboreshe afya za Watanzania, tuhakikishe kwamba vifaa tiba vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako. Anayefuata kama nilivyosema, Mheshimiwa Waitara, Mbunge wetu wa Ukonga.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ili na mimi nichangie, lakini kabla sijachangia naipongeza Ofisi ya Bunge kupitia Katibu wa Bunge kwa kitendo cha kuiwezesha Ofisi ya Mbunge wa Ukonga kuwa na fenicha. Kwanza ameonesha uzalendo kwa kuwa fenicha

zenyewe zinatengezwa pale Ukonga kwenye Jimbo langu, vilevile kwa kutengeneza mahusiano akaanzia kwangu, hivyo nawapongeza sana waendelee na moyo huo. Nawashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, sitaunga hoja kama CCM, kwa sababu wanaunga mapema halafu asilimia 95.5 wanalalamika! Huu mtindo haupaswi kuwa *entertained* kwenye Bunge, mimi nitaenda tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshauri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, taarifa ya Upinzani Bungeni imempa maswali wala asiyabeze ni mambo ya msingi kweli, kwa rekodi tu nataka nikumbushe mambo machache ambayo nataka ayazingatie kama atapenda, maana yake anaweza akakaidi tu.

Kwa mfano, nchi hii inataka kuwa nchi ya viwanda, lakini Watanzania wanataka kuhakikishiwa na Serikali hii, mimi siiti Serikali Tukufu sasa Mungu atakuwa nani! Wanasema hivi viwanda vilikuwepo……

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Hiyo kengele ni ya mtu mwingine wewe endelea tu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako hivi vitu vinachanganya hapa.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Naomba unilinde, hizi kengele na kelele uzuie kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa inaonesha kwamba viwanda viliuzwa, sasa wakati tunaenda kuleta huu Mpango ambao ni mzuri sana kwa Watanzania, lazima Watanzania wahakikishiwe tukianzisha havitauzwa tena, kutolewa bure au kugawanywa kama shamba la bibi? Hilo ni jambo la msingi kabla ya kwenda kwenye mpango wenyewe, hatuwezi kuweka hela mahali ambapo anaweza akaja mtu mwingine hapa, hapa Mheshimiwa Magufuli amekuja na habari ya viwanda, anaweza akaja mwingine na ajenda zake akaanza kuvigawa tena bure, unakuta nchi inapiga *marktime*. Sheria inasema nini juu ya hayo mambo ambayo yamefanyika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelalamika sana, watu waligawana viwanda, waliovunja utaratibu hawajashughulikiwa, hawajawajibishwa, hakuna mtu yupo Mahakamani, tunaleta mpango mwingine! Sasa nadhani hili jambo ni muhimu sana likazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kwenye ukurasa wa tatu, napitia ile taarifa ya Upinzani, wamesema fedha zilizotolewa ni asilimia 26, ni muhimu Waziri akatuonesha kama mipango iliyopangwa ilikamilika kwa asilimia 26 kwa eneo hili, hivi hizi zilizobaki asilimia takriban 74 amekuja na miujiza gani tena mingine mipya ambayo itawasaidia ili iweze kuwa *sustainable*, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote iliyopangwa haikuzidi nusu tangu imeanza kuzungumza Serikali hii mpya ya CCM sababu haya ni majina tu, alikuwepo Mheshimiwa Nyerere, amekuja Mheshimiwa Mwinyi amekuja Mheshimiwa Kikwete, sasa ni Mheshimiwa Magufuli. Sasa haya ni majina tu lakini Serikali ya Chama kilekile asilimia 60 ya mipango ya maendeleo haijawahi kufikiwa nchi hii .

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani mambo haya yangetusaidia kwa mfano, yametajwa hapa mambo ya msingi kabisa kwamba Deni la Taifa limeongezeka, nimejaribu kugawa hapa hizi trillion 41536.6 ni kama takriban 923,000 kwa kila Mtanzania hata aliyezaliwa leo, ambazo kama Taifa tunadaiwa katika nchi hii. Sasa nataka kujua, deni likiwa kubwa namna hii athari yake kiuchumi ikoje na watu wategemee nini? Maana tunadaiwa hapa tulipo kila mtu sh. 923,000 kwa mahesabu yaliyotajwa hapa, sasa nikasema haya mambo ni muhimu sana kuyazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye rasimu ya Mheshimiwa Warioba haya mambo yangeweza kujibiwa, sasa mkachakachua Waheshimiwa ndugu zangu CCM mkaleta mambo yenu, figisu figisu nyingi, mkapindisha haya mambo. Ile rasimu ilikuwa inaelekeza ili Taifa likope, ili hiyo hoja ije Bunge lijadili, liruhusu ili tuelezwe unakopa, haya maswali ambayo Mheshimiwa Silinde kwa niaba yetu, anauliza, uliweka dhamana ya nini, mlifanyia kitu gani, mipango ikoje, nani alikopa, vitu vya namna hiyo vingeweza kujibiwa sasa ile rasimu mmeichakachua, sisi Katiba hatuna, haya mambo yangeweza kujibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye hoja hizi ambazo zimezungumzwa. Miundombinu; tumezungumza hapa, mimi nilipo ni karibu na uwanja wa ndege, nitaomba Waziri mwenye dhamana na eneo hili anisaidie, uwanja wa ndege unajengwa *terminal III*, lakini taarifa ambazo ninazo *phase one* walikuwa na mkataba, *phase two* wanaendelea hawana mkataba eneo lile, lakini unazungumza kutengeneza miundombinu, tuimarishe uwanja wa ndege, lakini wako wananchi pale Kipawa walihamishwa kutoka pale wakapelekwa Kata ya Buyuni na Chanika, kuna ugomvi mkubwa wananchi wale hawajawahi kulipwa mpaka leo. Serikali imechukua watu imewahamisha kutoka eneo la Kipawa ikawapeleka Buyuni wakaenda kuwakabidhi maeneo ya watu, hakuna fidia. Kwa hiyo, aliyekabidhiwa eneo hawezi kujenga kwa sababu mwenye eneo hajalipwa, hivyo kuna mgogoro mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tunapoandaa mipango hii tusitengeneze matatizo kwa wananchi. Unawekeza eneo, unaweka watu pale wanafanya biashara zao lakini wananchi wako wanaishia kulia na kulalamika watu wana makabrasha mezani yamejaa, kesi nyingi na hawajui wazipeleke sehemu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyekiti Lukuvi amelipokea hili, nadhani na yeye kama ataendelea hivi atakuwa mzuri, angalau amesikiliza, ametoa taarifa ameleta ramani ya maeneo yale angalau uweze kuonesha maeneo ya wazi na maendeleo yaweze kwenda vizuri. Sasa hilo ni kwenye uwanja wa ndege, lakini kuna Mheshimiwa mmoja hapa amezungumza habari ya Dar es Salaam kwamba hakuna wakulima, siyo kweli! Zile hela zije.

Mimi ni Mbunge wa Jimbo la Ukonga nawakilisha Kata ya Kivule, Kata ya Kitunda, kata ya Mzinga, Msongola, Uwanja wa Nyani, Ukwende, Zingiziwa kuna maeneo watu wana mashamba makubwa wanalima mihogo na hata Wabunge wote mnaokaa Dar es Salaam mboga nyingi zinatoka Jimbo la Ukonga ziko safi kabisa. Kwa hiyo kuboresha huduma hii siyo dhambi watu wasibeze hapa, kama mtu anaomba huduma kwenye Jimbo lake asibeze Majimbo ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme. Ni kweli kwamba tunahitaji viwanda lakini Dar es Salaam pale maeneo mengi ni giza. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana anachukua hatua lakini kama hata Dar es Salalam ambako hawa Wawekezaji wanapita watu wetu ni giza, umeme ni wa kusuasua mpaka leo tunapozungumza, yaani kuna watu wanakaa pale kama wanakaa kijijini halafu unazungumza habari ya viwanda, umeme wa kawaida wa majumbani hautoshelezi, viwanda itakuwaje? Yaani umeme wa kawaida tu haujitoshelezi viwanda inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huwezi kuwa na viwanda, huna umeme, mazao ya kilimo na mifugo. Kuna watu wamekataa tamaa, wamezungumza wenzangu wa Mtwara, hata kule Tarime ukienda watu wa kahawa, wananchi wamefyeka mashamba, wengine wanaenda kulima zile bangi ambazo mmesikia watu wamesema na mirungi, wameweka tumbaku haina kiwanda, hamna usaidizi sasa lazima mje na mbinu Mheshimiwa Waziri ya kuonesha watu waliokata tamaa kulima mazao ya biashara kwamba soko lipo na bei itakuwa ni nzuri na makato na manyanyaso mengi ambayo yapo yataondolewa, maeneo yale hata ile kahawa na mahindi, wapo watu ma-*settler* wachache ambao ndiyo wanamiliki soko pale. Wanapanga bei, pembejeo zile zikienda kwenye Halmashauri wanagawana, kwa hiyo, kuna ulanguzi wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makandokando haya yangeweza kurekebishwa, angalau Watanzania mnapozungumza habari ya viwanda, watu wanakwenda njia imenyooka, vizingiti vimeondoka, ubaguzi pale hakuna, mambo ya namna hiyo yangetakiwa yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Ukonga, Ukonga kuna viwanda vya chakula cha kuku, lakini mayai yanapatikana na kuku wa nyama wa kisasa, lakini kule hakuna kiwanda cha kutotoa vifaranga rasmi**.** Vifaranga vingi vinatoka nje ya nchi na baadhi ya *material* inatoka nje ya nchi. Sasa wananchi wale wanachukua vifaranga wanawekeza, mtu amedunduliza, mama lishe, kijana wa boda boda  pamoja na kupata shida mjini hapa, kukamatwa kamatwa sana, lakini akipata kidogo anawekeza kuku wake 200, 500, wakikua baada ya miezi miwili, mitatu, minne kuku wote wanakufa, ukienda kuulizia unaambiwa kwamba shida ilikuwa ni kiwandani vifaranga vilikuwa na shida ambavyo hatuna viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mambo kama haya pamoja na kwamba tunawekeza tuone ubora wa mali ambayo inaletwa ili watu wetu wasiingizwe kwenye umaskini ambao kwa kweli tunajitengenezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dar es Salaam kwenye biashara kuna habari inaitwa *DECI* na Malingumu, kwamba watu walikuwa wanapanda pesa. Nimesikia Watanzania wote hapa na Wabunge mnafahamu, yaani pesa ikawa miujiza ya Mungu kwamba pesa unaweza ukapanda ikaota kama uyoga, ikazaa mara mbili, tatu na watu wakavuna na Mawaziri wa Serikali hii ya CCM walishiriki zoezi hili na wakataja maeneo kesi ikaenda Mahakamani. Mpaka leo wananchi wale wanasubiri malipo wamekuwa maskini, wameuziwa nyumba zao.  Kwa kweli mnapozungumzia Mpango Mheshimiwa Waziri ungejua hali iliyoko hiyo ungeenda sijui kujifungia wapi kama ni Mungu akutembelee upate miujiza uje na mipango ambayo inatekelezeka. Hizi ni kero ambazo zinaumiza wananchi wale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afya; sasa mmetangaza kwamba kuna, kwa mfano, mimi kule Ukonga, jana nimejibiwa swali langu na Mheshimiwa nimesikitika majibu, Jimbo la Ukonga na Segerea tunategemea hospitali ya Amana. Tumesema tujenge pale hospitali, Halmashauri imetenga kwa mwaka bilioni moja au milioni 900, hiyo hospitali itagharimu zaidi ya bilioni 600 kwa mpango uliopo, maana Waziri alisoma alichofanya hapa na ndicho mmefanya kuzuia *TBC* isioneshe na *TV* zingine watu wasione, watu wa Ukonga walikuwa wanalia. Waziri ametuma mtu hapa ameenda akachukua ame-*copy* na ku-*paste* ambacho tulipitisha Manispaa ya Ilala hakuongeza kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana kwa mpango ule ile hospitali itajengwa kwa miaka 26, nimewaambia ile Wilaya kama mpango wenyewe ni

ule, ile fedha tuifanyie re*allocation,* utajenga magofu fedha itapotea haiwezi kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuwa na viwanda, watumishi wetu hawa ni maskini hawana afya, unafanyaje? Mkienda kwenye viwanda vyenyewe, malipo pale pale Gongo la Mboto kuna Kiwanda cha Namela, mwenye kiwanda anawalipa watu wale sh. 4,000/= ambayo imetajwa hapa ndiyo posho ya kufanya kazi. Katika hali ya kawaida Mheshimiwa Waziri, wewe ni mtaalam wa mambo ya *finance*, hivi sh. 4,000/= Dar es Salaam utaishi kweli? Ndiyo mpango uliopo na Sheria imesema l50,000/= kwenye viwanda. Kwa hiyo, kuna mianya mnatoa wale wawekezaji wakija kwa nia njema tunawapa *support*, wamechukua ardhi yetu, nguvu kazi ya kwetu, tuna wataalam wanalipwa kidogo sana, lakini mwisho wa siku watatunyonya kweli kweli, sasa mikakati kama hii na mambo haya yangetakiwa yapangiliwe vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli litakuwa jambo langu la mwisho. Reli inayozungumzwa hapa tunahitaji pale Ukonga, huduma ya *TAZARA* na reli ya Kati kwa maana ya kusafirisha kupunguza misongamano, sasa hili jambo likifanyika itatusaidia.

Nimeona kwenye Mpango imeonekana, sasa shida ni kwamba na kwa ujumla haya makaratasi ukisoma uko chumbani unafurahi kweli kweli, nendeni mahali sasa myaondoe yaende kwenye vitendo ndiyo mahitaji! Shida ya nchi hii siyo mipango, shida ni kwamba mlichokiandika kiwe *transformed* kwenye *actions,* watu waone *actions* zote zimefanyika, barabara za lami zimetajwa, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Rais ametaja barabara ya Kitunda – Kivule - Msongola mara nne zote akiwa Bungeni hapa sasa imetajwa tena akiwa Rais nataka nishuhudie kama Rais atakuwa mwongo tena, maana yake kama alikuwa ananyimwa hela kugawiwa sasa hivi anagawa mwenyewe, anatumbua majipu na anafanya *reallocation* nataka tushuhudie mambo haya, ni matarajio ya Wabunge wengi kwamba mipango mliyoileta hapa inatekelezeka.

Halafu Wabunge wa CCM muache kupiga makofi sana huku, mnaunga mkono mwanzo halafu mnalalamika mwanzo mwisho hivi utawala bora unakujaje? Hivi ninyi Viongozi, Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa mnazima *TV*, mpango mzuri, maneno mengi na majibu mazuri ya Upinzani ya Mheshimwa Silinde hayajaonwa na Watanzania, hoja zetu hazisikilizwi, tuko hapa gizani kama wachawi humu ndani. Watu wamenywea humu ndani, humu ndani hamtaki watu waone kwa nini? Hivi ninyi nani amewaroga! Nani amewaroga? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia hii ya sasa hivi Serikali inakaa kabisa inafunga Vyombo vya Habari, mlisema *TV* yenu ni gharama siyo? Hizi za watu

binafsi zinawahusu nini? Mmeombwa hela? Haki ya Mungu nimesikitika sana, yaani watu wazima, Mawaziri kabisa mnakubali kwenda kuwazuia Watanzania, Ibara ya ndani ya Katiba ya nchi mnaivunja hivi ya haki ya kupata taarifa. Gharama mmesema ni bilioni…! hiyo *TBC* fungeni ni chombo chenu cha uenezi, endeleeni na mambo yenu, watu binafsi waruhusiwe humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii nchi imekuwa giza tunaongea hapa yaani mwende mchuje, mrekodi muweke mnayotaka ninyi halafu mtuletee tufurahie, halafu mnatuambia habari ya elimu hapa, mnatuambia mambo ya TEHAMA, humu mmeweka mambo ya TEHAMA, sasa TEHAMA maana yake nini? TEHAMA maana yake ni eti watu wafanye kazi, yaani mchukue viboko muwapige watu ambao hawaendi shamba sasa, kawatandike watu ambao hawaendi shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mtu amemwajiri mtu mzembe anaangalia *TV* ofisini kwake amfukuze kazi.

**MWENYEKITI**: Ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Nataka nipate majibu.

**MWENYEKITI**: Ahsante umesikika, anayefuata ni Mheshimiwa Mussa Zungu, Ilala.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kusema kuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze jitihada za Serikali na za Rais katika kuitakia neema nchi yetu, nimpongeze Waziri na Serikali kwa ujumla. Mimi nitajikita sehemu moja tu, sehemu ya mapato na hasa nitajikita kwenye sehemu ya makampuni ya simu nchini mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo tu, ukichukua watu milioni 10 kwa mwezi, katika hawa kila mmoja wao akitia vocha sh. 1500 kwa wiki, natumia kiwango cha chini sana, sh. 1500 kwa wiki, kodi ya Serikali ni sh. 450 kwa watu milioni 10. Kwa wiki hiyo ni bilioni nne na milioni mia tano, kwa wiki nne kwa sh. 6,000 tu ambazo anachangia yeye kwa kupiga simu kwa mwezi, Serikali inakosa bilioni 216. Pesa hizi zinakwenda kwenye Makampuni ya Simu, pesa hizi hazirudi Serikalini kwenye *excise duty* na *VAT* ya 30%. Mfano mdogo, ukinunua *bundle* ya sh. 20,000/= unapewa *package* ya shilingi 19,000/=, sasa najiuliza *VAT* na *excise duty* ya Serikali inakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaelekea pesa za Serikali zinatumika kunufaisha makampuni haya, huku Serikali yenyewe haipati kitu. Udhaifu upo kwa *regulator*. *Regulator* anatakiwa aingie katika mitambo ya makampuni haya ajue namna gani kodi ya Serikali inapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wanalipa 10,000/= kwa mwezi, 10,000/= kwa mwezi kodi ya Serikali ni shilingi 3000/=, kwa mwaka ni bilioni 360 zinaondoka, hakuna mtu anaye-*monitor* pesa hizi. Makampuni ya Simu wanapolipa kodi zao hawaweki *separation* za aina za kodi, *corporate tax*, *VAT*, *excise duty* na kodi zingine zote wanaziweka pamoja wanasema tunalipa bilioni 100, bilioni 50, lakini kuna pesa nyingi za Serikali zinapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka majibu, tunataka watu wa *TCRA* na Waziri wa Fedha yuko hapa, haya tumeyasema miaka yote, mwaka huu tunamwambia mwenyewe Mheshimiwa Rais, udhaifu ambao upo kwenye kukusanya mapato ya Serikali kwenye Makampuni ya Simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Management fee* three *percent*, matangazo ya makampuni haya ya simu yanapewa mpaka asilimia10 ya mapato yao. Kwa hiyo, kama kampuni inachukua asilimia10 kama kampuni inatangaza mapato yake kwa mwaka mathalani bilioni 100, bilioni 10 inakwenda kwenye matangazo. Matangazo yapi ya kwenda nchi hii kwa bilioni 10 kwa kampuni moja? Nataka nipate maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la *frequency* za *4G*, nataka Serikali iniambie nchi nyingi duniani *4G* ambayo ni *long term evolution*, baada ya hii *4G* sasa hivi itachukua miaka mingi sana kuleta mtandao huu wa *4G*. Wenzetu wanapiga mnada, wanampa mtu mmoja, yeye ndiye anawapa wengine, anapewa mnada, Waingereza wanauza *4G* mpaka milioni *300 pound, 600 billion*. Nchi ya jirani hapa walijaribu jaribu wakapata bilioni 110, nataka kujua *TCRA* masafa haya wanampa nani na wanapata nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mtambo wa *Call Accounting System*, tunataka kuwa na *forensic audit* ya mtambo huu tujue unafanya kazi vipi. Haiwezekani wenye Makampuni ya Simu wanakuwa na ujanja zaidi ya mtambo huu na katika lugha ya kitaalam wanasema *garbage in, garbage out*, anaye-*feed* mtambo huu tunataka atueleze anafuatilia vipi mapato ya Makampuni haya ya Simu. Nchi yetu ina uwezo wa kukusanya mapato makubwa sana kwenye Makampuni ya Simu kama *regulator TCRA* atafanya kazi yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti mapato ya Serikali na hasa nazungumzia *VAT* na *excise duty,* lazima sasa *TCRA* waweke utaratibu. Makampuni haya ya Simu sasa waweke *software system* ndani ya mashine zao,

ili wakati mtu ana- *top up* simu yake, ukiweka 10,000 kwenye simu yako, pale pale mashine ya simu yako ifanye kazi kama *EFD* ioneshe asilimia 30 ya Serikali. Hii ndiyo njia peke yake ya kudhibiti wizi unaofanywa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiweka sh. 10,000 na simu ikakuambia sh. 3,000 ya Serikali, sh. 7000 yako na *operator* kila mtu atajiona ufahari namna gani anachangia pato Serikalini. Hili kama halikufanywa tunamwambia tena Mheshimiwa Rais, hili ni jipu. Tunapoteza mapato mengi sana, *TRA* wanashindwa kudhibiti pato hili, *TCRA* wenyewe wanashindwa kudhibiti pato hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri wa Fedha yuko hapa tena huyu Waziri wa fedha tulikuwa naye kwenye Kamati ya Kodi, haya yote tuliyasema wakati akiwa mshauri wa uchumi, Ofisi ya Rais, sasa umeingia hapa Mzee, fanya hii kazi naomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa wazo hapa kwenye Bunge Januari mwaka huu kuhusu sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi nchi ya jirani inakusanya kodi pato la Serikali trilioni nane, daladala hizi, bodaboda hizi, wafanyabiashara wadogo wadogo wote hawa walelewe, najua haitawezekana kwa mwaka mmoja, jibu lililotolewa hapa na wataalam ni bughudha kwenda kukusanya hela hizi, ni bughudha kwenda kukusanya trilioni nane? Wakati nchi inahitaji mapato?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watendaji wa Serikali wana tabia ya kuwa na uvivu kwenye kukusanya hizi pesa. Naomba Waziri wa fedha yuko hapa na Waziri wa Mawasiliano, Naibu nafikiri yuko hapa, tujaribu na tufanye tu-*embark* na *process* hii ya ku-*collect revenue* kwa kiwango kikubwa ili nchi hii isiingizwe mkenge kama ilivyoingizwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo hii ya kuweza kuthibiti mambo haya ipo *TCRA* wanajua ipo, tatizo linakuja ni *willingness* ya kutaka kufanya shughuli kama hii. Kwa hiyo, mimi sina mchango mkubwa sana, nimezungumzia *4G*, nimezungumzia mapato, nimezungumzia na kipato cha *display* ya 30% ya Serikali ioneshwe kwenye simu zetu ili tujue mchango ambao Serikali inapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itawafanya *TRA* wala wasipate tabu, wanakwenda tu kwenye *system* ya *EFD* wanajua kila siku tunapata shilingi ngapi kwenye 30%. Udhibiti wa *credit card* tuelezwe, udhibiti wa hizi *credit card* uko vipi, *consignment* ikiingia inatolewa bandarini au *airport* kama mzigo au inatolewa kama *value* ya *airtime* inaingizwa nchini, *TRA* inatakiwa sasa ijue kama *consignment* imeingia bilioni tano, asilimia 30 ya bilioni tano tayari ni fedha ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumai leo nasema suala hili nafikiri labda ni mara ya saba au nane toka niingie kwenye Ubunge, sijaona mabadiliko yoyote. Natumaini sasa leo pamoja na Serikali hii na Rais wetu huyu, haya mambo sasa yafanywe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru kwa mchango wako, anayefuata ni Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kuchangia Mpango huu wa Miaka Mitano na Mpango huu wa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na elimu; ukiangalia Mpango huu umejikita zaidi kwenye mambo ya viwanda ili kubadilisha uchumi wa Taifa letu na maisha ya wananchi wa Tanzania. Nilikuwa najaribu kupitia mpango wote kwenye suala la elimu sijaona kama tumewekeza vya kutosha kwenye suala la elimu. Ninapoongelea suala la elimu, elimu inayoendana na viwanda tumewekeza kwa kiasi gani, Mpango huu umetaja kiwango gani, kiasi gani cha pesa ambazo tumeziwekeza kwenye *vocational training.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukulia kwa mfano Mkoa wa Mara, ndiyo Mkoa ambao umetoa Kiongozi mkubwa katika Taifa hili, ambaye ndiye amesababisha na ninyi mmekaa kwenye hivyo viti vya mbele hapo, Mwalimu Nyerere. Mkoa wa Mara hauna Chuo cha *VETA* hata kimoja, hauna Chuo Kikuu hata kimoja, Mkoa wa Mara watu wake ni maskini kweli, hakuna kiwanda cha kueleweka, Mkoa wa Mara hauna hospitali ya Wilaya, iko shida kweli kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashindwa kuelewa vizuri kwamba nilivyokuwa nasikia Tanzania ya Magufuli itakuwa ni nchi ya viwanda nilitegemea nitaona humu fedha za kujenga viwanda, sijaona! Sasa sijui ni viwanda vya namna gani maana nilitegemea Mkoa wa Mara tutapata pale kiwanda, vijana wetu watapata ajira, kumbe hamna ni blah, blah tupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi mmesema elimu bure 20,000/= sekondari, lakini wanaojenga madarasa ni wazazi, hawa wananchi wetu maskini ndiyo wanajenga madarasa, ndiyo wanajenga shule, asilimia 90 ya shule zinaendeshwa na wazazi, wewe umesema umeondoa 20,000/=. Iko hivi, wewe chukua asilimia 90 jenga madarasa, peleka madawati, acha wazazi walipe hiyo 20,000/=, hapo tutakuelewa lakini kama wazazi ndiyo wajenge madarasa wapeleke madawati, msiwadanganye Watanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Serengeti, ni Mbunge wa Jimbo la Serengeti, Jimbo ambalo kwa miaka mingi limeongozwa na CCM lakini hakuna hata kipisi kimoja cha lami, hata mita moja ya lami hakuna, hospitali ya Wilaya hakuna, Wilaya ya Serengeti kuna wengine hawajui iko Mkoa gani, iko Mkoa wa Mara! Nimeangalia hapa hata kwenye miundombinu ya barabara wanasema mikoa yote imeunganishwa na barabara ya lami, nikajiuliza hivi Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha umeunganishwa na barabara ya lami, barabara aliyoiasisi Mwalimu Nyerere ya kupita Butiama kwenda Arusha mpaka leo, Mheshimiwa Magufuli alikuwa Waziri wa mambo ya barabara, hata mwaka jana hakuja kuomba kura Serengeti maana barabara haijapita pale, lakini walimpa kura nyingi kuliko Lowassa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimpa kura nyingi eeh! walimpa kura nyingi wanataka kumpima waone kwamba uaminifu walioufanya kwake je, yeye atakuwa mwaminifu kwao, asipokuwa mwaminifu 2020 hawampi, habari ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa nasema ukienda kiuhalisia kwenye vijiji vyetu, kuna upungufu wa madarasa na baada ya kusema elimu bure watoto wamefurika mashuleni, madarasa hakuna, madawati hakuna, sasa nawauliza CCM fedha za kujenga madarasa ziko wapi humu, kwenye Mpango wenu mbona hausemi, ziko wapi? Mheshimiwa Waziri unisaidie utakapokuja hapa uniambie hela za madarasa na madawati ziko wapi humu au ndiyo zile za Bunge bilioni sita zitatosha? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vijijini kwenye shule za msingi, ninakotoka Serengeti nimeenda Shule ya Msingi Gwikongo haina dawati hata moja, mimi nimeamua kama Mbunge niwe mfano nisaidie angalau tupate madawati machache kwenye shule ile, lakini wamekuweko Wabunge miaka na miaka, dawati hata moja hakuna, ni shule hiyo! Wilaya ambayo imeongozwa na CCM muda mrefu, dawati shule ya msingi hakuna, halafu mnasemaje mipango, mipango gani hii! Upungufu wa Walimu ukienda shule za msingi, kuna shule moja ina walimu wawili tu, tangu uhuru mpaka leo wapo wawili, halafu mnasema wanafunzi wanafaulu wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM mnamsaidia shetani kazi nawaambia ninyi, maana mnatengeneza majambazi wengi, vibaka wengi, ambao baadaye watakuja kuwatesa ninyi wenyewe, maana ninyi ndiyo mtakuwa matajiri, watawaibia ninyi wenyewe. Unafikiri kama akimaliza darasa la saba, kamaliza *form four* hana ajira unafikiri atafanya kazi gani, atalala na njaa na wewe unashiba hapa, atakushughulikia! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko shida, ukienda sekondari Walimu wa sayansi ni kilio, hivi viwanda mnavyosema mnaanzisha siyo maana yake sayansi, *Physics, Chemistry, Biology, Mathematics* Walimu wako wapi? Walimu wa Sayansi wamekimbia Ualimu maana Ualimu haulipi, hata mimi ni mwalimu wa sayansi nimekimbia kwa sababu hali ni ngumu. *(Makofi)*

Walimu wanalia, walimu wa sayansi unakuta Mwalimu ni mmoja ana vipindi 50 kwa wiki, Mwalimu wa *art* ana vipindi vinne kwa wiki lakini mshahara unajua ni ule ule, hiyo biashara ngumu mzee! Kwa hiyo, walipeni walimu wa sayansi vizuri. Vijana wanapomaliza wamefaulu vizuri sayansi *form four* na *form six* wanaenda kwenye udaktari, wanaenda kwenye mambo mazuri na hata ninyi ambao mko hapa, wengi ambao mmesoma sayansi mmekimbia huko, wengi siyo walimu! Naomba Waziri unapokuja tuambie mmefanya nini kuhusu elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mapato. Serikali ya CCM ni ya ajabu sana, wakiona Halmashauri za Wilaya zimetengeneza vyanzo vizuri vya mapato wanabeba, kule Serengeti tulikuwa na *bed fee* wakabeba, nimesikia sasa hivi wanataka wachukue *property tax.*

**MJUMBE FULANI:** Eeh! wameshachukua.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Sasa ninyi kwa nini msitengeneze vyanzo vya kwenu huko Serikali Kuu, Halmashauri itengeneze vyanzo vya mapato, ninyi mbebe, halafu madawati sisi tutatoa wapi tuwapelekee wale watoto, yaani ninyi mnachukua fedha zote mnakula, eeh mnatumia zote, kwa mfano, mimi nimekuwa Diwani tangu 2010, miaka yote *Capital Development Grant (CDG)* 26 *percent* ndiyo inakuja, mnafanya nini? Hamuwezi kufanya chochote.

Nawaambia CCM pumzikeni tupeni CHADEMA hapa tuongoze nchi tuwaoneshe mambo, maana mmeshindwa! nenda kwenye pembejeo ni kilio, kila kitu ni kilio, ukija nimepewa mahindi ambayo mkulima wangu ameenda amepanda hayakuota, sasa hivi wanapaka rangi wanasambazia wananchi kule hiyo ndiyo Serikali ya CCM. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha siamini sana kauli yako ya mahindi kupakwa rangi. Tunaendelea na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega. Mheshimiwa Bukwimba, Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba!

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami kuchangia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa

wa Miaka Mitano. Pia nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi hasa Awamu ya Tano, kwa mwanzo mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi hasa katika utumbuaji majipu na dhamira thabiti ya ukusanyaji mapato ambao unakwenda kujibu changamoto kubwa ambayo ilikuwepo kwa ajili ya ufinyu wa mapato Serikalini ambapo inatuonesha mwanga sasa miradi ya maendeleo itakwenda kwa maana ya fedha kupatikana kwa wakati na maendeleo kufika kwa wananchi.

Pia, nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango kwa Mpango mzuri aliouwakilisha leo wa miaka mitano ambao unaonesha mwanga wa Tanzania mpya ambayo Watanzania walikuwa wanasubiri mabadiliko tuliyowaambia watayapata ndani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, nchi nyingi zimeendelea kwa kupitia mlango wa viwanda, nchi nyingi zimepiga hatua kwa maendeleo ya viwanda, lakini pamoja na maendeleo ya viwanda pia viwanda vinategemea maendeleo ya miundombinu kwanza, kwa sababu miundombinu ndiyo ufunguo wa maendeleo ya viwanda, pamoja kwamba maendeleo ya viwanda ndiyo ufunguo wa maendeleo ya uchumi, lakini bila miundombinu rafiki, miundombinu mizuri na wezeshi maendeleo ya viwanda yatakuwa yana walakini kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali yangu kwa sababu ili kuwe na maendeleo ya viwanda, lazima Serikali ije na mpango mzuri wa kuboresha hii miundombinu ukizingatia Mheshimiwa Waziri anasema miongoni mwa changamoto ambazo awamu ya kwanza haikuweza kutekeleza vema katika maendeleo mazuri ya miundombinu, kwa mfano, katika miradi mitano ile mikubwa ya mpango huu, lipo suala la Mkulazi, Kijiji cha kilimo lakini miundombinu kule siyo mizuri. Matokeo yake kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, mradi ule unatakiwa kutekelezwa pamoja na ushirikishwaji wa *private sector,* sasa *private sector* nyingi zikienda kule kufanya ukaguzi zinashindwa kufika kwa wakati. Hivi ninavyosema sasa hivi mawasiliano yamekatika huko Mkulazi kwenyewe, tunakwenda miezi sita kipindi cha miezi mitatu hii ya mvua huwezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ili kuwavutia hao *private sector* waje, katika kuutekeleza mpango huu kwa uhalisia wake ni vizuri kuboresha miundombinu ya Mkulazi ukizingatia barabara, mawasiliano, umeme pamoja na maji ili lile eneo liwe rafiki, na liweze kuwavutia wawekezaji wengi kwa ajili ya mradi huu ambao utakuwa unajibu changamoto nzuri kuhusu maendeleo ya kilimo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba nichangie katika suala la kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo, kilimo ndiyo kinachangia asilimia 75 ya ajira ya Watanzania, kilimo kinachangia pato la Taifa zaidi ya asilimia 25, lakini pia kinachangia katika fedha za kigeni asilimia 30 na pia kilimo ndiyo *source* kubwa ya mapato katika Halmashauri zetu nyingi Tanzania...

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa nani, nakuona kwangu kushoto Mheshimiwa, taarifa!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anayeendelea kuchangia sijui anasoma hotuba ya nani, maana yake ni kuchangia, yeye anasoma, naomba Mwongozo wako juu ya hilo.

**MWENYEKITI:** Bahati mbaya au nzuri Kiti hakikuwa kimeona hilo, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu unaruhusiwa kufanya marejeo *(reference)* kawaida, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye ukurasa wa saba nanukuu ni sahihi kabisa, lakini kuchangia kwa kusoma, hilo ndilo Kanuni zinakataza. Kwa vile, jicho la kiti halikuona hilo aendelee kuchangia na muda wake unalindwa. *(Makofi)*

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza unilindie muda wangu na pia taarifa yake siipokei, kwa sababu nilikuwa sisomi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nachangia katika umuhimu wa kilimo, lengo lilikuwa kwa sababu ya umuhimu wa kilimo kama nilivyosema, namwomba Mheshimiwa Waziri katika mpango wake anapokuja, ni vizuri akaongeza bajeti ya kilimo kutoka iliyopo sasa angalau ingefikia asilimia 10, kwa umuhimu wa kilimo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la kilimo, kilimo kinategemea ardhi na sasa hivi tumeona changamoto kubwa iliyopo hapa nchini ni migogoro ya ardhi, nilitegemea katika mpango huu, Serikali ingekuja na majibu ya kutatua changamoto hiyo, hasa katika kupima ardhi, kuzingatia matumizi bora ya ardhi, ili kila eneo lipate mmiliki na wale wananchi waweze kumilikishwa ile ardhi waweze kuitumia kwa ajili ya kupatiwa Hati Miliki kama Hati zile za Kimila, zinaweza zikawasaidia katika kujipatia mikopo katika taasisi za fedha na kuanza kulima kilimo cha kibiashara zaidi kama walivyojiajiri katika hicho kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, tatizo la kilimo katika nchi yetu hii siyo wakulima tu, tatizo kubwa ni miundombinu ya kilimo imeachwa nyuma. Ningeshauri Serikali iongeze bajeti ya kilimo katika miundombinu ya umwagiliaji, ili kilimo kiweze kuwa na uhakika wa mavuno na kiweze kuzivutia taasisi za

fedha ili kuwakopesha wakulima badala ya sasa wanategemea mvua na ndiyo maana wakulima wanashindwa kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri hata pale Serikali ilipokuja na mpango wa kujenga maghala kwa ajili ya kuhifadhia mazao, pesa zile zingetumika zaidi kwenye miundombinu ya kilimo, hasa umwagiliaji. Nafikiri tatizo la maghala wangekopeshwa tu, taasisi za fedha wangeweza kutoa kwa sababu, vile ni vifaa wezeshi tu vya kuhifadhia ambavyo vinavutia hata taasisi za fedha kukopesha wakulima, tofauti na sasa hawawezi kuwakopesha wakulima kwa sababu hawana uhakika mkulima huyu kama atavuna au atafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali ingeelekeza zaidi kuwekeza kwenye miundombinu ya kilimo badala ya mambo mengine, nina uhakika kikiwepo kilimo cha uhakika hizi taasisi za fedha zote zitavutika kwenda kuwekeza kwenye kilimo kwa sababu wana uhakika mkulima atavuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tukiwezesha katika mipango bora hii ya ardhi kupima, tukiwatengea wafugaji eneo lao, kuwatengenezea miundombinu na kuwaweka pamoja nina uhakika hata hawa wafugaji wataweza kukopesheka na wataweza kuendelea na itawavutia wawekezaji wa viwanda vya maziwa waje kuwekeza katika maeneo yale, badala ya sasa wanashindwa kuwasaidia hawa wafugaji kwa sababu wamekuwa wachungaji badala ya wafugaji na mtu anajua kwamba hata akiwekeza katika kiwanda cha maziwa hana uhakika wa kupata *raw material* ya maziwa kwa sababu hawa wafugaji ni wa kuhamahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la masoko ya kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda hapa alizungumza neno la busara kabisa na ni ukweli, kwa sababu alizungumza vizuri akasema, ili bidhaa zetu za kilimo za viwanda ziweze kuuzika lazima bei zetu ziwe za chini, kuna watu wamembeza kwa sababu tunataka tulete siasa katika suala la kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli uliopo haya mazao ya kilimo tunayolima, yaliyo mengi sisi siyo watumiaji tunategemea soko la nje. Soko la nje wauzaji siyo peke yetu, lazima lina ushindani wa hali ya juu, kama bidhaa zetu zitakuwa na gharama kubwa wanunuzi wana nafasi kubwa ya kwenda nchi nyingine au kununua sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mchangiaji mmoja alizungumza hapa akasema wakulima hawana uhakika mwaka huu wanalima mbaazi bei imepanda, mwakani imeshuka analima ufuta! sababu kubwa haya ni mazao ya muda mfupi na kama mazao ya muda mfupi, mwaka huu Tanzania mkilima ufuta mkipata bei nzuri mwakani nchi nyingine nazo zinalima, matokeo yake *supply* inakuwa kubwa kuliko *demand,* ndiyo maana bei inashuka bei nyingine

inapanda, sasa tukitaka tulete siasa katika mambo ya uchumi hatuendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Serikali kwa mipango mizuri inayokuja nayo, Waziri wa Viwanda tuelezane ukweli na ndiyo maana nilishauri siku moja ni vizuri kukaundwa taasisi ya utafiti wa masoko ulimwenguni ili kutoa taarifa kwa wakulima wetu kuwaambia nini kinachohitajika ulimwenguni sasa hivi kilicho na bei nzuri badala ya kilimo cha historia, umezaliwa baba yako analima kahawa, analima mkonge, unataka ulime kitu hicho tu, wakati mwingine zao hilo halihitajiki huko kwa walaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala la migogoro ya ardhi. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi kwa kazi kubwa aliyoifanya na mimi ni mnufaika mmojawapo. Alifika kijijini kwangu katika Kata ya Tununguo katika Kijiji cha Mliringwa na alichukua maamuzi hapo hapo baada ya kuona ubabaishaji. Aliweza kuirudisha kwa wakulima ardhi ya heka zaidi ya 3,500 kutoka kwa wawekezaji wababaishaji ambao waliipata kwa ujanja-ujanja. Nakuomba Mheshimiwa Waziri urudi tena, kama unavyoona Morogoro mkipita yote yale ni mapori, lakini siyo mapori ni mashamba ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa la mashamba pori, wenyewe wenyeji hatuna pakulima, kila shamba lina hati, lakini hayaendelezwi. Nakuomba sana urudi myahakiki, ili mturudishie tuweze kuendelea. Morogoro ilikuwa ndiyo hifadhi ya chakula, lakini kila mwaka uzalishaji wa chakula unapungua, sababu kubwa ni ardhi imeshikwa na watu ambao wameenda kukopea hela badala ya kuitumia kwa ajili ya uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho, naomba katika mpango ule wa Mkulazi, shamba namba 217 lenye hekta 63,000, mpango wa Serikali hekta zote 63,000 mnataka muwape Wawekezaji, heka 3,000 tu ndiyo mmetubakizia watu wa Mkulazi, watu wa Morogoro na Watanzania kwa ujumla, hizi heka 3,000 hazitoshi kwa Watanzania katika kijiji hiki cha mfano kinachotaka kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu na naishauri Serikali, tusiiuze hii ardhi kwa mgongo wa wawekezaji kwa watu wachache kama mpango unavyosema, heka 20,000 kwa mwekezaji mmoja wa miwa, heka 20,000 kwa mwekezaji wa pili wa miwa na heka elfu tano tano kwa maana ya 20,000 zilizobaki kwa wawekezaji wanne wa mpunga, halafu Watanzania tuliobaki au watu wa Morogoro heka 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ni vizuri ardhi hii ikagawanywa mara mbili, nusu ikaenda kwa *outgrowers* kwa maana ya watu wa Mkulazi, Morogoro na Watanzania kwa ujumla waje wapate elimu ya kilimo cha kisasa pale kwenda kusambaza kwingine badala ya kuiondoa ardhi hii yote kuwapa

wawekezaji huko mbele tunakokwenda kutakuwa ni kweusi, tusije kupata madhara kama wanayoyapata nchi nyingine, huko mbele vizazi vyetu vikaja kugombea ardhi na kuuana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omary Mgumba. Tunaendelea, anayefuata ni Mheshimiwa Sabrina Sungura hayupo, tunaendelea, anayefuata Mheshimiwa Ali Salim Hamis, Waheshimiwa naendelea na nafasi hizi hazitarudi! Anayefuata ni Mheshimiwa Ally Saleh hayupo, anayefuata ni Mheshimiwa Stanslaus Nyongo!

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda nitoe shukrani kwa Wabunge wote waliotoa michango mizuri kabisa na ushauri mzuri. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mpango kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa Pili kwa kweli ni Mpango mzuri iwapo utekelezaji angalau utafikia asilimia 50 au asilimia 80, tunajua inawezekana kwa namna moja au nyingine inaweza isiwe asilimia 100, lakini basi angalau ikiwa asilimia 80 tutakuwa tumekwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** katika mpango huu nizungumzie kidogo upande wa viwanda na maeneo mengine, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi tulipokuwa tunainadi wakati tunaomba kura kwa wananchi, tulisema kwamba tutajikita zaidi kwenye viwanda, tutaanzia kwenye viwanda vinavyotumia malighafi tunazozalisha nchini, kwa maana ya mazao yanayotokana na kilimo *(Agro Processing Industry)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *agro processing* inabidi tujitahidi tujikite tufanye tafiti mbalimbali tuweze kutafuta mbegu zenye tija, kwa mfano, mbegu za alizeti tunazotumia kwa sasa ni mbegu za miaka ya nyuma, hakuna mkakati madhubuti wa kutafuta mbegu mpya ambazo zinaweza zikatoa mafuta mengi ya kutosha. Mbegu tunazozitumia sasa hivi ni mbegu ambazo tunapata mafuta kwa asilimia 60 mpaka asilimia 70, tunatakiwa tupate mbegu mpya, tafiti zifanyike, ili tuweze kupata mafuta mengi yanayotokana na mbegu tunazosindika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta ya alizeti tunapata asilimia 70 kumbe tungeweza kupata mbegu ambazo tunaweza tukapata mafuta asilimia 80 mpaka asilimia 90 tukipata mbegu bora, Mtanzania anayelima alizeti, anayelima pamba, atapata kipato kikubwa na mzalishaji au msindikaji wa

mafuta atapata faida kubwa na tutapata mafuta mengi ambayo ni kwa gharama nafuu na tutakwenda kuyauza kwenye soko letu kwa gharama nafuu na vilevile tunapokwenda kwenye ushindani wa soko la Kimataifa basi tutauza kwa bei nzuri na bidhaa zetu za Tanzania zitaweza kuuzika katika masoko yote ya Afrika Mashariki na ya Kimataifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tulitangaza kwamba, tutajikita kwenye viwanda ambavyo vinazalisha au vinavyozalisha ajira kwa wingi. Viwanda vikubwa, kwa mfano viwanda vya *textile (*viwanda vya nguo), vinazalisha ajira kwa watu wengi. Unakuta kuna watu wengi wanafanya kazi ya kutengeneza nguo kwa mfano suruali au shati, kila mmoja ana kazi yake mmoja anapinda, mwingine anatengeneza tundu la kifungo, mwingine anafanya shughuli nyingine, kwa ujumla kunakuwa na ajira nyingi sana kwa Watanzania. Kwa hiyo, tutapata ajira kubwa, watu wataweza kufanya kazi, wataongeza kipato pia itaongeza uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, tujikite kule tusisahau tuliyoahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tujikite kwenye viwanda mama. Suala la Liganga na Mchuchuma, viwanda vinavyozalisha vyuma, viwanda vinavyozalisha nishati ya umeme, tujikite huko ili tuweze kupata umeme wa bei nafuu, tupate malighafi za bei nafuu na tuweze kuuza kwenye viwanda vidogovidogo hapa nchini, hapo tutaweza kujikwamua. Bila kufanya vile itakuwa ni tatizo kwa sababu hata wenye viwanda waliopo sasa hivi, wanaozalisha bidhaa mbalimbali, bidhaa nyingi tunadhani zinazalishwa nchini lakini ukichunguza kwa nyuma yake unakuta zinaingizwa kutoka nje ya nchi kama malighafi na malighafi zenyewe zinatozwa kodi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake uzalishaji unakuwa ni wa gharama kubwa na uuzaji wa bidhaa unakuwa ni wa bei juu, tunashindwa kuingia kwenye ushindani kwa sababu bidhaa zetu ni za bei ya juu, tunakuta kwamba, bidhaa zetu haziuziki, zinazouzika ni za nje ya nchi na ndiyo maana uingizaji wa bidhaa za nje ni mkubwa kwa sababu bidhaa za nje zinauzwa kwa bei nafuu bidhaa zetu zinakuwa na bei ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nizungumzie katika masuala ya Mkoa wangu wa Simiyu. Mkoa wa Simiyu ni mkoa wenye malighafi nyingi zinazotokana na kilimo, lakini Mkoa wa Simiyu ni Mkoa mpya, hatuna barabara. Ni miradi michache ya barabara ambayo tayari imeshaanzishwa, lakini utekelezaji ni mdogo.

Tunaomba Mkandarasi aliyeko *site* apewe pesa ili *project* iendelee, tutengenezewe barabara ya lami na tukishaunganisha Mkoa wetu wa Simiyu tukaweka kiwango cha lami kuunganisha na barabara ambazo zinakuja Dar-es-Salaam kuna uzalishaji mkubwa wa pamba ambapo marobota ya pamba

yanayozalishwa katika Mkoa wa Simiyu yataweza kuja Dar-es-Salaam na kulisha viwanda vyetu vya *textile* na mambo yanaweza kuendelea na uchumi unaweza kuimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kuongelea katika Mkoa huo wa Simiyu ni suala la mradi wa maji. Kuna mradi wa maji kutoka Ziwa Viktoria unaotakiwa kuleta maji katika Mkoa wa Simiyu, tunaomba utekelezaji wa mradi huu uharakishwe. Tunategemea maji mengi ya kutoka Ziwa Viktoria kwa matumizi ya aina mbili, kwa maana ya *domestic use* na vilevile tutumie maji kwa ajili ya *irrigation. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Mwanza ina mpunga wa kutosha. Tunaweza tukalima zaidi kwa maana ya kulima mpunga kwa chakula, tulime mpunga kwa maana ya zao la biashara. Sasa hivi duniani watumiaji wa zao la mpunga ni wengi wanazidi kuongezeka, waliokuwa wanaongoza ni wale watumiaji wa zao la ngano, sasa hivi zao la mpunga limeongezeka, watu wanatumia zaidi mchele, kidogo wanatumia na mahindi, lakini zao la mchele linatumika zaidi. Kwa hiyo, tujitoe katika zao la mchele kudhania ni zao la chakula, sasa tutambue mchele ni zao la biashara.

Mkituletea maji ya kutosha katika Mkoa wetu wa Simiyu, basi tuna hakika wakulima Mkoa wa Simiyu wataweza kulima mpunga kwa wingi na mpunga huo tutaweza kulisha kwa asilimia kubwa Tanzania nzima, tunaomba mradi huo utekelezwe mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo unahitaji pesa nyingi ambazo tuliambiwa kwamba, zimeshatolewa kiasi kidogo na *feasibility study* imeshafanyika. Tunaomba basi utekelezaji ufanyike mtuletee maji ya kutosha katika Mkoa wa Simiyu tuweze kulima, tuweze kulisha mifugo, tutumie maji yale kwa tija, ili tuweze kuleta maendeleo. Kuna Mikoa mingine ina ardhi kubwa kama Simiyu, lakini ardhi haitumiki kwa sababu hatujaweza ku-*facilitate* ardhi yetu itumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kusonga mbele kuna suala la rasilimali watu. Nchi yetu ina watu zaidi ya milioni 46, kuna vijana wengi hawana ajira, vijana wengi wako mtaani ambao kwa kweli tukiweza kuweka mazingira mazuri ile tunasema ni *human resources* ambayo inaweza ika-*generate* uchumi wetu ukakua kwa hali ya juu. Tumeshindwa kutafuta namna ya kutumia nguvu za vijana tulionao mjini. Ukienda mjini, ukienda vijijini unakuta vijana wanacheza mpira, wanacheza *pool!* Mheshimiwa Rais juzi kazuia *pool!* Wanacheza *pool* kwa sababu, hawana kazi ya kufanya, tuna nguvu kazi kubwa katika nchi yetu ya Tanzania lakini tunashindwa kutafuta namna ya kuitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu wa miaka mitano kwenda 2025 tutafute namna nzuri ya kuweza kutumia nguvu ya vijana wetu. Ukienda mjini vijana wanacheza mpira, mpira wenyewe wanacheza wengine wanavuta bangi, wako kwenye vijiwe hawana kazi ya kufanya! Tunaomba tuangalie na upande huu, tusiangalie tu vitu vingine, lakini tuangalie tutatumia vipi nguvukazi za hawa vijana kwa maana ya kunufaisha uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ningeweza kuliongelea katika sekta binafsi, ili tuweze kuimarisha uchumi ni lazima tukumbuke sekta binafsi ndiyo sekta pekee inayoweza ikasaidia kuongeza au kufanya *industrialization,* twende kwenye nchi ya viwanda, bila sekta binafsi hatuwezi kufika. Tuweke mazingira mazuri kwa sekta binafsi, mazingira mazuri ambayo yatawawezesha watu wa sekta binafsi wafanye kazi zao vizuri, wafanye kazi zao kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama kwa harakaharaka katika masuala ya kodi, ni lazima tuitazame vizuri. Kwa mfano, mtu anaingiza bidhaa kwa maana ya uzalishaji, anaingiza mashine kubwa za uzalishaji, ukifika pale anatozwa kodi ya *VAT,* mtu analeta mashine ya kuja kutengeneza ajira, analeta mashine kubwa ya uzalishaji, lakini katika *importation* unakuta anachajiwa *VAT! VAT* ina-*discourage* kabisa watu kuingiza bidhaa kwa ajili ya uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *VAT* nchi zingine mtu anapo-*import capital goods* kwa maana ya kwenda kuzalisha hatozwi kodi! Nenda Msumbiji, nenda nchi zingine, hawatozwi hiyo kodi! Sasa asipotozwa hiyo kodi na Tanzania tunatoza, basi mwekezaji huyu hawezi kuwekeza Tanzania atakachokifanya ni kwenda nchi nyingine na kuwekeza na akiwekeza kule ata-*create* ajira kule, ata-*create production* kule ya tija, tunajikuta tunabaki palepale na Mpango wetu unabaki kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tubadilike, twende mbele, tuangalie nini tuanze nacho na nini tumalize nacho, lakini tukienda kwa kubeba mambo yote tunaweza tukajikuta tunamaliza miaka mitano bado hatujafika kule tunakotakiwa kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme suala lingine kuhusu uwekezaji kwa maana ya uwekezaji wa nje na ndani. Tunayo *TIC,* tutazame *TIC* ijikite kwa kuwawezesha wawekezaji wa ndani waweze kuwekeza vizuri. Wawekezaji wa nje wanapokuja nchini kwetu na wao wanakutana na mazingira mabaya vilevile. Ukiangalia nchi yetu katika huu Mpango wa Serikali wa miaka mitano tumeweka katika namba mia moja thelathini na kitu! Ina maana kwamba, hatuna mazingira mazuri ya uwekezaji! Ni lazima tuangalie leo tunapoamua kuwekeza au kukaribisha wawekezaji tuangalie *Central Government* inasemaje na *Local Government* inasemaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *conflict* kati ya *Central Government* pamoja na *Local Government*, *Central Government* tunakaribisha mwekezaji, lakini mwekezaji akienda kule kijijini, akienda kuwekeza, akikutana na watu wa Serikali za Mitaa kule wanamuona mwekezaji kama ni adui. Mwekezaji anakutana na mazingira magumu, anafukuzwa na wakija watumbua majipu wananchi wakisema huyu mwekezaji hafai watu wa chini wanashangilia. Tunamwona kama mwekezaji ni mwizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba itolewe elimu, mwekezaji atambulike kwamba huyu ni mwekezaji anakuja kwa faida ya nchi yetu, mwekezaji anakuja kutengeneza ajira, mwekezaji siyo mwizi. Elimu maalum itolewe watu watambue kama mwekezaji ni mwenzetu. Kinachoendelea sasa hivi wawekezaji wamekutana na mazingira magumu, unakuta watu wa *NEMC* wanasimamisha kiwanda huyu anachafua mazingira, kiwanda kinasimamishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisimamisha kiwanda palepale umesimamisha ajira ya watu walioajiriwa pale, ukisimamisha kiwanda *production* inasimama, huyu mtu *ana-fixed cost* unamwingiza kwenye gharama kubwa, unadhani kesho atakuja kuwekeza Tanzania? Tunaomba uwekwe utaratibu, elimu itolewe, kama ni watu wa *NEMC* wanakwenda kusimamisha viwanda visifanye kazi eti kwa sababu ya mazingira, basi hao watu wa *NEMC* wawe wameshatangulia kwenda kutoa elimu ya kutosha kumwelekeza mwekezaji ni namna gani ya kutunza mazingira ili tusiwe tunasimamisha *production unnecessary* kusema kwamba huyu mtu anaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mazingira mazuri ya kumfanya huyu mtu aone kwamba kuwekeza Tanzania ni vyema, kuwekeza Tanzania utapata faida, hakuna anayewekeza bila kupata faida, lazima tuwawekee mazingira mazuri ya wao kupata faida na tuweke mazingira mazuri ya sisi kama Watanzania kupata faida, tuweke mazingira mazuri kwa vijana wetu kupata ajira kama Watanzania kupitia uwekezaji wa nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kusema kwamba kuna tafiti mbalimbali za kibiashara zinafanyika, tunazibeza hatuzifanyii kazi. Ukienda kwenye Vyuo Vikuu kuna tafiti mbalimbali zinafanyika, yaani *Marketing survey* na *marketing research*, tafiti hizo ziweze kutumika. Wengine wanafanya tafiti kwa maana ya kupata *degree* zao, kuna wengine wanafanya tafiti kupata *masters* zao na wanafanya tafiti ambazo ni za kweli, wanakwenda *field* wanakusanya *data* za kutosha, wana-*interpret* zile *data* walizozipata kule na vilevile wanakuja na mapendekezo nini kifanyike. Tunaomba tutumie tafiti hizo tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nyongo kwa mchango wako mzuri, umetusemea na wengine ambao kwa sasa hatuwezi kusema kwa Mkoa wa Simiyu.

Nisimame ili nitoe tangazo moja kwa sababu tusiwasumbue sana Waheshimiwa Wabunge kwenda kujiorodhesha kule.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 38(5): "Iwapo Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo Bungeni siku ya Alhamisi kunakuwa hakuna kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu."

Kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu hatakuwepo Bungeni kwa maana hiyo, kwa mujibu wa kifungu cha 38(5) hapatakuwepo na Maswali kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge ambao mnaenda ofisini kujiorodhesha kwa zoezi hilo bakini tu kwenye ukumbi kwa sababu kipindi hicho kwa kesho hakitakuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Bashe hayupo, anayefuata ni Mheshimiwa Omari Kigua hayupo; naendelea, anayefuata Mheshimiwa Riziki Shahari Ngwali hayupo; tunaendelea anayefuata ni Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha Mpango wake na nikazidi kupata maswali mengi ya utekelezaji wa Mpango wake kwa sababu mambo mengi ambayo ameyaandika yanaonekana kwenye nadharia na huenda yasitekelezwe au yasitokee kabisa kama Mpango uliopita. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba anataka kuweka mazingira mazuri ya kibiashara kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafanya maendeleo ya viwanda Tanzania

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mazingira hayo mazuri ya kibiashara Mheshimiwa Waziri hakuyaeleza kinaga ubaga na hilo linanitia mashaka, kwa sababu nikifikiria moja kati ya vitu ambavyo ni vya kipaumbele ili tuweze kukuza viwanda Tanzania tunaongelea habari ya umeme, miundombinu lakini mpaka leo na hata ukiangalia katika bajeti tuliyonayo hakuna nguvu ya ziada ambayo Serikali imeiweka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano wa mazingira ambayo tunaishi Watanzania leo, bei ya umeme bado iko juu na wanasema kwamba

wamepunguza kwa asilimia mbili lakini *effect* yake katika punguzo hilo haionekani katika uhalisia wa maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika mazingira ya sheria ambazo Mheshimiwa Waziri alitakiwa azieleze kwamba ndiyo zimerahisisha utekelezaji wa sera hii ya viwanda, sioni kama ameonesha kwa njia yeyote ila ameweka sheria kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wadogo wadogo, labda kama yeye alipokuwa anaongelea maendeleo ya viwanda alikuwa anaongelea wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii wawekezaji wadogowadogo hasa wale wanaohusika na mazao ya kilimo wanawekewa vikwazo, wanawekewa sheria ngumu na wanawekewa tozo mbalimbali ambazo mwisho wa siku zinawafanya wazidi kukwama katika harakati hii ya kujiendeleza katika kutengeneza malighafi kwa ajili ya maendeleo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano moja katika Jimbo la Kahama Mjini, Jimbo lile kuna watu wanashughulika na biashara ya upakiaji na uchakataji wa zao la mpunga, lakini leo hii ukiangalia tozo ambazo wanatozwa watu wale mpaka wanafikia hatua ya kukata tamaa kujihusisha na zao hili la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamewekeza fedha zao kwa ajili ya kutengeneza na kupaki zao hili la mpunga, lakini kuanzia asubuhi mpaka jioni umeme hauwaki, ukiwaka jioni Polisi wanapita wanasema hairusiwi mtu kufungua kiwanda usiku. Kwa hiyo, wanajikuta ndani ya mwezi mzima watu wale wanashindwa kufanya uzalishaji, kwa hivyo hata zile fedha ambazo wamewekeza mle wanashindwa kuzirejesha kama walizikopa kwenye mabenki, lakini pia wanashindwa kuzizalisha ili ziweze kuwaletea faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa ukiangalia ambao ni wazalishaji, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, anataka kuendeleza viwanda, lakini nimesikitishwa na taarifa ya Waziri anasema kwamba bei za mazao zinapaswa zizidi kushuka. Swali hasa lilikuwa limeelekezwa kwenye zao la maziwa ambapo Mkoa wa Shinyanga tunafuga sana ng'ombe, kwa sasa hivi lita ya maziwa ni shilingi mia nne mpaka shilingi mia tano na watu wale hawanufaiki, kumfuga yule ng'ombe ni gharama, sindano moja inakugharimu kuanzia laki nne mpaka tano kwa ngombe mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ile shilingi mia nne, shilingi mia tano kwa lita ya maziwa unaambiwa izidi kushuka sasa sijui yauzwe lita moja shilingi mia mbili, hapo sijamuelewa vizuri! Kwa maana hiyo, ni kwamba, tunawakatisha tamaa wakulima, tushushe bei ya zao la maziwa, tushushe bei ya zao la pamba, tushushe bei ya zao la tumbaku, halafu unasema watu tuko katika harakati za kuzalisha malighafi ya kutosha ili tuweze kuendeleza viwanda Tanzania!*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukisikia kauli mbalimbali za Serikali zikibeza misaada, lakini ukiangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema wazi kwamba gharama kwa ajili Mpango huu wa Maendeleo itakuwa ni trilioni 107 na Serikali itatoa trilioni 59 tu, hiyo baki inayobaki tunategemea kuitoa wapi? Bila shaka fedha hizo huenda zingetoka kwa wahisani au wafadhili na labda kukopa kwenye mabenki ambapo mwisho wa siku inaonekana kwamba fedha hizo tunashindwa kuzirejesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kutoa kauli badala yake inazidi kuwabeza hawa watu. Sasa hivi tuko katika ulimwengu wa teknolojia, wanazipata hizi taarifa na hakuna mtu yeyote anayeshtuka na kuona kwamba yule mtu anayetusaidia angalau kidogo tunatakiwa tumheshimu, badala yake tunatoa kauli za kukejeli na kauli za dharau, wakati leo hii waziri anathibitisha wazi kwamba ana zaidi ya nusu ya gharama ya bajeti ambayo hajui atakapoitoa. Matokeo yake anategemea kwenda kuzidi kuwabana watu kwa kuchukua *property tax* za Halmashauri, anategemea kwenda kuwabana watu kwa kuchukua kodi mbalimbali ambazo Halmashauri inakusanya kwa ajili ya kujiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika mazao mbalimbali ambayo leo hii yalitegemewa yatunufaishe Watanzania. Wakati tunachambua sheria ndogo za Halmashauri, tulionamkulima amebebeshwa mzigo mkubwa sana. Kwa mfano, moja kati ya sheria ndogo mkulima anaambiwa achangie mpaka fedha kwa ajili ya Mwenge, hivi kweli Mwenge, kwa nini Serikali Kuu isitoe hiyo pesa kama kweli inaona hilo jambo ni la muhimu sana hata inambebesha mkulima mdogo kutoa hiyo pesa ikiwa ni moja kati ya tozo ambayo imelimbikizwa katika zao lake lile ambalo anategemea kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni sehemu ambayo Mheshimiwa Waziri ananieleza juu ya kuboresha ufundi stadi ili kuweza kupata watu ambao wataweza kufanya kazi katika hivi viwanda ambavyo vinategemewa kuanzishwa. Katika mikoa tumeona kuna *VETA* moja tu katika kila Mkoa na mtu anavyotaka kufungua Chuo cha Ufundi Wilayani kuna ukiritimba mwingi na *process* ndefu ambayo inamkwamisha mtu binafsi kuweza kufungua Chuo cha Ufundi au Chuo cha *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri afahamu kabisa kwamba tunayo sera ya kwamba mwekezaji anatakiwa kuajiri watu wanaozunguka eneo alilowekeza. Walio wengi na miradi mingi inawekezwa maeneo ya vijijini na maeneo yale hayana watu ambao wana elimu ya juu na wanategemea kupata watu ambao angalau wanaweza kuwa na elimu ya ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa mgodi wa Buzwagi na Bulyanhulu ambayo ipo katika Vijiji vya Kakola na Wilaya ya Kahama, maeneo yale watu wengi siyo kwamba wana elimu ya juu, lakini hakuna Chuo cha Ufundi kwa ajili ya kuendeleza wale watu, unamkuta mtu anafanya kazi ya kibarua zaidi ya miaka minne, mitano, kwa sababu hana jinsi ya kusoma angalau masomo ya jioni ili aweze kupanda kutoka ile *rank* aliyopo kwenda juu, inambidi aendelee kufanya kazi ile itakayomtesa kwa miaka nenda miaka rudi halafu leo Waziri anasema anataka kuendeleza ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaelewa vizuri mkakati wa Waziri anaposema anataka kuuza viwanda, kwa sababu kwa upeo nilionao ni kuwa viwanda vikubwa vinatokana na viwanda vidogovidogo ambavyo vinaanzishwa na wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii pale Kahama tunalo soko la wakulima, wale watu wamejiunga kwenye ushirika na wamekusanya fedha zao wamejitahidi wameweza kutengeneza lile soko na leo linaonekana ni moja kati ya masoko makubwa katika Mji ule. Hata hivyo, leo ukiangalia soko lile Serikali imekubali ule ushirika kuupeleka ukauzwa kwa mtu binafsi, wakati Sheria ya Ushirika iko wazi kwamba soko lile lilitakiwa liuzwe kwa ushirika mwingine ulio hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linaungwa mkono na Serikali, kibali kimeshatoka, soko lile ambalo wananchi wamekusanya jasho lao linapelekwa kupewa mtu binafsi, wakati wale watu waliweka nguvu. Nilitegemea Serikali iwasaidie, iwawezeshe, iwape mtaji ili lile soko liweze kuwa kubwa, liweze kukidhi mahitaji ya ndani na ya nje ya Mji ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutilia mkazo katika elimu. Kama kweli tunataka kwenda katika biashara ya viwanda ni lazima tuhakikishe tunatoa elimu ambayo ni ya ubunifu na wananchi wana uwezo wa kutoa ubunifu kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. Elimu tuliyonayo leo hii ni ile ya kukariri, ndiyo maana unasikia mara leo Mama Mheshimiwa Ndalichako anasema kuna *GPA*, mara anarudi kwenye *Division*, ni kwa sababu hatuna *system* ambayo inaweza kutambua njia sahihi ya utoaji wa elimu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tuko *serious* hatuwezi kusema tunaenda kuendesha elimu kwa njia ya mtu kutoa matamko tu kwenye magazeti. Elimu inatakiwa iboreshwe kwa kufanyiwa utafiti na ikidhi mahitaji ya Watanzania na siyo kwa kukidhi mahitaji ya Serikali ya CCM inasema hivi, kesho inakuja Serikali nyingine inasema mnawayumbisha watoto mnawa- *frustrate,* naomba Serikali iwe *serious* tunapoongelea masuala ya elimu kwa ajili ya mabadiliko ya viwanda hatuongelei tu suala la kufurahisha chama fulani au chama fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ningependa kuongelea suala zima la miundombinu. Barabara za Mitaa na barabara za *TANROAD,* barabara hizi zimegeuzwa kama mitaji. Tunayo barabara ambayo inatoka Kahama inaelekea Kakola pale Jimbo la Shinyanga kuunganisha na Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafahamika wazi kwamba uwezo wa ile barabara haiwezi kubeba magari ya ukubwa wa namna ile ambayo yanapeleka mizigo mbalimbali kuelekea mgodini na kuelekea Geita, badala yake *TANROAD* imegeuza ile barabara kama mtaji, kila mwaka ile barabara inafanyiwa *repair*, inamwagiwa kifusi na ku-*level,* sasa hivi ni zaidi ya miaka kumi tangu mgodi ule umeanzishwa barabara ile inafanyiwa *repair* kila mwaka na mamilioni ya fedha yanapotea. Naomba Waziri husika alitazame hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongelea maendeleo ya viwanda hatumaanishi kudunduliza pesa, bora kama fedha ni ndogo basi tuwekeze mahali ambapo tunaona kwamba italeta tija na italeta maendeleo ya nchi hii, lakini siyo tunaruhusu watu wanatumia hii kama ni njia ya kujinufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Naendelea na orodha yangu, Mheshimiwa anayefuata ni Julius Kalanga Laizer.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mi nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala huu uliopo mbele yetu. Nami nianze katika maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza tunazungumza habari ya mipango ya nchi yetu kwa miaka mitano na kama tunazungumza mipango tujue pia madhara ya mipango ambayo iliwahi kujadiliwa hapa Bungeni kwa waliokuwepo na haikufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakumbuka kwamba miaka minne iliyopita nchi yetu ilijadili habari ya Sheria ya Manunuzi hapa katika Bunge na ikaleta mvutano mkubwa sana. Leo tunasema sheria hiyo ni mbovu kuliko sheria zilizowahi kutokea kwenye nchi yetu na kila mtu analalamika. Kwa hiyo, tunapojadili suala hili ni vizuri tukaweka maslahi ya Taifa letu mbele tukajadili na mkapokea ushauri kwa ajili ya kujenga uchumi wa Taifa letu. Sheria mbovu hizi ambazo ziko kwenye Taifa letu ni majanga kwetu sisi wote. Kwa hiyo ni vizuri mkapokea ushauri na mkaufanyia kazi kuliko kutazama tu imetolewa na watu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nitaanza na elimu. Leo tunazungumza kwamba tunaenda kutoa bei elekezi ya ada za shule katika

shule za binafsi na hii ni kwa sababu ya *fear*, hii ni kwa sababu ya hofu ya miundombinu mibovu na taaluma yetu katika nchi yetu. Kwa hiyo, kwa sababu tumeona shule za Serikali zinafanya vibaya tunawalazimisha wawekezaji wengine nao wa *subsidize* ada zao ili wafanye vibaya tuweze kujishindanisha nao, ni vizuri Serikali ikaiga na kufanya *competition* kwa kufanya mambo yafuatayo katika elimu kwa miaka mitano:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuboresha miundombinu na maslahi ya Walimu. Bahati nzuri tunaambiwa Rais alikuwa Mwalimu, Waziri Mkuu alikuwa Mwalimu, Mheshimiwa Profesa Ndalichako alikuwa naye ni Mwalimu na asilimia kubwa ya Wabunge hapa ni Walimu. Leo unazungumza habari ya Mwalimu anayetembea kilomita mbili, tatu kwenda na kurudi kila siku shuleni, hana nyumba anategemea mshahara wake alipe nauli, anategemea mshahara wake alipe nyumba ya kupanga kule shuleni, halafu akafanye vizuri, hawezi kufanya vizuri! Kama tumeshindwa kujenga nyumba za Walimu tuwape Walimu fedha kwa ajili ya kupanga maeneo ya kuishi, tunawalipa shilingi ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni madarasa na nyumba za watumishi hakuna katika shule nyingi za vijijini, mnategemea huyo mwanafunzi atafaulu kwa namna gani? Kwa hiyo, ni vizuri tukawa na mipango inayolenga kuboresha elimu yetu tukajishindanisha na shule za *private* kuliko kuwaambia shule za *private* washushe ada ili nao wafanye vibaya tuweze kujiona kwamba wote ni kundi la wajinga, haiwezekani! Ni wajibu wa Serikali kutoa elimu kwa wananchi wake, wahisani hawa wanatusaidia tusiwa-*discourage* kwa kuwalazimisha kufanya jambo ambalo hawawezi kufanya kwa ajili ya kuendeleza elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu lingine ni suala la mifugo, simwoni Mheshimiwa Waziri lakini nilitamani awepo, kwa sababu sisi ni wafugaji na sehemu kubwa ya Watanzania ukiwaacha wakulima ni wafugaji. Ukienda Mji wa Kajiado, Kenya asilimia 80 ya mapato yao yanatokana na mifugo na mifugo hiyo inatoka Tanzania, inatoka Shinyanga inakuja Arusha inasafirishwa inaenda Namanga inaenda Kenya. Kwa nini sisi tunashindwa kujenga viwanda kwa ajili ya ku-*accommodate* bidhaa zinazotokana na mifugo? Tunategemea kujenga uchumi wa viwanda kwa kutegemea wafadhili, lakini hatutaki kujenga viwanda vinavyo-*accommodate* bidhaa zinazozalishwa na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo maziwa, nyama, na ngozi, lakini hatuna viwanda vya namna hiyo. Nawaambia mwaka 2020 tutakuja kuzungumza habari ya utekelezaji wa mipango hii kwa asilimia 10 au asilimia 15 kama hatutakubaliana kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa na wananchi wetu zinajengewa mazingira ya kupata soko la uhakika ili waweze kuzalisha zaidi. Kwa hiyo, tutashauri kuwepo na viwanda vya bidhaa zinazotokana na mifugo,

ngozi, nyama na maziwa maeneo ya shinyanga, Arusha ili kudhibiti upelekaji wa mifugo yetu nchini Kenya na kwenda kuwanufaisha watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji ule unaishi kwa ushuru tu wa mifugo, lakini sisi hata soko tu la kuuza mifugo hatuna, hata kiwanda cha maziwa hatuna, halafu tunazungumza nchi ya viwanda!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na viwanda vilevile ni lazima tuwe na miundombinu, ardhi tumetengeneza mazingira gani kwa ajili ya kufanya uwekezaji. Kwa hiyo, tunaposema mnapiga kelele hamna mipango mnatu-*challenge* lakini ukweli ndiyo huo! Huu siyo Mpango wa kwanza kuletwa na Serikali, umeshaletwa miaka mitano, lakini leo tukiwauliza mmetekeleza mipango ile kwa asilimia ngapi hakuna! Sasa tukisema hata huu hamtekelezi mnasema tunawapinga, tunataka mtu-*prove* kwamba tunawapinga bure kwa kufanya utekelezaji wa mipango hii mliyoleta kwa asilimia angalau themanini, kitu ambacho hakiwezekani, hamuwezi kufanya kwa sababu mnapenda kuandika lakini hamtaki kuweka mipango ya kupata fedha ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni muhimu katika suala la viwanda, leo tunazungumza habari ya viwanda, lakini hatusemi kwa nini viwanda vilikufa, hatusemi kwa nini tulikwama na tumeweka *mechanism* gani ya kuendelea hapa. Sisi wenyewe ni mashahidi, katika watu wanaouwa viwanda nchi hii ni Serikali kwa kuwa-*discourage* wawekezaji wa ndani na kuwakumbatia wawekezaji wa nje. Maeneo mengi watu wanalalamika, mkulima anazalisha alizeti, unaweka kodi kwenye uzalishaji wa mafuta, lakini mafuta yanayotoka nje yanaingia na zero, halafu mnategemea mtu alime alizeti, mtu atengeneze kiwanda cha alizeti kama anaweza kuagiza mafuta nje bila kodi, halafu tunasema tunazalisha! Hatuwezi kuwa na viwanda vya namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya leo tunazungumza wao wameweka asilimia arobaini ya manunuzi yao yote lazima yafanyike na *local contractor* ndani ya nchi yao, sisi tunasema bilioni mbili tu *international competition.* Hatuwezi kujenga nchi kama hatuwa-*encourage* wawekezaji wa ndani kufaidi uchumi wa nchi yao. Ndiyo maana leo tunawaambia Kiwanda cha Urafiki kinakufa kwa sababu asilimia hamsini na moja ni ya China, asilimia arobaini na tisa ni Serikali na Wachina wanataka kubadilisha kile kiwanda cha Urafiki iwe ni sehemu yao ya kuingiza bidhaa kutoka China na kufanya *dumping* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iangalie kiwanda cha Urafiki. Mheshimiwa Waziri tulikuambia kwenye Kamati na narudia kusema kwa kweli tunaomba Wabunge tuisimamie Serikali kwa sababu kuna hujuma na kuna ufisadi mkubwa katika Kiwanda cha Urafiki, kwa sababu Wachina wamepewa asilimia hamsini na moja, Serikali inashindwa kununua asilimia tatu tu, ili iwe na

*say* katika kiwanda cha Urafiki. Hatuwezi kuendesha nchi yetu kama viwanda tulivyonavyo sisi tunaviua wenyewe kwa sababu tunaogopa kuwashughulikia watu waliotufikisha hapa, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge katika hili tukubaliane katika mambo ya msingi kwa ajili ya Taifa letu, acheni ushabiki wa kivyama, kila mtu ameletwa hapa kwa maslahi ya wananchi wake na tuna wajibu wa kujibu tulichokifanya tukiwa huku Bungeni, hii ni nchi yetu sote yakiwa mazuri ni ya kwetu, yakiwa mabaya ni yetu sisi sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine katika hilo suala la kiwanda cha Urafiki; tumeenda kiwanda ni kichafu, China wanasema wanataka kukifanya soko walete vitu vyao hapa wamalize wao, sisi tubaki kama watazamaji na bidhaa feki, ndiyo maana leo zimeingizwa simu chafu na simu feki nchini. Badala ya kuzungumza ni Sheria gani inaruhusu kuingiza tunazungumza kwenda kuwanyang'anya Watanzania zile simu! Tudhibiti kwanza uingizwaji wa bidhaa feki, lakini siyo kuja kumuumiza mwananchi ambaye uliingiza bidhaa halafu yeye amenunua unamhukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ambalo nataka kusema katika hili, ni suala la Wanyamapori, kwa sababu tunazungumza habari ya utalii, lakini hatuzungumzi habari ya mwananchi anayekaa na wale wanyama anafaidi nini katika rasilimali ya Taifa lake. Leo wanyama wanavamia mashamba, leo wanyama wanavamia watu, hivyo wananchi hawaoni faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri katika hili na katika Bajeti yake, kwa kweli tuoneshe mazingira ya kwamba, wananchi wale wanaokaa karibu na Hifadhi za Taifa wananufaika zaidi katika mapato yanayopatikana ili wao wenyewe washiriki kulinda rasilimali za wanyama wale waliopo kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wananchi wenyewe hawaoni faida ya wale wanyama wanaona kama ni kero, kwa kweli tutaendelea kupata shida na Hifadhi zetu hazitakuwa na tija kwa sababu wananchi wenyewe hawaoni manufaa ya yale maeneo ambayo wao yanawazunguka kwa ajili ya mapato ya maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la mwisho ni viwanda. Tumezungumza habari ya viwanda vyetu nini kiliviua. Mfano, tulikuwa na Kiwanda cha Nyama Simanjiro, lakini siasa iliua kile kiwanda, watu mia sita wakaacha kazi kwa sababu siasa ziliingia, kiwanda kikaonekana mtu ana *interest* zake za kisiasa ikaua. Kama hatutadhibiti mwingiliano wa siasa na rasilimali za Taifa letu kwa kweli hatuwezi kusonga mbele na siyo mashindano ya

kutumbua majipu iwe ni mashindano ya kuwaelekeza wananchi wetu waende katika maslahi na haki. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mtu anataka kumfukuza mtu kazi, tunatengeneza Taifa la waoga ambao watumishi wetu hawatafanya kazi kwa uhuru na ndiyo tunawategemea kuzalisha katika nchi yetu. Wabadhilifu washughulikiwe lakini tusishindane kufukuza watu kazi, tushindane kuwaelimisha watu wetu, tusiwaoneshe dunia kwamba Watumishi wa Umma na Wataalam wote ni wezi. Tukijenga sura ya Taifa letu hivyo, tutaonekana watu wote ni wendawazimu. Haiwezekani siyo kila Mtumishi wa Umma ni mwizi kwenye nchi yetu, siyo kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila mtu anafukuza wengine wanafunga kiwanda huku, mwingine wanafunga geti huku, mwingine anafanya hivi huku, *what kind of that* nchi? Utawala wa Sheria uko wapi katika hilo? Tunatamani nchi yetu watumishi wapewe nafasi ya kufanya kazi na kuonesha matumizi ya taaluma zao walizosomea ili nchi yetu isonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mbunge aliyeiandika hii bajeti, wameandika wataalam, sasa kama tunawa-*discourage* Mawaziri wanasema tunarekodiwa, wanaogopa kusema hii bajeti haitoshi nchi haiwezi kusogea. Kwa mfano ameonesha mtu mmoja, Waziri wa Ardhi ameonesha kuthubutu na nampongeza na nitaendelea kumpongeza kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na watu wachache wanaothubutu kuwasaidia Watanzania kwa sura hiyo tutaacha alama ya utumishi kwenye Taifa letu. Kwa nini leo tuzungumze habari ya maadhimisho ya Sokoine, habari ya Nyerere kwa nini sisi tusiache *legacy* kwenye Taifa letu, tukaacha siasa tukaenda kwenye mipango inayotekelezeka kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutajenga utaratibu huo wa kupokea ushauri wa kitaalam kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu tutaendelea kusema haya na nawaambia hamtatekeleza kama hamtaweka *priority* ya vipaumbele vichache na kutoa vikwazo vilivyoua viwanda vyetu na kuwapa wataalam nafasi ya kutumikia Taifa lao, kuliko kufanya kila jambo siasa. Kama kuna mambo ambayo Rais anasema yanawezekana na hayawezekani tumwambie hayawezekani *professionally*, hili haliwezekani! Twende kwenye yale mambo ya msingi ambayo hata taaluma inaruhusu kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kusema tunajenga reli, tunasema tunajenga viwanda, tunatoa elimu bure kwa wakati mmoja kwa uchumi wa nchi yetu ambayo tunasema tunakusanya trilioni moja kwa mwezi, mara miezi kumi na mbili, trilioni kumi na mbili, lakini tunataka tujenge reli ya trilioni 300 na

kutoa elimu kwa trilioni tano mpaka sita, hiyo hela itatoka wapi? *it is impossible* tuwe na *priority* ambazo tunatekeleza, tukasema jamani *we have done this,* kuliko kuwa na vipaumbele mia mbili halafu Wabunge hapa tunapiga makofi. Tunawaambia Serikali tengeni vipaumbele vichache ambavyo vinatekelezeka kwa ajili ya maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaaendelea na wachangiaji wawili tu kwa muda tuliobaki nao Mheshimiwa Ali Salim Khamis na mwisho atakuwa Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Khamis!

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii kuweza kutoa mchango wangu. Kwanza nitangulie kwa kusema kwamba kutenda inatoka moyoni na haitoki mdomoni. Sasa nijikite katika huu Mpango na nimsaidie Kaka yangu hapa Waziri wa Fedha pengine inaweza ikasaidia ili kulivusha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoangalia katika kulinyanyua Shirika la Ndege la *Air* Tanzania, Waheshimiwa Wabunge Shirika la *Air* Tanzania ni Shirika la mwanzo Afrika Mashariki na nchi zote za Afrika Mashariki zinalitegemea shirika hili. Hatujui kilichosibu ni nini mpaka leo tumekuwa wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Shirika hili kufa, sijui hawa ambao walishiriki kulisababishia shirika hili kufa walichukuliwa hatua gani na mpaka leo hii inaonekana kwamba upo umuhimu wa kulihuisha shirika hili tena jambo ambalo mimi siamini kama tuna uwezo kwa sasa hivi kulihuisha Shirika la Ndege la *Air* Tanzania eti tu kwa sababu tutanunua ndege tatu siyo kweli. Ikiwa hakuna hatua ambazo tumezichukua wakati shirika limekufa, leo hii tuchukue hatua ya kulifufua shirika hili siamini mpaka sasa hivi na sijui kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha wataalam wako wamekushauri sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, ukiangalia leo *Ethiopian Airline* hawakukurupuka tu kuanzisha Shirika la Ndege, walitafuta wataalam ambao ni wazoefu wa kuanzisha Mashirika ya Ndege. Ukiangalia *Emirates Air* hawakuanzisha tu shirika kwa sababu walikuwa na pesa, lakini walitafuta wataalam ambao wana fani ya kuanzisha mashirika ya ndege, ndiyo maana leo wamefanikiwa. Leo tunakwenda katika ushindani wa kujenga shirika la ndege, majirani zetu Ethiopia ambao tumewasaidia siku nyingi mpaka mwaka jana wana ndege 76 na wame-*order* ndege mpya 46 ili kulihuisha shirika zikiwemo ndege za *Air Bus.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui manufaa ya hizi ndege ambazo zitanunuliwa na Serikali zije ziwanufaishe wananchi, imani yangu kukuomba Mheshimiwa Waziri ungerudi tena ukafanya utafiti kabla ya fedha hizi za umma hazijapotea.

Leo ukiangalia shirika hili lina madeni chungu nzima, na ikumbukwe kwamba shirika hili ni Shirika la Tanzania, ikiwemo na Zanzibar, Zanzibar imechangia asilimia kubwa ya shirika hili na ukiangalia katika takwimu ndege ambazo zilikuwa zikimiliki shirika la *Air* Tanzania nyingi zimenunuliwa na Serikali ya Zanzibar, lakini matokeo yake fedha hizi zote zimepotea na hakuna hatua ambazo zimechukuliwa, sasa tusitegemee kwamba shirika hili litahuika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba fedha za wananchi zisitumike kununua ndege, watu wakafanya haraka kununua ndege, watafutwe wataalam ambao wanaweza kushauri ili kuanzisha shirika litakalokuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa shirika la *Precision Air,* tulitegemea kwamba lile shirika litakuwa ni Shirika la Tanzania japo kuwa la wazalendo, lakini matokeo yake lilipoanza kufanya kazi vizuri Kenya *Airways* wameanza kulimiliki hili shirika, asilimia 51 sasa hivi iko Kenya *Airways* badala ya *Precision Air*, matokeo yake ni nini? Hili shirika maana yake tena sasa haliendi kuwa Shirika la Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri ungetafuta watu ambao wana fani hii ya kuanzisha mashirika ya ndege ili zikitumika fedha za umma, zitumike kwa mantiki ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niongelee katika masuala ya utalii. Mheshimiwa Waziri umetuletea kitabu chako hiki cha Mpango. Ukija kwenye ukurasa huu wa 14, unaelezea suala zima la utalii. Kutoka mwaka 2010 mpaka 2014, kumekuwa na ongezeko la watalii kutoka 784,709 na mpaka mwaka 2014 tumepata watalii 1,142,217, maana yake ni ongezeko la watalii 357,508 kwa muda wa miaka minne. Kwa hiyo, ukigawa hii kwa *ratio* ya miaka minne maana yake Tanzania tunapata watalii 89,000 kwa wastani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize vivutio vya utalii tulivyonavyo, hivyo kweli sisi tulileta watalii 89,000 kwa mwaka mzima? Hii Wizara inafanya shughuli gani, Bodi ya Utalii inafanya kazi gani. Ikiwa leo hii inaonesha pato la nchi hapa lilivyoongezeka kupitia hawa watalii, 357,000 kutoka dola milioni 1,254,600 mpaka kufikia dola 2,006,000, ni tofauti ya dola 1,880,599, hili ni ongezeko la pesa za kigeni kwa watalii 357,000. Je, Mheshimiwa Waziri hukuliona hili, kwamba hili ni eneo ambalo lingeweza kusaidia nchi yetu kuweza kupata mapato zaidi na kuweza kwenda huko tunakotaka kujitegemea katika huo uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia suala la bandari, Mheshimiwa Waziri bandari ndiyo uchumi nchi, Dubai, Hongkong wanafanya jeuri ya fedha kwa sababu ya bandari. Leo bandari zetu ukienda katika hii bandari ambayo

unaambiwa inaimarishwa ya Dar es Salaam bado, bandari ambayo inaweka msongamano wa mizigo mpaka inakuwa watu kuchukua mizigo yao badala ya kwenda kufanya biashara wapate faida, sasa wanakula hasara kwa sababu ya mizigo inayorundikana katika bandari moja ya Dar es Salaam na kuchelewa kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiangalia hiyo Reli ya Kati, imeanzia katika Bandari ya Tanga lakini Bandari ya Tanga haishughulikiwi imeachwa hivi tu na wala haimo katika Mpango. Bandari ndiyo shingo na roho ya uchumi wa nchi, leo inaachwa Bandari ya Tanga inakufa na Bandari ya Mtwara tunaenda kujenga Bandari ya Bagamoyo. Hivi tutegemee kweli huu uchumi wa viwanda utakua na wakati bandari ya Tanga ina miundombinu ya reli kutoka bandarini kwenda sehemu nyingine, leo tumeua kila kitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui, napata mashaka kwamba kweli tunaweza kufanikiwa kwenda katika uchumi wa kati kupitia viwanda ambavyo tunategemea kwamba viwe mkombozi wa nchi hii. Nina imani kama kweli unajenga ile dhana ya kiuchumi, basi naomba ufahamu kwamba bandari ndiyo uti wa mgongo wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uvuvi, miaka iliyopita michache tu, Mheshimiwa Rais wa sasa alikuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alikamata meli hapa, meli ile ilikamatwa ina samaki wa bahari watupu, baada ya kuwakamata hao watu na meli kukamatwa kupelekwa Mahakamani haikuonekana kwamba kuna umuhimu, kwa kuwa bahari yetu ina samaki wa kutosha, sasa tuwekeze katika uvuvi ili pato la nchi yetu liongezeke. Ndiyo maana nimetangulia kusema kwanza kwamba kutenda inatoka moyoni siyo kwa mdomo, sasa ikiwa hali hii tutakwenda nayo hivi, tutazungumza haya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nimesafiri nimepitia uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam kulikuwa na mvua, uwanja wa *International Airport* unavuja, sijui kama Waziri mhusika kama ameenda kutembelea pale, nenda ushuke pale eneo la abiria mtu anashuka kwenye ndege ya *Emirates* au *Etihad,* ama *Qatar* eneo la kushukia abiria hakuna feni, hakuna *air condition,* watu wanatoka majasho sasa ni *impression* gani ambayo unampa mgeni anaingia ndani ya nchi yako, anakuona wewe ni mtu wa aina gani? Hii ndiyo taswira ambayo tunawapa watu wanaoingia hapa kwamba hawa watu wenyewe ni wa hovyo hovyo tu, kila kitu chao wameweka hovyo hovyo tu, lazima wewe atakudharau mwanzo tu anapofika akiona hali kama ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo *International Airport* inavuja, wageni wanafika pale *airport*, maana yake ingekuwa angalau kuna mafuriko, uwanja umejaa maji sawa, Lakini leo mvua ya kawaida tu uwanja unavuja! Sijui kama

Waziri amewahi kwenda kwenye eneo la abiria wanaposhuka kwenye uwanja wa ndege, kutoka katika safari zao nchi za nje ili aende akashuhudie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru. Mheshimiwa Bashe!

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutupatia fursa sote kukutana katika kikao hiki, lakini nitumie nafasi hii vile vile kumpongeza na kumtakia kila la kheri Rais wa Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu niseme ujumbe mmoja kuna *popular speech* aliwahi kuitoa Baba wa Taifa Mkoani Tabora, ambayo alikuwa anazungumzia historia na hadithi ya vijana wanaokwenda kuchumbia kwa binti mzuri lakini wakawa wanazomewa zomewa ukigeuka unageuka jiwe. Kwa hiyo, nimwombe tu kelele nyingi zinaweza zikawepo, asikubali kugeuka jiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa masikitiko, masikitiko yangu ni kwamba, ni aidha kuna *disconnection* kati ya *vision* na mwelekeo wa Rais na walio chini wanaoandaa Mipango mikakati kufikia *vision* hiyo. Jambo la kwanza ambalo naona wengi wetu tunaimba viwanda, viwanda, tunasahau kwamba viwanda ni matokeo ya *efficiency* ya sekta zingine, ndiyo tutapata viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *nature* ya nchi yetu hakuna viwanda kama sekta ya kilimo haitopewa kipaumbele kinachostahili, hakuna viwanda kama sekta ya usafirishaji haitopewa kipaumbele kinachostahili na nianze kuwaambia Wabunge wenzangu tunaosema reli ya kati tunapongeza, hakuna reli ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu hiki nendeni ukurasa wa kumi na saba mkasome, naomba ninukuu *construction of new Central Railway Lane to standard gauge,* ukienda chini sehemu inayosema *this project is facing number of challenges as follows.* Kipengele namba tatu, *the choice of route* that is Dar es Salam, Tabora, Kigoma with *branches* to Tabora Mwanza, and Kaliua - Mpanda, Dar es Salaam – Isaka – Kigali – Keza - Msongati *has not been decided, and this is the railway we want.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutaki *railway* ya *project ya ADB,* inayotoka Dar es Salaam kwenda Isaka, kwenda Keza, *this does not help this country* na niwaombe wenzangu wa Kanda ya Ziwa na Mikoa inayopita reli, hakuna reli yetu, haipo! Hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimesoma Mpango wa Serikali, Mpango wa Mwaka Mmoja unatokana na Mpango wa Miaka Mitano. Serikali inataka kufufua *General Tyre,* mmeshafanya *study* kujua kwa nini *General Tyre* ilikufa, *you are going to allocate two billion shillings* kwa ajili ya *General Tyre*.

Swali la kujiuliza hii *General Tyre* ni wangapi wamewekeza, nendeni kwenye rekodi *NSSF* iliwekeza *nine billion shillings* imeshindikana kufufuliwa kile kiwanda, leo mnapeleka fedha za walipa kodi kwenda kuwekeza kwenye *dead project* lakini *study* zipo, wamekuja wawekezaji na Waziri Mwijage anajua, wameomba wawekeze *sixty billion shilling*s kwa ajili ya kufanya *investment* kwenye kile kiwanda, leo mnataka kuchukua fedha za umma kuweka hapo, *this is wrong thinking*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunawekeza *ATC*, hebu jamani tufanye *study airline industry*, Kenya *Airways* ambayo *partner* wake ni *KLM* mwaka jana wame-*register two million U.S dollar loss*. *South African Airline* kila mwaka inapoteza *one million U.S dollar*, sasa hivi wanataka kuunganisha *Airlines* tatu ku-*streamline operation* zao, sisi *ATC* toka Mwalimu Nyerere, kaja Mzee Mwinyi, kaja Mzee Mkapa, kaja Mzee Kikwete tumeshindwa ku- *revive!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Serikali fedha za umma kupeleka kununua ndege *is wrong direction,* lazima tufanye *business sense decision* siyo kila maamuzi jamani ya kisiasa. Hizi ni fedha za walipa kodi, fedha hizi tuzipeleke kwenye huduma za jamii, fedha hizi tuzipeleke kwenda ku-*revive Textile Industry*, Mwigulu hayupo hapa, yupo nimemuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Mpango wa Mwaka Mmoja, ukisoma Mpango wa Miaka Mitano, hapa wanazungumzia *C to C* na hakuna *strategy*, wanaelezea tu *cotton to clothes,* hawasemi wanafanya nini, *there is no investment* kwenye *cotton*. Niwaambieni watu wa maeneo tunayozalisha pamba hakuna *investment* kwenye Mpango wa Miaka Mitano, hakuna *investment* kwenye Mpango wa Mwaka Mmoja. Hatuwezi ku-*revive* uchumi wa nchi hii kwa kwenda kuwekeza kwenye mpunga, Serikali inatenga fedha kwa ajili ya mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Mwigulu, nimekutana nae *private as my brother and friend,* nchi hii tunazalisha mazao mengi fanya *strategic decision*. Mazao mengine waachie *District Commissioners* mahindi, mchele, mbaazi, mananasi tuwaachie kwenye Wilaya. Chukua mazao ya msingi, chukua *cotton*, chukua kahawa, chukua korosho, chukua katani, chukua tumbaku, mazao haya yata-*turn around* na kumsaidia Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mwijage kuweza kufanikisha wazo la kuwa na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili ufugaji, na-*declare interest* mimi ni mfugaji, tunajadili kama ufugaji ni jambo la ajabu, mkulima leo akilima heka mbili mwaka kesho akalima heka tatu tunasema *growth*, mfugaji akiwa na ng'ombe tatu zikafika saba anaharibu mazingira!

Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuwa na mifugo mingi baada ya Ethiopia. Kwa mwaka 2015 Ethiopia kwa *tannery industry* imewaingizia *five hundred million US dollar,* leo Kenya wanajenga kijiji cha viwanda vya ngozi, *raw material* yao sehemu kubwa wanachukua Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *what is the plan*? Ukisoma kitabu cha Miaka Mitano Mpango kinaelezea tu tokea tulivyoanza kuzalisha ngozi mpaka tulipofeli, hamna mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna umuhimu na mimi nashauri kwamba, kwa kuwa tunataka kujenga viwanda kwanza tukubali kwamba viwanda ni matokeo, ni *efficiency* ya *agro sector* ni *efficiency* ya *energy sector*, ni *efficiency* ya Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Mheshimiwa Ndalichako, ni *efficiency* ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Profesa Mbarawa, ndiyo tunampata Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mwijage! *There is no miracle*, hakuna muujiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda pale Mkoa wa Tabora tunalima tumbaku na wakulima wa tumbaku wapo, wanafahamu utitiri wa kodi *intermediaries* wamejaa kati ya mkulima na mnunuzi kila *intermediaries* hapa anavuta kidogo mkulima anabaki maskini. Nimeona kwenye Mpango tunazungumzia *special zones* ambazo tutaweka *either* viwanda, sijaona Tabora, Tabora tunazalisha tumbaku haijatajwa, ningemwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango na Dada yangu Mheshimiwa Ashatu... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tunakushukuru kwa mchango wako mzuri, nilifanya makusudi kukuweka wa mwisho kwa jioni ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, safari yetu ya jioni ndiyo imeishia hapa, nawashukuruni sana kwa michango yenu. Nina tangazo moja Wabunge wote ambao hawajajaza fomu za maombi ya kuchangia katika shughuli za bajeti mpaka mwisho wa kuhitimisha maombi ya Makadirio ya Matumizi kwa Wizara zote ama kwa mafungu yote mnaombwa mjaze fomu husika mkionesha *preference* zenu au chaguo lenu muoneshe majina yenu, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamepeleka fomu hizi lakini bila majina. Inakuwa vigumu sana kuandaa orodha hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, hilo ndilo tangazo langu la mwisho kwa leo. Baada ya kusema hivyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 21 Aprili, 2016 Saa Tatu Asubuhi)*